BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/ Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe.**	**Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe.**	**Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe.**	**Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/ Jimbo la Kiembesamaki**

12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/ Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara na Viwanda /Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati/ Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum / Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum / Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**

25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**

49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chake Chake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg.	**Raya Issa Msellem**	**-**	**Katibu**

Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 31 Mei, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa idhini ya Baraza lako Tukufu naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 110

Kukabidhiwa Majukumu ya Ugatuzi kwa Taasisi Husika

Mhe. Hidaya Ali Makame – Aliuliza:

Tangu utekelezaji wa Sera ya Ugatuzi uanze kumekuwa na changamoto kadhaa za utekelezaji moja wapo ikiwa baadhi ya shughuli zilizogatuliwa hasa kwenye Sekta ya Kilimo hazijakabidhiwa rasmi kwa Serikali za Mitaa ili waweze kuzitekeleza kwa ufanisi.

Je, kuna sababu gani inapelekea majukumu hayo kuchelewa kukabidhiwa rasmi kwa Serikali za Mitaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake Nam. 110 kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ikumbukwe kwamba kuanzia Julai, 2017 serikali iliamua baadhi ya majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Serikali Kuu yahamishiwe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Majukumu hayo ni pamoja na Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi, Huduma za Afya ya Msingi pamoja na Elimu kwa Wakulima/Wafugaji (*extension services).*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ugatuzi wa majukumu unakwenda sambamba na rasilimali watu, fedha na vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu hayo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta ilianza utekelezaji huo hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, hatua ya mwanzo ilikuwa ni ya ugatuzi na majukumu na fedha na hatua ya pili ambako ndiko tunakoelekea tutapoanza mwaka mpya wa fedha wa 2018/2019 ni ya ugatuzi wa rasilimali watu pamoja na vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya hapo juu, hakuna majukumu yaliyochelewa kukabidhiwa kwa Serikali za Mitaa kwa kuwa maagizo hayo ya Serikali kuhusu majukumu yaliyogatuliwa tayari yalikwishatekelezwa. Jambo kubwa ambalo lilikuwa halijafanyika ni uhamisho wa watumishi kutoka Wizara za Kisekta na kukabidhiwa kwa Serikali za Mitaa ambako watawajibika moja kwa moja kwa wakurugenzi husika.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengine ambayo yamefanyiwa kazi katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 ni pamoja na kubainisha Sera na Sheria zinazopaswa kurekebishwa ili ziendane na matakwa ya ugatuzi na kutayarisha miongozo ya mipango, fedha na bajeti; kutayarisha mkakati wa mawasiliano na kukuza uelewa wa ugatuzi na kutayarisha miundo mbinu ya kitaasisi na majukumu yake.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona tena ukanipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa majibu yake haya, lakini pia nimuulize swali dogo katika majibu yake haya kasema kwamba hakuna majukumu yaliyocheleweshwa.

Mhe. Naibu Spika, majukumu yaliyocheleweshwa yapo, na mpaka sasa hivi baadhi yanaendelea kuwepo kwa hiyo hilo aliamini. Lakini hata hilo suala la uhamisho alilosema kwamba ndio lilichelewa nayo ni baadhi ya majukumu. Sasa kama wizara tayari tumeshapitisha bajeti hapa na tutaendelea na wizara nyengine ambazo tayari ziligatuliwa. Kwa sababu majukumu bado yapo ambayo hajakabidhiwa ni utaratibu gani utafanyika mpaka kumalizika kwa mwaka huu iwe tayari kimeshakaa kila kitu katika utaratibu wake na kazi zinaendelea kama kawaida. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuelewe jambo jipya siku zote haliendi kama vile ambavyo tunatarajia labda liende kwa *speed* tofauti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba nimerejea kusema hakuna kucheleweshwa ila tunakwenda hatua kwa hatua, lakini vile vile lieleweke kwamba hili ni jipya na kadri tutakavyokuwa tunaendelea kutakuwa kukibainika changamoto za hapa na pale, na pale ambapo zinabainika hizo changamoto serikali itaendelea kuchukua hatua kufanya mawasiliano. Vikao mbali mbali vitaendelea kufanyika ili kuona kwa namna gani tunaweza tukaona kwamba changamoto hizo haziturejeshi nyuma.

Mhe. Naibu Spika, lakini nifahamike tu kwamba jambo hili ni maamuzi ya serikali kwa hiyo kwa vyovyote vile itakavyokuwa tunaamini shughuli zetu hazitokwama wala hakutakuwa na mtu ambaye anaweza akakwamisha mpango huo wa serikali ambao umeainshwa na serikali. Kwa hiyo, kiufupi ni kwamba hatua zinaendelea kuchukuliwa na niamini kwamba jambo hili litakapofika Julai, 1 mwaka 2018/2019, naomba nikuhakikishie kwamba wale watumishi wote ambao wako kwenye sekta hizo tumeshawaainisha, tushaendelea kufanya nao kazi na nikuhakikishie kwamba kuanzia kipindi hicho tutakuwa tumekabidhiwa rasmi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kuniona, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yenye mzunguko naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza lenye kifungu (a) kama ifutavyo:

(a) Kwa kuwa ugatuzi ni jambo jema ambalo tumelifikisha hapa na umekiri kwa sababu Mhe. Hidaya Ali Makame kasema lipo tatizo na yapo matatizo na kwa kuwa Wizara ya Utumishi imeshindwa kubainisha wazi wafanyakazi wanaowapeleka hasa wa ugatuzi wa kilimo. Je, serikali ina mtazamo gani wa kuwabainisha wafanyakazi wale ili kusiwe na mishahara hewa hapo baadae.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba majibu ambayo tutaendelea kuyatoa si ya kuzungusha wala sio mzunguko. Lakini hata hivyo, bado naendelea kusema kwamba jambo hili tunakwenda hatua kwa hatua na ndivyo lilivyoratibiwa kwamba lifanyike hatua kwa hatua na hadi hivi sasa wizara inayohusika na utumishi haijashindwa kuwabainisha wale watumishi

ambao wanatakiwa waje katika sekta zetu. Isipokuwa ni zoezi ambalo linaendelea kufanyika na tumesema kwamba zoezi hili kwa kuwa tunahamisha wafanyakazi kutoka taasisi moja kwenda katika taasisi nyengine hili zoezi linahitaji umakini mkubwa. Kwa sababu lina *document* za wafanyakazi, lakini vile vile tunaangalia na mahitaji mengine ambayo tuna miundombinu na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba jambo hili hakuna taasisi ambayo imeshindwa kufanya wajibu wake na badala yake ni hatua kwa hatua ambazo ndio tunakwenda na pale tutakapokamilisha kwa mujibu wa ulivyosema nadhani Julai, 1 jambo hili litakuwa limefikia katika hatua nzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba nitoe majibu ya nyongeza kutokana na swali Nam. 110 ambayo yametokana na wajumbe walioiuliza. Kwanza, nataka Mheshimiwa kwa idhini yako nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ambayo ameyatoa katika kulieleza suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba katika suala zima la ugatuzi serikali iliweka mpango wa utekelezaji wa ugatuzi, mpango huo unaelekeza ni mambo yepi yatachukuliwa hatua mwanzo na yepi yatafuata baadae. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba katika mwaka wa fedha tunaoendelea nao hivi sasa yako mambo yalitekelezwa na serikali kwa maana mpango wenyewe kuanza kutumika kama alivyokwisha kueleza Mhe. Naibu Waziri. Katika mwaka huu wa fedha, fedha ambazo zilikuwa zinawahusu watumishi wote 9,710 tayari zimeshaingizwa kwenye bajeti yetu na Baraza hili la Wawakilishi limeshaziidhinisha fedha hizo.

Mhe. Naibu Spika, ifikapo tarehe 1 Julai, watumishi wote 9,710 watahamishiwa rasmi kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambao watakwenda kutekeleza majukumu ya ugatuzi. Kwa hiyo na mwaka huu wa fedha vile vile tutatekeleza suala la kuoanisha sera na sheria kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba zipo sheria na sera ambazo zinahitaji zifanyiwe marekebisho na mapitio ili ziendane na ugatuzi. Kwa hiyo, serikali katika suala zima la ugatuzi halikukurupuka ispokuwa limeweka mpango wa utekelezaji. Kwa hiyo, mwaka uliopita tumetekeleza kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, mwaka huu tunatekeleza, na mwaka huu pia tumeweka mpango mkakati wa kuzipitia sera na sheria za kisekta ili ziendane na suala zima la ugatuzi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Wizara wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutokutekeleza vyema nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Wizara ya Utumishi tayari imeshafanya wajibu wao wa kuwabainisha watumishi wote ambao wanagatuliwa, na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa hivi sasa inafanyakazi ya kupita kwenye vituo vyote vya afya, vituo vyote vya kilimo, skuli zote kujua walimu na watumishi walioko huko ili kujiepusha na ile orodha nitakayokabidhiwa ifikapo tarehe 1 tusije

tukawa na watumishi hewa. Kwa hiyo, sasa hivi ofisi yangu inafanya kazi hiyo kwa ajili ya kufanya uhakiki ili kuwajua wale waliopo na itakapofika ile orodha maana yake tutakuwa tumejiridhisha kama hakuna watumishi hewa. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kuniona kunipatia fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa majibu yao mazuri. Lakini wakati akijibu Mhe. Naibu Waziri alisema waligatua fedha kwa ajili ya wafanyakazi ambao wametangulia katika ugatuzi, lakini sasa wanataka kuendelea katika kugatua rasilimali watu.

Je, serikali imeandaa vipi utaratibu wa kuwa na ofisi za kutosha katika kuwaweka rasilimali watu wanaokusudia kugatuliwa ili ufanyaji wa kazi kiufanisi uweze kupatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kusema katika majibu ambayo yalifuatia au nimeanzia ni kwamba jambo hili tunalifanya katika umakini wa hali ya juu. Kuhusu rasilimali ambazo tumeshaanza kuzitumia hizo ni kwamba hatua nyengine ambayo tunayoendelea nayo moja na hilo katika suala la majengo au miundombinu yetu ya majengo tumeizingatia. Na ikumbukwe kwamba sasa hivi katika taasisi zetu tukipita katika baadhi ya maeneo tunaona marekebisho mengine yanaendelea kufanyika hatua kwa hatua ili kuonesha kwamba pale watendaji wetu hawa kwa kweli wengine tumeshapokea lakini na wale ambao watakapokuja tujue ni namna gani tunajipanga katika kuona kwamba hawatopata usumbufu katika kufanya kazi zao za kila siku.

Nam. 124

Ongezeko la Riba katika Benki za Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi wake imetoa fursa ya uanzishaji wa mabenki ili kutoa mikopo kwa wananchi kwa lengo la kujiendeleza kimaisha. Hata hivyo, riba zinazotozwa na benki hizo ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* ni kubwa sana.

(a) Je, serikali inalionaje suala hili la riba kuwa kubwa na kupunguza.

(b) Je, kwa mabenki ya binafsi kuna utaratibu wa sheria wa kuwapangia kupunguza riba.

(c) Je, kama mabenki ya binafsi hayataki kupunguza riba. Je, benki yetu ya *PBZ* inalionaje suala hili la kupunguza riba.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake Nam. 124 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Kimsingi Benki za Biashara hufanya biashara ya fedha ikiwemo kukusanya amana, kuwekeza katika maeneo mbali mbali, kukopesha kwa watu wanaohitaji, lakini pia kununua na kuuza fedha za kigeni na kutoa huduma nyengine mbali mbali za kifedha. Na kiacha ada zinazotozwa kwa huduma, riba ni sehemu kubwa ya gharama ama inapokopa benki au inapolipa kwa amana za wateja. Na bei inakuwa bei pale inapokopesha. Kiwango cha riba kinachotozwa na benki hizo aghlabu huathiriwa na mambo manne.

La kwanza, wingi wa fedha zilizopo kwenye mzunguko *money circulation*. Lakini la pili, kiwango cha mahitaji ya fedha hizo hususan kwa njia za mikopo *demand*. La tatu, gharama za upatikanaji wa fedha ikiwemo riba inayotozwa kwa benki hizo na kukopa. Nne, kiwango cha riba kinachotozwa na Benki Kuu kwa benki za biashara na uwezekano wa mikopo kutolipwa na gharama nyengine za uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla kiwango cha riba kinachotozwa na benki hizo kinategemea mwenendo wa soko la fedha, kwa maana upatikanaji wa fedha lakini vile vile mahitaji *(demand)*. Serikali haina utaratibu wa kupanga kiwango cha riba ya kutozwa na Benki ya Biashara.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali inaelewa mwenendo wa kiwango cha riba na inafuatilia kwa karibu utendaji wa soko la fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*).

(b) Mhe. Naibu Spika, hakuna utaratibu wa kisheria wa kuwapangia, kupunguza au kuongeza riba kwa benki binafsi; na

(c) Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) nayo ni Benki ya Biashara na inaendesha shughuli zake katika mazingira yale yale ya soko la fedha, na kwa namna hiyo haitamudu kutoa huduma zake kwa kiwango tofauti na riba inayotozwa na benki nyengine za kibiashara.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini na mimi najaribu kuongeza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kila mmoja anafanya biashara, lakini biashara kama biashara inategemea sana na mfanyabiashara mwenyewe. Kwa hali ya kwetu kwa biashara zetu hasa

nikisema kwa upande wa Zanzibar, kama yeye ikiwa ni dhamana wa Wizara ya Fedha na Mipango, wananchi huwa wanategemea sana benki kwa ajili ya kujiendeleza.

(a) Je, haoni kwamba kiwango hicho ambacho sasa hivi, inawezekana kuanzia asilimia 20 au 18 ni kikubwa kulinganisha na mahitaji ya Wazanzibari kwa mikopo.

(b) Ni mara nyingi hapo nyuma benki zilikuwa zina *amount* kubwa zaidi ya hiki kiwango cha asilimia 18 pengine, ilikuwa asilimia 22, 21 au 20, lakini wakashusha mpaka asilimia 18. Je, mara ya mwisho amefanya mazungumzo na wenye benki ikiwemo benki yake, ili kuwapunguzia wananchi riba.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Nitaomba kuyajibu kwa pamoja kwa sababu yanalingana.

Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba huko nyuma benki zilikuwa zinachaji viwango vya juu, nyengine zilikuwa zinachaji *rate* ya asilimia 21 na nyengine mpaka asilimia 22. Ni kweli vile vile kwamba zipo benki hivi sasa zinafikiria kupunguza na nafikiri zipo karibu benki tatu ambazo zimeshaonesha nia ya kupunguza ama zimeshapunguza kabisa. Nazo ni *NBC, National Microfinance Bank* na *CRDB.* Hizi zimepunguza viwango na ziko katika *rate* ya asilimia 16. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini kama nilivyosema katika jibu mama kwamba hii *rate* inategemea na hali ya mzunguko wa kifedha uliopo nchini, lakini vile vile mahitaji, hili ni soko kama soko la bidhaa nyengine linategemea *demand* na *supply* na hiyo ndio inayo-*determine* bei kwa maana ya riba. Kwa vile soko sasa linatengamaa na bei zinashuka na benki ya *PBZ* nayo inazingatia suala hilo na inatarajia kushusha kiwango cha riba ndani ya mwezi Juni mwaka huu kutoka asilimia 18 mpaka asilimia 16.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango juu ya takwimu zake ambazo mabenki ya watu binafsi kama *NMB, CRDB* na mengineyo kama nimesahau wamepunguza kiwango cha asilimia 16. Lakini na yeye kwa bahati nzuri Mhe. Waziri ametwambia *PBZ* imo katika mipango ya kuhakikisha kwamba itashusha kiwango hicho hicho kulingana na hali inavyokwenda. Pamoja na hiyo, nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba wazo hilo ni zuri lakini namuomba lisipotee kwa sababu likiondoka hilo haoni kwamba kama haikupungua riba wateja wengi watakimbia na kukimbila benki hizo kukopa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba tayari Benki ya Watu wa Zanzibar imeshazingatia na tayari uamuzi umeshafanyika, na kuanzia mwezi Juni *rate* itakuwa asilimia 16. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuweza kuniona ukaweza kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kujibu vizuri swali hili kwa mbwembwe kabisa.

Vile vile naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulifanya jambo hili ili wananchi waweze kupata huduma kama vile kuweza kupata kupitia kulipa kodi, lakini kupata mshahara na mambo mengine. Kwa kuwa Wilaya ya Micheweni ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeachwa nyuma kuweza kupatikana huduma hii. Je, ni lini Wilaya ya Micheweni itafikiriwa kuweza kupata huduma hii ya kibenki.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwanza ni utaratibu wa benki yoyote ile ikiwemo ya *PBZ* kuhakikisha inapata wateja wengi zaidi. Kwa hivyo, suala la ku-*cover* maeneo yote nchini ni suala ambalo linapewa umuhimu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kwa sasa hivi na kwa vile teknolojia imekua, huduma hizi zinatolewa kwa njia nyingi. Kuna huduma ambazo zinatolewa ama kwa kufungua tawi katika eneo, lakini na katika kufungua tawi hilo kutategemea pia lazima ziwepo *factor* ambazo zitapelekea benki kuamua kufungua tawi hilo, kwa maana idadi ya wateja ni moja ya *factor* hiyo.

Lakini huduma nyengine zinazotolewa ni kupeleka *ATM* katika maeneo hayo, vile vile huduma ambazo sasa benki wanazitoa ni *internet banking* kwa kutumia *internet*, kwa hivyo lazima watu waeleweshwe. Lakini hata kutumia huduma hizo kwa kutumia simu zao za mkononi. Benki inaendelea kutoa taaluma ili wananchi waweze kutumia huduma hizo katika mitandao, hiyo itawarahisishia, vile vile itawa- *facility* kupata hizo huduma zinazotolewa na benki.

Kwa hivyo, Micheweni ni moja ya eneo hilo, kama hakuna tawi na halipo kwa sasa hivi, lakini *ATM* ni moja ya njia ambazo zitaweza kuwafikishia huduma hizo wananchi wa eneo hilo, lakini vile vile taaluma itatolewa ili waweze kutumia huduma za kifedha kama M-Pesa na Ezy-Pesa, hizo ni huduma ambazo unaweza kuzipata sehemu yoyote nchini.

Nam. 135

Utaratibu Mpya wa Kuweka Namba za Gari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na utaratibu wa kuweka namba mpya za gari za abiria hasa zinazokwenda mashamba. Utaratibu wa zamani namba zinafuatana mfano namba 1 Mkokotoni, namba 2 Bumbwini, namba 3 Mndo, namba 4 Pwani Mchangani, namba 5 Ndagaa, namba 6 Chwaka, namba 7 Bweleo, namba 8 Unguja Ukuu, namba 9 Bwejuu, namba 10 Makunduchi, namba 11Binguni.

(a) Je, kwa nini utaratibu huu mwepesi wa kuweka namba za gari umeondoshwa na badala yake umekuja utaratibu mpya wa namba mpya na majina.

(b) Je, kwa nini utaratibu huu mpya wa kuweka majina ya maeneo hayo usibakishe nambari za asili kama zilivyokuwa zikifuatana na majina.

(c) Je, wahusika katika sekta ya usafirishaji abiria nchi kavu wanashirikishwa katika mabadiliko kama haya.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 135 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa zamani haukuondoka ila umeimarishwa zaidi kuendana na mazingira ya sasa.

(b) Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa sasa umezingatia utaratibu wa zamani kwa njia zote zilizokuwepo zamani, ila njia kuu zote zinazoingia mjini zimepewa nambari kama ifuatavyo;-

Njia nambari 1 ni gari zote zinazoingia mjini kupitia Bububu, hivyo gari iliyokuwa nambari 1 kwa vile inapitia njia nambari 1 inaandikwa 101.

Njia nambari 2 ni gari zote zinazoingia mjini kupitia Amani hivyo gari zinazopitia njia hiyo zitaanza na nambari 2 kama vile 204 Mchangani, 206 Chwaka.

Njia nambari 3 gari zote zinazoingia mjini kupitia Fuoni hivyo gari zote zinazopita njia hiyo zitaanza na nambari 3 kama vile 310 Makunduchi, 308 Ungujaukuu, 311 Binguni.

Njia nambari 4 gari zote zinazoingia mjini kupitia Kisauni kama vile 407 Fumba.

(c) Mhe. Naibu Spika, wahusika katika sekta ya usafirishaji wanashirikishwa katika mabadiliko yote yanayofanywa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

(a) Je, hamuoni kuweka manambari mengi ambayo watu hawayaelewi kwamba inaharibu utaratibu uliozoeleka na tunaharibu asili yetu. Ni sababu gani ya msingi iliyochukua hatua hiyo. Hilo moja.

(b) Je, kuna sababu gani ya kutokurudia uasilia wetu wa zamani, wengi tunaamini na mimi mmoja nikiwemo naamini kwamba namba za asili ziko vizuri kuliko za sasa na mila zetu na desturi zetu za Kizanzibari.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kilichotendeka hakuna kilichoharibiwa, isipokuwa tumetengeneza. Hizo namba hapo zamani zilipowekwa ziliwekwa na sasa hivi pia zimewekwa. Maisha yanabadilika na nchi inaendelea mabadiliko ni lazima, tuyakubali mabadiliko hayo kwa sababu tumeona kwamba ndio yenye tija kwa wale ambao wanalisimamia.

Mhe. Naibu Spika, mji sasa hivi barabara zake nne kuu ndio kuu ambazo zinazoingia mjini, kwa hivyo namba hizo zimepewa namba hizo na zitaendelea kuwa hivyo kwa sababu tumeona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bado swali la pili.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Nimeyajibu yote mawili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa ubadilishaji huu wa namba umewapa mzigo matajiri wa magari haya na madereva kwa kutoa fedha kuweza kubadilisha.

(a) Je, Mhe. Waziri haoni kama bado ukiondoa zao la karafuu linaloingiza mapato ya serikali ni magari haya ya abiria na mizigo.

(b) Kwa nini muda mwingi bei za mafuta zinapandishwa mara kwa mara, lakini bei za nauli za abiria hazipandishwi, ukitilia maanani wenzetu hawa tunawapa mzigo mkubwa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid maswali yake kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, gari zilizozungumziwa hapa ni gari za abiria na mizigo.

(a) Kuna magari ya mizigo tofauti na gari ya abiria na mizigo. Gari zilizozungumziwa hapa ni gari za abiria na mizigo na ndizo zinazopangiwa njia kwa ajili ya kuingia mjini kwa nambari hizo zilizopangwa. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hilo halizuii kufanyika hizo shughuli zinazofanywa na gari isipokuwa kufuata utaratibu ndicho kinachotakiwa.

(b) Mhe. Naibu Spika, bei za mafuta zinapanda lakini bei za gari hazipandi. Suala la mafuta kwanza haliko chini yetu wanapopandisha na kushusha, yako chini ya wizara zinazohusika. Lakini mabadiliko ya bei za gari huwa yanafanywa kila mwaka wakati wanapobadilisha leseni, na pale wanapoona inafaa kulingana na bei ya mafuta ilivyo basi wanapandisha. *(Makofi)*

Nam. 118

Umri Mdogo wa Wanafunzi Wanaomaliza Darasa la 6, 7 na 10

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza elimu na kufanya majaribio ya mitihani ili kuwapima wanafunzi uwezo wao kielimu, lakini kumekuwa na changamoto ya watoto wa darasa la sita (6) na la saba (7) na la kumi (10) wanakuwa na umri gani na kuwa hawana tena nafasi ya kuendelea wala hakuna muongozo wowote wa watoto wale.

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wanaotoka darasa la sita, la saba na la kumi kila mwaka.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuwawekea muongozo wanafunzi ambao hurudia mitihani.

(c) Huu mfumo wa elimu wa kuwatoa watoto darasa la 6, 7, 10 ambao bado ni wadogo na mawazo yao ni ya kitoto una manufaa gani kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 lenye vifungu (a), (b) na (c). kama ifuatavyo:

(a) Kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya mwaka 2006, elimu ya lazima itatolewa kwa watoto wa Zanzibar kwa miaka kumi na mbili hadi kufikia Kidato cha Nne. Hata hivyo, mwanafunzi yeyote ambaye hajafikia kiwango cha ufaulu katika mitihani yake ya Kidato cha Pili itamlazimu ajiunge na Vituo vya Amali kama atataka kuendelea na masomo. Hivyo, Darasa la Sita hakuna mtoto anayetoka ila wa Kidato cha Pili wako wanaotoka ambao hawajafaulu. Kwa mwaka 2017, jumla ya wanafunzi 46,580 walifanya mitihani na wanafunzi 34,458 walifaulu na waliobakia 12,122 hawakuweza kuendelea na masomo ya Kidato cha Pili.

(b) Wizara tayari imetoa muongozo kuwa wanafunzi wote ambao walifanya mtihani wa Taifa kwa ngazi ya elimu ya msingi na darasa la kumi mwaka 2017 na ambao hawakufikia kiwango cha ufaulu kinachotakiwa warudie darasa.

(c) Kwa mujibu wa mfumo wa elimu ya Zanzibar kwa mwanafunzi anayemaliza elimu ya msingi, yaani darasa la sita na ambaye amefikia kiwango cha ufaulu anaendelea na elimu ya sekondari, na ambaye hakufikia kiwango cha ufaulu kinachohitajika anarejea darasa. Kwa hali hiyo, hakutakuwa na mwanafunzi mdogo atakayetoka kwa kuwa hajamaliza elimu ya lazima. Kwa ambao wamemaliza Kidato cha Pili wana fursa ya kujiunga kuendelea na masomo ya ufundi katika vituo vya Amali kwa wanaotaka. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Katika majibu yake aliyoniandikia waziri ameniambia kwamba elimu ya mifumo ya Zanzibar ni mtoto mpaka afikie darasa la kumi na mbili ni elimu ya lazima. Leo darasa la kumi watoto wanatolewa wanaambiwa waende wakatafute mafunzo ya amali. Pia kuna watoto 12,000 ambao wanamaliza kila mwaka pengine na zaidi katika mfumo wa darasa la kumi ambao ni wadogo sana wa umri wa miaka 12.

(a) Mhe. Naibu Spika, mimi namuuliza Mhe. Waziri. Je, mfumo wa zamani uliuona haufai kwa nini, wakati wewe ni mmoja uliyefaidika na mfumo ule.

(b) Je, mfumo huu ambao tunao sasa hivi, tumeuiga nchi gani na tumefaidika nini au tuna hasara gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said maswali yake mawili kama ifuatavyo. Ni kwamba mfumo wa elimu duniani ni mfumo ambao unabadilika kulingana na mabadiliko ya haja, lakini pia mabadiliko ya sayansi na teknolojia, uchumi na mzingira mengine yanayofanana nayo. Kwa hivyo, hakuna mfumo wa elimu ambao umetulia duniani. Lakini hata hivyo, mabadiliko yaliyofanywa katika mfumo wa zamani wa elimu ulitokana na wadau wa elimu Zanzibar ambao ulishirikisha wadau wote, wanafunzi walishirikishwa, walimu walishirikishwa, viongozi wa elimu walishirikishwa, wananchi hata nyinyi wawakilishi mlishirikishwa kutoa maoni na ukaja mfumo huu ambao tunautumia sasa.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na kasoro nyingi au hitilafu nyingi katika mfumo wa zamani na hitilafu kubwa iliyotajwa ni kwamba vijana wetu wanamaliza elimu katika umri mkubwa sana kiasi kwamba wanapotaka elimu katika nchi nyingine inakuwa ni vigumu kuweza kupata kwa misingi ya umri. Wenzetu wanatoa elimu kwa misingi ya umri, ukifika umri fulani, elimu fulani, shahada fulani. Sasa mfumo huo umekuja kusawazisha suala hilo na niseme tu mfumo huu tupo katika hatua za utekezaji haujafikia *hundred percent* ni kwamba sasa hivi tumefikia kidato cha tatu mwakani ndio tutafikia kidato cha kumi na mbili na tutaufanyia tathmini mfumo huu kuona kwamba una faida gani au una hasara gani. Na tathmini hiyo inaweza ikatuwezesha ama kuendelea nao au kubadilisha kwa mujibu wa maoni ya wadau. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini ndani ya majibu yake alisema wanafunzi wale wa darasa la sita waliofeli wataendelea kurudia darasa. Mheshimiwa nilitaka kujua hivi sasa tuna tatizo la wanafunzi kurundikana katika madarasa jambo ambalo halioneshi kama linaleta ufanisi. Je, wale wanafunzi watakaofeli wakarudia darasa na wale wapya watakaoingia hivi sasa hawatoweza kuleta usumbufu zaidi na ikaweza kukosekana ufanisi wa kupasisha katika darasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba sasa hivi katika baadhi ya skuli kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi katika darasa, lakini pia msongamano huu hauwezi kutufanya kuwakosesha vijana wetu haki ya elimu, elimu ni haki ya vijana wetu. Lakini hata hivyo, juhudi nyengine za wananchi na serikali zinachukuliwa kwa kujenga madarasa ili kupunguza msongamano huu. Lakini hata hivyo, kwa upande mwingine wa kitaalam tumewawezesha walimu wetu kuwapa mafunzo ya kuweza kusomesha madarasa makubwa. Walimu wetu wamezowea kusomesha madarasa ya kawaida, lakini tumewawezesha kwa mafunzo mbali mbali ili kuweza kumudu kusomesha madarasa makubwa bila ya kuathiri ufanisi unaotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunakubaliana kwa upande mmoja kwamba darasa kubwa linaweza kuathiri matokeo ya wanafunzi, lakini pia tuna ushahidi wa madarasa madogo ambayo wanafunzi wanafanya vibaya vile vile, lakini hii hatuichukui kama ni moja ya kulala bila kuongeza idadi ya madarasa hapana. Lakini tuseme ufaulu wa wanafunzi unategemea mambo mengi sana si moja wala si mawili wala si matatu, inawezekana darasa likawa na wanafunzi kumi na tano na tunayo lakini yanafanya vibaya, na inawezekana wanafunzi wanasoma madarasa yana wanafunzi mia mbili wanafanya vizuri mfano Mtopepo na Kijitoupele. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe.Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba hata huu mfumo uliopo hivi sasa unaweza ukabadilika ikibidi kubadilika. Je, serikali haioni sasa ipo haja ya kuwaweka wataalam chini wakaja na mfumo mmoja ambao uta-*accomodate short comings* zote zile ambazo tunazo katika mfumo wetu ili kuwa na mfumo mmoja ambao utachukua muda bila kubadilika kwa sababu kubadilisha mifumo kila wakati tunawa-*confuse* watoto wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Wanu Hafidh Amer swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, baada ya mfumo wa aina yoyote kuwekwa mategemeo ni kwamba huwezi kufanyiwa kazi na hatimae huwezi kuleta matokeo yanayokusudiwa, haitegemei kwamba mfumo baada ya kuwekwa baada ya mwaka mmoja au miwili ubadilishwe itakuwa mfumo juu ya mfumo hakuna tija yoyote. Sasa ili kuondoa uwezekano wa mfumo kubadilisha mara kwa mara ndio maana kwamba katika zoezi hili huwa tunashirikisha wadau wote. Niseme kwamba mfumo huu uliwashirikisha wadau wote kwa kipindi kirefu kidogo, ulichukua mazoezi miaka miwili mitatu kuwashirikisha. Kwa hivyo, niseme kwamba katika ushirikishaji wenyewe na hao wataalam uliowasema walikuwemo na wakaja na mfumo huu ambao tunautekeleza. Lakini pamoja na hivyo kwa kuwa mfumo ni klitu ambacho kinawekwa na binaadam, wakihisi mfumo huo hauna tija basi wakati wowote unaweza kubadilishwa. Lakini nisisitize kwamba mfumo huu pia uliwashirikisha wataalam na kila aina ya mfumo unaofanyika basi wataalam wana sehemu yao. Ahsante sana.

Nam. 199

Uingizaji wa Vyakula Visivyo na Viwango Nchini

Mhe. Ali Suleiman Ali (Jimbo la Kijitoupele) - Aliuliza:

Hivi karibuni kumejitokeza baadhi ya wafanyabiashara nchini kuingiza vyakula visivyo na viwango kwa ajili ya matumizi ya binaadam na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. Kwa kuwa tatizo hili linaendelea kuwepo.

Je, wizara inachukua hatua gani za kisheria kwa wafanyabiashara hao.

Mhe. Naibu Waziri Wizara ya Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 199 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara na Viwanda imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba sekta ya biashara inaendelea kwa mujibu wa sheria na kanuni. Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013 imempa mamlaka Waziri wa Biashara na Viwanda kuhakikisha wanaoingiza na wanaosafirisha bidhaa kuingia kutoka nje ya Zanzibar wanapata kibali kutoka Wizara ya Biashara na Viwanda. Sheria hiyo imeeleza wazi kwamba bidhaa ambazo zinahitaji uangalizi wa serikali, bidhaa ambazo zinaruhusiwa kuingizwa ndani ya Zanzibar na bidhaa ambazo haziruhusiwi kuingizwa ndani ya Zanzibar kwa vile zina madhara kwa matumizi ya binaadam.

Mhe. Naibu Spika, taasisi mbali mbali hutumika kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa ndani ya Zanzibar zipo salama kwa matumizi ya binaadam miongoni mwa taasisi hizo ni kama vile *ZFDA*, na *ZBS*. Aidha, hatua mbali mbali za kisheria huchukuliwa kwa wafanyabiashara wa bidhaa ambazo zimegunduliwa hazifai kwa matumizi ya binaadam. Aidha, sheria hizo hutumika kutegemea na tatizo husika. Kwa mfano, bidhaa iliyokosa tarehe ya mwisho wa matumizi *(expire date)* bidhaa hiyo hairuhusiwi kuingia ndani ya Zanzibar. Bidhaa mbovu pamoja na zile zinazopigwa marufuku kuingia Zanzibar, bidhaa hizo huwa zinaangamizwa moja kwa moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza tukiri kwamba bidhaa nyingi zinazoingia Zanzibar hasa bidhaa za matumizi ya chakula kwa binaadam zinaingizwa mbovu. Jana kama tumeangalia televisheni tumeshuhudia shehena kubwa ya unga wa ngano pamoja na mchele umeingizwa mbovu. Swali langu lipo hapa Mheshimiwa.

(a) Je, bidhaa hii ikitoka huko inakotoka haina uangalizi wowote wa kutizamwa usalama wake.
(b) Kwa kuwa bidhaa hii ya chakula inapita katika bandari yetu na wataalam wako pale pale inakuwaje inapakuliwa kutiwa katika maghala wakati haifai.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar bidhaa nyingi zinazoingizwa si mbovu wala si bomu. Nina ushahidi ambao nataka kumwambia Zanzibar tumeunda taasisi mbili kuu nazo ni Taasisi ya Dawa, Vyakula na Vipodozi kazi yake ni kuangalia usalama wa chakula, lakini pia tunayo Taasisi ya Viwango ipo chini ya Wizara ya Biashara kazi yake kuangalia viwango.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli jana TV zimeonesha, lakini nataka kumwambia Mhe. Mwakilishi mpaka akaona TV zimeonesha hiyo ni kazi kubwa iliyofanywa na taasisi mbili za serikali, taasisi ya madawa ndipo yeye akajua. Huko zinakotoka kila dunia ina utaratibu wake. Kwa mfano, unapotaka kuingiza bidhaa kutoka nchi yoyote duniani, aidha bidhaa ile itakuwa imechekiwa katika ile nchi husika au itakuwa kuna sheria ambayo lazima bidhaa ile ichekiwe inapofika nchini.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile jana ameona kwenye TV ni wazi kwamba taasisi zetu mbili zinafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba bidhaa zinazoingia nchini zinakuwa nzima na ndio maana tukaweza kuzitoa. Hilo suala tunalijua na huyo mtu ukienda kuangalia ghala lake hapo lipo chini ya uangalizi wa polisi. Mhe. Naibu Spika, vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama huyo mtu vinamtafuta ameshakimbia. Kwa hivyo, suala hilo tunalo na tunalifanyia kazi kikamilifu. Mhe. Naibu Spika, hiyo ndiyo kazi ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Muongozo wako Mheshimiwa. Swali langu sikujibiwa ipasavyo. Kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, nimeuliza hivi kwa kuwa tuna waangalizi katika bandari yetu ya Zanzibar na bidhaa inaingia pale pale sijui ukaguzi wenyewe haukuwa sahihi au vipi inakuwaje zikapita bidhaa mbovu zikifika ndani ziangamizwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, mimi ni Naibu Waziri wa Wizara ya Biashara na Viwanda sihusiki na bandari, kwa vile sihusiki na bandari lakini nitamsaidia kitu. Pale bandarini kuna taratibu mbili, moja unakagua bidhaa ikiwa bandarini, lakini mbili bidhaa inaruhusiwa kutoka halafu inachukuliwa *specimen* inakwenda kukaguliwa. Sasa kilichotokezea imewekwa kwenye ghala mtu hajaruhusiwa kuiuza lakini ametaka kuiuza. Sasa uone umakini wa serikali ameshaitia ghalani hajaruhusiwa kuiuza ameweza kuiuza ndio maana tukamtia nguvuni na huyu mtu tunae na tunahangaika nae. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, huo ni umakini wa taasisi zetu mbili, Taasisi ya Dawa, Vyakula na Vipodozi na Taasisi ya Viwango ambayo ipo chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri mtoto wa mkulima na mkwezi. Lakini mbali na majibu haya kama tulivyoona jana katika vyombo vya habari na bahati mbaya unga ule na mchele ule umesambazwa ndani ya majimbo yetu yaliopo katika mji wa Zanzibar, na kwa kweli unga ule haufai na mchele ule haifai. Na kwa vile viongozi wetu na sisi tukiwa kama viongozi na wafanyabiashara ambao wanawapenda wananchi wao ni wa kizalendo, huwa tunatoa sadaka katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Sasa kutolewa kwa unga na mchele ule umeleta taswira mbaya kwa nchi yetu. Je, serikali ina tamko gani hasa kuhusiana na mfanyabiashara huyu ili kuwa komesho kwa wafanyabiashara wanaotoa vyakula vibovu hususan katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nampongeza sana Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuonesha umahiri na kuwapenda wananchi. Naomba kumjibu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawapenda wananchi zaidi na ndio maana ukaona mtu huyu narudia tena kusema, tumetoa katika vyombo vya habari huo ni ujasiri wa serikali kuona hili suala tunalijua na tunalifanyia kazi na huyu mtu tunamtafuta ameshakimbia. Vyakula vyengine alikwenda kuvitupa Kibele kwa sababu vime-*expire*. Tunamtafuta hatujamuona ameshakimbia nchini na vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya kazi nzuri ya kumtafuta. Mheshimiwa ninachotaka kumwambia ajue kwamba mpaka yeye kaona kwenye TV ni kwamba serikali inafanya jukumu lake ki-*haki lillah taala* la kuwalinda wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumwambia serikali ina taasisi mbili, Taasisi ya Viwango na Taasisi ya Dawa, Vyakula na Vipodozi. Taasisi hizi zinafanya kazi nzuri na mfano nakupa, kuna kontena tano zipo bandarini zimekuja na mafuta zimeleta mafuta ya gari ya *holex*, mafuta ambayo hayana viwango tayari tunayo. Kuna vitu vingi tumeona ushahidi taasisi mbili hizi zinafanyakazi ukiangalia TV siku zote vitu vinakuwa *destroyed*, vinachomwa kwa sababu serikali inafanya kazi, taasisi inafanya kazi, zinafanya kazi kuhakikisha tunawalinda wananchi wetu. Ahsante.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali yangu (a) na (b) ya nyongeza. Taasisi za serikali tatu zipo pale bandarini zinafanyakazi ya ukaguzi, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Biashara na Viwanda. Lakini kwa bahati mbaya biashara hizi zinafika mpaka mitaani zikiwa zimeharibika. Je, serikali haioni kama wanaokaa pale hawafanyi vizuri na hatua gani ambayo inachukua.

Lakini swali langu (b) kwa miezi mitatu bidhaa zilizokamatwa hapo bandarini ni hatua gani zilizochukuliwa na wahusika ni kina nani na nani ambao wanatuletea biashara mbovu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo. Anasema kwa miezi mitatu, au la mwisho kwamba kuna bidhaa zipo bandarini. Mheshimiwa kuna utaratibu mmoja baada ya taasisi hizi kugundua bidhaa hizi hazifai kuingia nchini taratibu mbili tunazichukua. Taratibu ya kwanza kuhakikisha kwamba bidhaa iliyoingia nchini na haina viwango au haiko salama ni kuirudisha nchi iliyotoka. Kwa maana yale makontena yaliyoko bandarini ya bidhaa ambazo hazifai tunataka kuzirudisha kwa sababu kama tutazi-*destroy* sisi inaingia *cost.* Au bidhaa nyengine tunazozi-*destroy* zinakuwa zina mambo ambayo hayafai kuingia katika ardhi yetu. Kwa hivyo, makontena yale tunataka kuyarejesha katika nchi yaliyotoka na ndio maana yako pale.

Lakini swali jingine anasema kuna taasisi tatu zipo bandarini, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya na Wizara ya Biashara na Viwanda. Mhe. Naibu Spika, kila bandari duniani taasisi hizi lazima ziwepo katika kuhakikisha na kulinda wananchi wake kwa vyakula vinavyoingizwa, dunia nzima taasisi hizi bandarini zipo. Sasa uwepo wake pale ni *standard* ndio matakwa ya bandari katika *standard* za dunia na zinafanya kazi yake.

Naomba kusema tena hata kama ukiona mambo haya wananchi tunayajua na tunayasikia ni kwa kazi kubwa inayofanywa na taasisi hizi na ndio maana tukawa tunayajua. Kutokuwepo kwa taasisi hizi bado Zanzibar tungekuwa tunakula vyakula ambavyo havina viwango na havina usalama. Uwepo wa taasisi hizi ndio tunayagundua mambo mengi ambayo tunayafanyia kazi na tunayashughulika. Tutaendelea kupambana na mfanyabiashara yeyote atakayeingiza chakula au bidhaa zozote katika nchi yetu kwa matumizi ya binaadam ambazo hazina viwango au hazina salama. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 18

Uharibifu wa Mazao na Kimapunju wa Uroa

Mhe. Hidaya Ali Khamis (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wa Uroa hasa wakulima ambao wamepata hasara kubwa ya kuvamiwa mazao yao na kimapunju na kupelekea mavuno kidogo. Kwa kuwa kimapunju ni viumbe wanaohifadhiwa kwa shughuli za kuvutia watalii.

Je, kwa nini wakulima walioharibiwa mazao yao na kimapunju hawalipwi fedha kama wale wenzao wa Jozani na Pete.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:

Kwanza kabla ya kujibu naomba kusema yafuatayo: Leo Mhe. Naibu Spika, tuko kati kati ya Mwezi mtukufu wa Ramadhan tarehe 15 kama ni mlima basi tuko juu tumeshafika kileleni sasa tunashuka. Naomba sana Waheshimiwa pamoja na wananchi sote tushuke salama ili tuweze kuimaliza Ramadhan yetu tukufu hii kwa kuacha mabaya yote na kufuata mema yote ili tubarikiwe.

La pili, napenda kuzungumza kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakumbuka hichi ni kipindi chake cha pili kuingia katika Uwakilishi wa Jimbo la Paje, nadhani kama ataendelea zaidi na uwakilishi huu atakuwa mbioni kuwa Mwakilishi mkongwe, sio kama Mugabe lakini kwa kule Zimbabwe ataitwa jongwe kama ataweza kuendelea.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa jibu swali lililokuleta hapo umekuja kujibu maswali. Mimi nilikuruhusu umezungumza ya Ramadhan sawa, lakini sasa hivi tena la Mhe. Jaku naona si wakati sahihi wa kulizungumza, isipokuwa ujibu swali lake. Na ni kutokana na kanuni zetu unatakiwa ukija hapa unajibu swali moja kwa moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Jozani na Ghuba ya Chwaka wanaendelea kufaidika na mapato yanayotokana na watalii kutokana na faida zinazotokana na uhifadhi wa kimapunju. Hii imetokana na ukweli kwamba wananchi hao kwa kushirikiana na serikali wameweza kuanzisha mfumo mahsusi wa kuhifadhi maliasili na kuweka vivutio mbali mbali kwa ajili ya utalii.

Kuhusu wananchi ambao wanazunguka Hifadhi ya Kiwengwa-Pongwe wakiwemo wananchi wa Uroa, wapo katika hatua za awali za kuanzisha na kuendeleza utalii wa kimazingira ili baadae waweze kuweka vivutio vya utalii kama vilivyopo katika Hifadhi ya Jozani. Hivyo basi, Wizara

ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Halmashauri husika kupitia mfumo wa ugatuzi itaendelea kuwashajihisha wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Kiwengwa-Pongwe wakiwemo wananchi wa Uroa kuhifadhi na kuanzisha miradi ya kitalii itakayopelekea kuongeza mapato na hatimae kuweza kufaidika kama ilivyo kwa wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia majibu haya yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wengi ambao wako katika maeneo haya ya Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini wana changamoto kubwa kuhusu kimapunju na ndio swali mama lilivyouliza huku.

Je, serikali ina utaratibu gani wa kuweka haya maeneo ya hifadhi kwa hawa wanyama kimapunju kwa sababu tunajua kwamba kimapunju ni hifadhi na ni wanyama ambao ni kivutio kwa utalii. Lakini pia kuna changamoto kubwa kwa wakulima wetu kwa kuharibiwa mazao yao na bila ya kupata fidia yoyote kutoka serikalini au ndani ya wizara.

Je, Mhe. Waziri kuna taratibu gani ambazo mtaziweka ukiachilia mbali hizo za kuweka vivutio vya utalii kwa hawa wakulima wadogo wadogo ambao wanaathirika sana kwa mazao yao kuliwa na kimapunju.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ukweli tunakubali kwamba kimapunju kwenye mashamba ya kilimo popote walipo ni changamoto kwa maana wanaharibu mazao. Lakini kwa sababu tumeamua kuhifadhi msitu wetu ule pamoja na wanyama hawa ambao ni kivutio basi itatubidi tutumie maeneo yale kwa kazi hiyo. Sasa utaratibu ambao tunakusudia kuufanya ni kuhamasisha wananchi walime maeneo ya jirani ya maeneo yale ili wasipate athari za hao kimapunju.

Lakini pia nimeeleza hapa mwanzo kwamba wananchi ambao watakuwa wanaathirika na kimapunju wenye mazao yao pale, wakiweza kuweka miradi ambayo itakuwa ya kivutio wataweza kupata mapato ambayo yatafidia mapato yale waliyokuwa wanayapata kutokana na kilimo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yana ufafanuzi mwema kwa ajili ya wananchi wa sehemu tatu, Kiwengwa, Pongwe na Uroa. Maswali yangu yenye (a) na (b) kama yafuatavyo.

(a) Wananchi wa maeneo haya katika hifadhi yao waanzishe miradi ya utalii ili wapate mapato wagawane baadae. Je, ni miradi ya aina gani ya utalii ambayo inahitajika katika hifadhi hiyo.

a) Hao kimapunju wapo kijiji gani kati ya kijiji cha Kiwengwa, Pongwe na Uroa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, aina ya miradi ambayo wanaweza kufanya ni ile miradi itakayokuwa kivutio kwa watalii, kwa mfano vitu vya kufuma kwa mikono na vivutio vyengine ambavyo vitawavutia watalii, hata kanga na vitenge na mambo mengine yoyote ambayo yatakuwa yanatengenezwa hapa Zanzibar basi yatakuwa ni vivutio. *(Makofi)*

Halafu kwamba kimapunju wapo kijiji gani na kijiji gani. Tumesema kwamba kimapunju wapo katika maeneo yote yanayozunguka msitu ule wa hifadhi wa Jozani, vijiji vote vile vinavyozunguka msitu wa Jozani wapo kimapunju, na wakati mwengine wanaweza hata wakatoka wakaingia katika maeneo mengine.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuendelea kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kujibu maswali yake vizuri kabisa, naomba niweke vizuri tu katika *Hansard* juu ya swali lililoulizwa na Mhe. Ali Suleiman Ali katika kujua miradi ya utalii ambayo inafanyika mle ndani ya hifadhi ya utalii katika misitu.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba wizara ina dhamira ya dhati kabisa kuendeleza vivutio ndani ya misitu ya hifadhi, vivutio hivyo ambavyo vitakuwa ni miradi mikubwa itakayoiongezea mapato serikali itajumuisha miti mikongwe ambao wapo watu wanakwenda kufanya tafiti za aina mbali mbali juu ya uhai wa miti ya aina hiyo. Pia na miti ambayo haipatikani sehemu nyengine lakini hapa petu inapatikana ambayo imo ndani ya hifadhi tulizoziweka.

Lakini vile vile ndani ya misitu kumekuwa na faraja na tumepata baraka za aina yake kwa baadhi ya wanyama, mbali ya kwamba tuna aina ya kimapunju ambao wanapatikana pekee Zanzibar na kivutio kikubwa kwa utalii bado tuna aina nyingi ya vipepeo ambavyo vinapatikana hapa Zanzibar na sehemu nyengine havipatikani.

Lakini kuna wanyama ambao wameletwa miaka mingi iliyopita kwa mfano paa nunga, ni wanyama ambao wana vivutio vya aina yake kwa utalii. Kwa hivyo, sehemu hizo za hifadhi nazo zinaendelezwa ili kuhakikisha kwamba watalii wanakwenda katika maeneo hayo kuangalia misitu, wanyama, ndege na vivutio vyengine ambapo vipo hivyo.

Lakini vile vile ni maeneo gani ambayo katika misitu hii mitatu iliyozungumzwa kwenye ukanda wa Chwaka mpaka kufikia ukanda wa Kiwengwa, wanyama hawa kimapunju zaidi wanapatikana wapi. Ni ukweli kama lilivyoulizwa swali na Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba wakulima wa Uroa, Marumbi na Chwaka wana tatizo kubwa sana la kimapunju, kimapunju hawa ni hao hao wanaosafiri yaani wana-*immigrate* kutoka eneo moja kwenda eneo jengine. Kimapunju hao wanaweza kutoka Jozani, wakapita Ufufuma, wakaingia Marumbi, wakatoka wakapitia msitu wa Uroa na kumalizia msitu wa hifadhi Kiwengwa.

Kwa hivyo kimapunju hawa zaidi wanapatikana maeneo ya Marumbi, na Marumbi tayari wamelalamika juu ya suala hili na sisi Wizara ya Kilimo tumeanza kuchukua jitihada ili kuhakikisha kwamba tunawalinda, tunawatetea na tunayaenzi haya maeneo ya vivutio kwa wananchi wa Marumbi nao kupata faida kama wanavyopata wananchi wa Jozani na sehemu nyengine za hifadhi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 69

Wizi wa Mifugo Uliokithiri

Mhe. Hidaya Ali Makame (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Wananchi wa Maungani na Kisakasaka kwa kipindi kirefu wamechoka kufanyiwa vitendo vya wizi wa mifugo.

(a) Hatua gani zinachukuliwa kukabiliana na wimbi la wizi wa mifugo.
(b) Mifugo mingapi imekamatwa pamoja na wahusika wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba wizi wa mifugo ni tatizo katika maeneo ya Maungani, Kisakasaka na maeneo mengi ya Unguja na Pemba. Aidha, ifahamike kwamba matendo ya wizi ni kosa la jinai ambalo husimamiwa na vyombo vya ulinzi na sheria, hivyo inakuwa sio suala ambalo linasimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Kilimo. Aidha, Wizara hushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika ushauri katika kupunguza vitendo hivyo vya kihalifu.

(b) Mhe. Naibu Spika, wizara haina takwimu za idadi ya wizi wa mifugo inayoibiwa kwani watuhumiwa wote hupelekwa polisi na kumaliziwa katika vyombo vya sheria.

Hivyo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ikitaka data kama hizo basi lazima iende sehemu za polisi. Kwa hivyo, namshauri pia Mheshimiwa aende polisi akadai hizi takwimu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri jibu lako hilo la mwisho sio sahihi hata kidogo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu, lakini kama tunavyofahamu wizara hii ni wizara ambayo tunaitegemea sana wakulima na wakwezi. Wizara hii ndio wizara jembe yenye wasomi wengi wenye *PhD, Masters* na wengineo. Kwa hivyo, tungetegemea hapa ndani ya Baraza leo tukapata takwimu sahihi ya hawa wezi wa mifugo ambao wanaikabili jamii yetu.

a) Sasa mimi nimuulize tu Mhe. Naibu Waziri, ni lini atatuletea takwimu sahihi ya wezi hawa wa mifugo wanaohusika na maeneo ya Kisakasaka na kwengineko.

b) Kama wizara inachukua utaratibu gani wa kufuatilia kila pale panapohusika kuhakikisha kwamba suala hili la wizi wa mifugo linakoma na linakuwa mwisho ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza, kuhusu takwimu tutazifuatilia huko zinakokusanywa kwenye vyombo vya sheria tutaziwasilisha kwenye Baraza hili kwa kipindi hichi hichi tunachoendelea na bajeti, tutawasilisha kabla ya kumaliza bajeti.

Swali lake la pili anasema wizara inachukua hadhari kubwa sana kuhusu tatizo hilo la wezi wa mifugo kwa sababu kwa kweli wizara inakereketwa sana na vitendo hivi vya wizi wa mifugo. Nimesema hatua tunazochukua kwa sababu ya ugatuzi ni kwamba tunashirikiana na wizara husika kutumia vikosi vyetu hivi vya SMZ, kazi maalum katika kulinda maeneo yote ambayo yana mifugo hususan yale maeneo ambayo yana wizi wa mifugo uliokithiri na tutatilia mkazo sana katika kulinda mifugo hiyo isiendelee kuibiwa.

Mhe. Naibu Spika: Swali la mwisho la nyongeza Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili la wizi wa mazao na mifugo limekuwa ni tatizo kubwa kwa sehemu nyingi za Unguja na Pemba kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri, ikiwemo jimbo langu la Konde na maeneo mengine. Na kwa sababu mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika wanaoibiwa hapa huchinjwa humu na hawasafirishwi kupelekwa nchi nyengine. Je, mimi nilitaka nijue tu, ni utaratibu gani unaochukuliwa kuwadhibiti hawa wachinjaji wa ng’ombe na wauzaji wa kwenye mabucha, ili kuhakikisha kwamba nyama inayouzwa katika yale mabucha imechinjwa kihalali na muuzaji amepata vibali vyote kutoka Wizara ya Kilimo na wizara nyengine husika.

Swali (b) je, serikali inalifahamu tatizo la wizi wa kuku uliosambaa mitaani mwetu. Kama inalifahamu ni hatua gani wanazozichukua kudhibiti huo wizi wa kuku wa kienyeji katika mitaa yetu ili wakulima wetu, wafugaji wetu wasinyong'onyezwe na tatizo hili la wizi wa mifugo kama hili. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa swali la (b) tayari ameshalijibu nafikiri ndio swali la msingi kabisa kuhusiana na hili tayari limeshajibiwa. Lakini swali (a) Mheshimiwa ataweza kuendelea kulijibu. *(Makofi)*

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili , Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la (a) kama ifuatavyo:

Utaratibu wa kudhibiti wachinjaji, utaratibu tulionao katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kudhibiti wachinjaji ni kuweka machinjio mahala maalum ambamo mnakubalika. Wale wote ambao wanachinja nje ya maeneo hayo huwa wanafanya kosa kubwa sana, na pindi tukiwagundua huwa tunawachukulia hatua kali kwa sababu kwanza kiafya inakuwa hairuhusiki. Kwa hivyo, sisi tutaendelea na kuhakikisha kwamba tunakuwa na machinjio ya kutosha na kuhakikisha ng'ombe wote wanachinjwa na kusafirishwa kupelekwa mahala mnamouzwa wakiwa katika hali ya usafi ili pasije pakatokezea matatizo ya magonjwa kwa binaadam.

Kwa hivyo, kwa ufupi tunasema tu kwamba tunadhibiti suala hili kwa kuweka machinjio mahala maalum pamoja na kuweka watibabu wetu, wataalam wetu wakaguzi wa nyama katika kila maeneo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, niendelee kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuweka fasaha kabisa katika kuwatosheleza Waheshimiwa Wawakilishi kwenye maswali yao, hususan kwenye maswali ya nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuweka sawa tu bado *hansard* kuhusu takwimu ambazo zimeulizwa. Kama tunavyojua wizara yetu ina vitengo vya kufanya utafiti ni wazoefu kabisa kwa masuala ya takwimu. Na kama Mhe. Hidaya Ali Makame alivyoona kwamba wizara hii ina umuhimu wa kuwalinda hususan wakulima, wafugaji, wavuvi na athari hizi wanazozipata za wizi nataka nimfahamishe tu kwamba, takwimu inaweza ikachukua muda mrefu. Kwa sababu takwimu inahitaji ufuatiliaji na ni wazi wizara yangu haitapendelea kuleta takwimu ambazo si sahihi, suala la kuwakamata wezi wa mifugo, wezi wa kuku kama ilivyoulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid ni suala ambalo linahitaji mashirikiano, ni suala mtambuka na wizara nyengine. Kwa hivyo, sisi Wizara ya Kilimo tutaendelea na jitihada za kufuatilia takwimu hizo, tutaziweka takwimu hizo na pale zitakapokuwa na mfumo maalum ndio tutakapoziwasilisha ndani ya Baraza lako Tukufu.

Lakini nilikuwa naomba niweke *hansard* sawa tu sio kwamba katika kipindi hiki tunaweza tukazileta zile takwimu vipande vipande, takwimu tutazileta kwa urefu wake baada ya kufanya utafiti wa kina na kujua hasa kipi kinafanyika. Lakini ni kuongeza tu kwamba kweli hata wizara yetu inaumia sana kuona kwamba wakulima wanafanya jitihada za wazi kuhakikisha wanatafuta kipato chao na kuongeza pato la serikali, lakini bado tu kuna watu ambao wanawarejesha nyuma. Hata ndani ya Baraza tunawaita hivi hivi tu wezi au majizi, kwa hivyo hata wale wezi wa ng'ombe, wezi wa kuku wote ni wezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa katika suala zima la kuwadhibiti wezi nataka tuelewe wazi kwamba wezi na wao moja ya kazi yao ni ile kuiba, wale wezi moja ya kazi yao wanayojipanga nao ni kuiba. Kwa hiyo, ni suala linalotaka jitihada maalum, sisi kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri tutaongeza jitihada za kuweka vituo vya machinjio, lakini vile vile tutaendeleza mashirikiano na Wizara ya Tawala na vikosi vyetu vya Idara Maalum, ili kuhakikisha kwamba tunatumia watu wetu wenye uzoefu wa kushika hawa wezi tuwakamate. Lakini mwisho kabisa ni kusema kwamba tutaendelea kusimamia sheria. Sheria zote zetu zipo kwa hivyo wezi wanapokamatwa sheria zinapotumika zikifanya kazi vizuri wizi utaondoka *automatically.*

Mhe. Naibu Spika, zamani ulikuwa unaweza ukaisahau baiskeli nje ya nyumba yako ukaiacha usiku mzima lakini sasa ukiweka kwa masaa manne tu, wezi umewapa kazi. Kwa hivyo, ninachokitaka kukisema hapa ni kuzisimamia sheria tushirikiane na Jeshi la Polisi na wenzetu waweze kuzifuata hizi sheria katika kuzitendea haki. Tunaporudi nyuma katika kuzitendea haki sheria sisi wizara yetu ndio inapokosa kuwatendea haki wakulima, wavuvi na wengineo ambao wanaibiwa mazao yao. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba kuweka sawa.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea napenda kuwakaribisha wageni wetu waliofika hapa leo ambao ni wageni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi wanaotoka katika *Institute of Containing and Professional Studies (ICPS)* jumla yao ni kumi na sita na wanaongozwa na mwalimu wao Ndg. Khamis Ali Khatib. Ahsanteni sana vijana wetu na karibuni sana, karibuni. *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika: Katibu.

H**OJA ZA SERIKALI**

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kuniona na niendelee kwamba sina malengo ya kupoteza muda, lakini nasimama hapa kwa kutumia kanuni ya 42(1) hali kadhalika …

Mhe. Naibu Spika: Kanuni ya ngapi?

Mhe. Simai Mohammed Said: 42(1). Lakini pia natumia kifungu cha katiba 23(1) ambacho kinasema kwamba kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii katiba hii na sheria za Zanzibar, kuchukua hatua za kisheria kama zilivyowekwa kuhakikisha hifadhi ya katiba na sheria za nchi.

Mhe. Naibu Spika, wiki iliyopita nilizungumza baada ya kipindi cha maswali na majibu na ulinipa nafasi nikazungumza pia kwa moyo wangu na kutaka pia kwamba suala la vijana au watoto ambao waliokuwa chini ya umri wanatumia vyombo vya moto hususan maringi mawili ambao umaarufu wake pasola. Nikaomba serikali bila ya kupata majibu siku hiyo hiyo walichukue walifanyie kazi. Nikakumbushia tena mara ya pili na Mhe. Waziri akatoa agizo. Lakini Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu ni kwamba kukumbusha ni wajibu wetu na tupo

katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan tunatakiwa sote tuwe tunatumia busara sana na wajibu wetu tusiwe na jazba na tuwe tunakwenda vizuri, hasa katika kuwatumikia wananchi wetu. Lakini kwa masikitiko yangu Mhe. Naibu Spika, baada ya agizo la Mhe. Waziri hadi leo ukipita huko mitaani na nje matendo haya yanaendelea wewe mwenyewe ni shahidi pia karibuni kama siku nne, tano tulikuwa nje pia tulikuwa tukijadili jambo hili pia. Lakini wengi Wajumbe wa Baraza hili pia wamekuwa wamekuwa wakitilia msisitizo juu ya suala hili la vijana au watoto walio chini ya umri kutumia vyombo vya moto maringi mawili.

Sasa mimi malengo yangu niseme tu kwamba leo itakuwa mara ya tatu nakumbushia nafanya hivi kwa nia nzuri. Sasa mimi niseme kwamba tuna Serikali ya Mkoa wa Mjini na tuna Serikali zetu za Wilaya, lakini pia tuna Serikali Kuu na tuna vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Jambo hili kwa sasa tunaelekea katika kumi na kumi na tano la mwisho la Ramadhan yetu, lakini pia tunaelekea katika sherehe za Iddi. Mimi niombe kwamba hasara hii tunaipata kwa vijana wetu, lakini pia kiafya ambapo matibabu sasa yanakwenda upande wa Mnazi Mmoja.

Lakini pia katika mazingira ya huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan sasa hivi hasa katika suala la *road rage* vijana hawa wamekuwa sasa wanapita na hivi vyombo vya moto maringi mawili umaarufu kama pasola au vespa wanakupita mbele yako bila ya kuogopa.

Sasa mimi kwa kweli sasa hivi napata khofu kwamba sijui tufanye kitu gani. Lakini mimi nimesimama hapa Mhe. Naibu Spika, nataka muongozo wako, lakini pia nikitambua kwamba sina uhakika Waziri wa Nchi hayupo, Waziri mwenye dhamana na Naibu Waziri siwaoni hapa, pia naamini Mwanasheria Mkuu yupo na Serikali na Mawaziri wengine wapo. Kwa hiyo, labda tutaweza kupata majibu ili na sisi pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na ma-*back benchers* ambao ni watetezi au wasemaji wa wananchi ili tuweze kujua hasa kutoka hapa leo. Niseme leo hasa kweli binaadam anasema kukumbusha usichoke lakini kwa kweli na mimi pia uso wangu umeumbwa na haya kwa hiyo leo nitakuwa nasema kwa mara ya mwisho. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said na kama ulivyosema kwamba hoja hii umewahi kuileta na nafikiria leo ni mara ya tatu tena kuizungumza kama unavyosema mwenyewe. Waheshimiwa Wajumbe suala hili nafikiri labda tuwaambie serikali wajibu, lakini suala hili sote tunalifahamu kwamba lipo na linaendelea na nafikiri hoja yake kwamba serikali izidi kuhakikisha kwamba inaweka utaratibu maalum wa kunusuru maisha ya hawa vijana, lakini hata watu wazima vile vile. Kwa sababu ajali inapotokea si yule tu anayesababisha ajali bali na wengine ambao wapo katika maeneo yale wanaweza kupata athari hizo. Kwa hiyo, nafikiri nikupongeze sana Mheshimiwa kwa hoja yako na mimi naamini serikali yetu ni sikivu kabisa inasikia. Lakini kama ulivyosema kukumbushana kupo, tunakumbushana zaidi imekuwa ni mazowea kila ikifika kipindi cha Ramadhan hususan katika wiki mbili hizi za mwisho tunakuwa na misiba mingi inayosababishwa na ajali za barabarani. Kwa kweli hili ni jambo ambalo linasikitisha sana lakini tunaiomba serikali na nafikiri serikali yetu inasikia hapa kwamba mzidi kuchukua hatua zaidi hasa kuhusiana na hawa wanaoshughulika na masuala ya barabarani. *(Makofi)*

Mimi labda kuna mserikali yeyote ambaye anaweza labda kulizungumzia hilo, lakini niombe tu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa kwamba serikali imesikia na ichukue hatua, ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru Mhe. Simai Mohammed Said kwa kuendelea kukumbusha hoja hii. Kama alivyosema mara ya kwanza na akasoma Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 ambayo kwanza imeweka utaratibu wa namna ya utoaji wa leseni na mtu yeyote ambaye yupo chini ya miaka 18 haruhusiwi kuendesha chombo chochote kikubwa bila ya kuwa na leseni. Hilo la kwanza.

Lakini la pili Mhe. Naibu Spika, hili jambo sio la serikali tu peke yake kwa sababu hawa vijana wananunuliwa vyombo majumbani, sisi wazee ndio tunaowanunulia vyombo hawa vijana. Kwa hiyo, natambua Mhe. Simai Mohammed Said na yeye pia ni mzee, kwa hiyo na yeye kwanza ana jukumu namba moja la kuhakikisha kwamba hamnunulii mwanawe chombo ambacho kipo chini ya umri.

La pili, tutaendelea sisi kama serikali kukumbushana na wenzetu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanaendesha vyombo iwe pasola, iwe magari na hawana leseni ya kuendesha vyombo hivyo, basi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watu hawa. Kwa hivyo, mimi niombe jamii yetu yote kwamba hili jambo ni letu sote, sio mzigo tu wa serikali wa kusema serikali lishughulikieni, ni letu sote kwa sababu sisi ndio wazee na hawa watoto wanapotoka majumbani wanatoka na sisi tukiwaona na tukiwatuma na tukiwaachia watumie hivyo vyombo. Kwa hivyo, sisi tunalichukua lakini tunalichukua kwa mintaarafu ya kuzungumza na wenzetu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba wanaendelea na doria zao za kila siku wanazofanya, ili kuhakikisha wale wote ambao wanaendesha vyombo kinyume na taratibu za sheria basi hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, umetoa muongozo mzuri, lakini pia nimshukuru Mhe. Simai Mohammed Said kwa kukumbushia, nadhani kwa majawabu haya hatosimama tena kukumbushia tena, atakuwa karidhika na majawabu ambayo yametoka. Nashukuru Mheshimiwa. *(Makofi)*

HOJA YA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka Fedha 2018/2019 - Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Waziri kabla ya kuendelea kwa sababu umeniletea ki-*note* hichi kunitambulisha wageni wako ambao wamefika hapa leo, basi nichukue fursa hii kuwatambulisha wageni hao ambao ni wageni kutoka taasisi ya *TAHA* naomba kama wako hapo wasimame, *MILELE Foundation* karibuni sana, *FAO* karibuni sana na Kampuni ya ZAIDI wapo wamekuja kushiriki katika uwasilishaji wa Bajeti yetu. Karibuni sana wageni wetu. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nitoe shukrani zangu za dhati kabisa ndani ya moyo kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kwa uwezo wake wa kutuwezesha na kutusaidia kuweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu. Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Na si kwa upendeleo lakini nitoe shukrani zangu za dhati ndani ya mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan ikiwa leo tuko katika kumi la pili kati kati ya mwezi, kumi la maghfira, basi nitoe pongezi zangu na shukrani za dhati kwa familia yangu hususan kupika futari mke wangu ambaye amenipa moyo mkubwa sana usiku wa jana kuamkia leo kuweza kuja kuwasilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Aidha, siusahau uongozi wa jimbo, uongozi wa wilaya na uongozi wa tawi katika jimbo langu pamoja na waajiri wangu wote ambao wameniwezesha kufika hapa kuweza kutekeleza majukumu ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa na kwa idhini ya Baraza lako Tukufu hili naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu na kuliomba likae kama Kamati kwa ajili ya kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa huu Programu hii (PBB).

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima na wenye afya ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendelelo ya wananchi wetu wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, ambapo asilimia 70 na wahusika wengi wanajishughulisha na kazi za kilimo, ufugaji, uvuvi na uhifadhi wa maliasili zetu.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kuiongoza nchi yetu katika misingi ya umoja, usalama, amani na utulivu. Aidha, tunampongeza kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020 inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kufanikisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwa wananchi na kukuza uchumi.

Vile vile tunamshukuru sana kwa kutuonesha imani ya kututeua tena kushika uongozi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, hivyo nasi tunamuahidi kwamba tutafanya kazi kwa jitihada, uzoefu, maarifa ili kuleta maendeleo katika sekta hii ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake kubwa za kumsaidia na kumshauri vizuri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi yetu na kuleta manufaa kwa wananchi hasa kwenye sekta hii ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kukupongeza wewe binafsi, Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaokusaidia kuliongoza Baraza lako na

tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu akuzidishieni uwezo, hekima na busara, ili sote kwa pamoja na Wajumbe tupate wepesi wa kuliendesha kwa mafanikio na ufanisi Baraza lako hili tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa miongozo na ushauri mnaoutoa kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi kwa kufanikisha utekelezaji wa malengo katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 ambayo imefanikiwa kwa asilimia kubwa. Aidha, tunaishukuru Kamati kwa kufanikisha maandalizi ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019. Napenda kuihakikishia Kamati yako kwamba maoni, ushauri, mapendekezo na maarifa waliyotupatia tumeyazingatia, tumeyachukua na katika bajeti hii ninayoiwasilisha yatatekelezwa kwa miongozo yao.

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Kilimo ikijumuisha mazao, mifugo, uvuvi na misitu bado inaendelea kuwa ni mhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar na inatoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha ambapo asilimia 40 wameajiriwa na sekta hii; na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii ambayo imeongoza kwa ukuaji katika Pato la Taifa na kufikia wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2017 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2016. Nampongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango kwa usimamizi wake wa takwimu hizi ambazo naziwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2017 sekta ya kilimo imekuwa ya pili kwa kuchangia pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 27.9 ikilinganishwa na asilimia 25.5 mwaka 2016. Aidha, kuimarika kwa sekta ya utalii katika nchi yetu kumetokana na mchango mkubwa wa sekta ya kilimo kwenye maeneo ya baharini, hifadhi za taifa na vyakula tofauti vinavyotokana na sekta hii ya kilimo ambayo imepelekea kuongezeka kwa ajira katika maeneo hayo; na upatikanaji wa chakula cha ziada kwa ajili ya biashara, kuwa na uhakika wa chakula na hatimae kupunguza umaskini.

HALI YA UZALISHAJI

Mhe. Naibu Spika, uzalishaji wa matunda na mazao ya chakula kwa jumla umefikia tani 357,932 mwaka 2017 na kuongezeka kwa asilimia 32.1 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani za mwaka jana 2016 ambazo ni 111,883. Uzalishaji mkubwa kabisa ni wa zao la muhogo tani 142,714 sawa na asilimia 40 ya uzalishaji wa mazao yote; hii inafuatiwa na uzalishaji wa ndizi tani 73,243 ambazo sawa na asilimia 20.5 ya uzalishaji wote. (Angalia kiambatisho Nam. 1).

Mhe. Naibu Spika, takwimu za kilimo zinaonesha kuongezeka kwa mavuno kwa baadhi ya mazao ya chakula na biashara mwaka 2017 ikilinganishwa na mwaka 2016. Zao la mpunga limeongezeka hadi kufikia tani 39,683 mwaka 2017 ikilinganishwa na wastani wa uzalishaji tani 20,603.5 kwa miaka mitano 2012 hadi 2016 ikiwa ni ongezeko la tani 19,079.15. Karafuu zimeongezeka kutoka tani 4,678.69 mwaka 2016 hadi kufikia tani 8,277.2 mwaka 2017, Viazi vitamu kutoka tani 24,834.3 mwaka 2016 hadi 34,203.09 mwaka 2017, mahindi yameongezeka kutoka tani 891.73 mwaka 2016 hadi tani 1,585.59 mwaka 2017. Mazao ya mboga (tungule,

nyanya, bilingani, bamia, mchicha, tango, pilipili na matikiti) kutoka tani 26,512 mwaka 2016 hadi kufikia tani 32,679 mwaka 2017.

Mhe. Naibu Spika, ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula hasa mpunga limetokana na mpango ulioanzishwa na Wizara wa kuanzisha mashamba ya mfano yenye ukubwa wa ekari 50 katika kila Wilaya. Wakulima katika mashamba hayo pamoja na wakulima wote katika mabonde ya umwagiliaji hekta 810 wamepatiwa mahitaji kamili ya pembejeo (mbolea, dawa na mbegu) matokeo yake ni kuongezeka uzalishaji kutoka tani 0.9 hadi tani 1.33 kwa ekari kwa mpunga wa kutegemea mvua na wastani wa 2.5 hadi 4.5 kwa mpunga wa umwagiliaji. Aidha, kuwepo kwa hali ya hewa nzuri, juhudi za sekta binafsi ikiwemo TAHA, ZAIDI, *Milele Foundation*, maduka ya pembejeo na Mkakati wa Serikali wa kutoa miche ya mikarafuu bila ya malipo kila mwaka zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya mboga, chakula na karafuu.

Mhe. Naibu Spika, takwimu zimeonesha pia kushuka kwa uzalishaji kwa baadhi ya mazao ya chakula yakiwemo viazi vikuu kutoka tani 3,519.92 mwaka 2016 hadi tani 2,678.05 mwaka 2017, mbaazi kutoka tani 1,414.42 mwaka 2016 hadi tani 1,271.97 mwaka 2017 na chooko kutoka tani 125.04 mwaka 2016 hadi tani 114.19 mwaka 2017.

Mhe. Naibu Spika, takwimu za kilimo zinaonesha kwamba eneo lililolimwa limeongezeka, jumla ya ekari 91,270 zimelimwa aina tofauti za mazao ikilinganishwa na ekari 70,270 zilizolimwa mwaka 2016. Nawapongeza sana wakulima na leo nipo mbele yao kuwasilisha bajeti yao kwa kile walichokifanya. Zao la mpunga pekee kwa mwaka 2017 limelimwa ukubwa wa ekari (29,017) ikiwa ni sawa na asilimia 31.8 ya eneo lililolimwa. Kati ya hizo ekari 26,891 zimelimwa mpunga wa kutegemea mvua na ekari 2,126.4 zilizobakia zimepandwa mpunga wa kumwagilia maji kwa kutumia teknolojia za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, eneo la pili linalofuatia lililimwa muhogo ekari 24,312.5 sawa na asilimia 26.6 ya eneo lote lililolimwa. Eneo lililolimwa mihogo limeongezeka na kufikia ekari 8,516.6 mwaka 2017, kutoka ekari 6,448.2 mwaka 2016 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 32. Wakati eneo lililolimwa viazi vitamu pia limeongezeka na kufikia ekari 4,886 mwaka 2017 kutoka ekari 3,547.8 mwaka 2016, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 37.7. Takwimu pia zinaonesha kwamba eneo lililopandwa mazao tofauti ya matunda na mboga ikiwemo mchicha, nyanya na mabilinganyi yameongezeka kutoka ekari 825 mwaka 2016 hadi ekari 1,220 mwaka 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 48.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa sababu zilizochangia ushukaji wa mazao hayo ni pamoja na kupungua kwa maeneo yaliyolimwa mazao ambapo viazi vikuu kutoka ekari 703.8 mwaka 2016 hadi kupungua ekari 535.6 mwaka 2017, mbaazi kutoka ekari 437.9 mwaka 2016 hadi kupungua ekari 393.8 mwaka 2017 na chooko kutoka ekari 312.61 mwaka 2016 hadi ekari 285.48 mwaka 2017. Aidha, hali halisi inaonesha kwamba baadhi ya wakulima hasa katika maeneo ya maweni wameanza kulima mazao ya mboga tofauti na mazao ya mizizi, nafaka na jamii ya kunde yaliyokuwa yakilimwa asili. Aidha, nawahakikishia wakulima kwa ujumla wao nikiwa hapa nawasilisha bajeti yao ya kwamba soko la uhakika la mazao yao lipo na Wizara inashauri

waendelee kulima mazao hayo ili kuongeza lishe, uhakika wa chakula na afya na Wizara iko pamoja nayo.

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha ongezeko la uzalishaji wa maziwa kutoka lita 40,895,412 kwa mwaka 2016 hadi lita 40,958,058 kwa mwaka 2017. Uzalishaji wa mayai umepungua kutoka mayai 186,163,932 mwaka 2016 hadi mayai 167,694,202 mwaka 2017 (Angalia kiambatisho Nam. 2 & 3). Aidha, takwimu zinaonesha kuwepo kwa ongezeko la idadi ya mbuzi waliochinjwa kutoka 1,625 mwaka 2016 hadi kufikia 2,739 mwaka 2017 sawa na asilimia 169 na kuku kutoka 707,792 mwaka 2016 hadi kufikia kuku 819,994 mwaka 2017 sawa na asilimia 116 ya ongezeko. Kwa ujumla maendeleo katika sekta ndogo ya mifugo imechangia upatikanaji wa ajira, kuongeza mapato kwa Serikali na watu binafsi na kuimarisha lishe kwa jamii.

Mhe. Naibu Spika, takwimu za mazao ya baharini zinaonesha kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kutoka tani 33,892.5 zenye thamani ya TZS136.15 bilioni kwa mwaka 2016 hadi kufikia tani 35,057.2 zenye thamani ya TZS164.10 bilioni mwaka 2017. Kwa upande wa zao la mwani uzalishaji umeshuka kutoka tani 16,665 kwa mwaka 2015, tani 11,113.30 mwaka 2016 hadi kufikia tani 10,981 mwaka 2017. (Angalia kiambatisho Nam 4). Kushuka kwa zao la mwani napenda kueleza sababu kabisa kwamba kumechangiwa na maradhi yatokanayo na mabadiliko ya tabia ya hali ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa uhifadhi wa misitu na maliasili zisizorejesheka, takwimu zinaonesha ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya kuni kutoka mita za ujazo 19,532.25 mwaka 2016 hadi kufikia mita za ujazo 23,114 mwaka 2017. (Angalia kiambatisho Nam. 5). Kwa mazao ya maliasili zisizorejesheka kumekuwepo na ongezeko la uchimbaji na matumizi ya mawe kutoka tani 81,377 mwaka 2016 hadi tani 91,728 mwaka 2017 na mchanga kutoka tani 576,476 mwaka 2016 hadi kufikia tani 832,043 mwaka 2017. (Angalia kiambatisho Nam. 6).

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako takwimu na sababu nyingi nilizozieleza hapo katika ukurasa wa 4 mpaka ukurasa wa 9 katika kitabu wanachokisoma Wajumbe kwa kina kabisa naomba ziingizwe katika *hansard* yako ya Baraza lako Tukufu kama zilivyo katika kitabu changu cha hotuba hii ninayoiwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, ongezeko la matumizi ya maliasili zisizorejesheka linatokana zaidi na mahitaji makubwa ya miradi ya maendeleo ikiwemo kasi kubwa ya ujenzi kwenye makaazi mapya ya wananchi, miundombinu ya uwanja wa ndege, bandari, viwanja vya michezo, pamoja na barabara za mijini na vijijini. Aidha, Wizara inaendelea kutoa taaluma ya Uhifadhi wa Maliasili zetu pamoja na kuhamasisha njia mbadala katika kuwawezesha wananchi katika kupunguza matumizi ya Maliasili Zisizorejesheka, nishati ya kuni kwa kutumia majiko sanifu na gesi salama. Wizara inaendelea na kuratibu utaratibu mzuri wa matumizi ya mchanga. Hivyo, tunatoa wito kwa wananchi na Halmashauri kushirikiana na Wizara katika kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali zetu.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA MWAKA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imesimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs)*, Mipango Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo *(ATI)*.

MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilikadiriwa kukusanya TZS 4.93 bilioni kutokana na vyanzo vyake 11 vya mapato. Kipindi cha miezi kumi Julai, 2017 hadi April, 2018 Wizara imekusanya TZS 8.15 bilioni sawa na asilimia 165 ya malengo yaliyowekwa kama inavyoonesha bajeti hii. (Angalia kiambatisho Nam. 7) kimeeleza kwa vizuri zaidi. Ongezeko hilo limetokana na utaratibu mpya wa uchimbaji wa mchanga unaotekelezwa na Serikali pamoja na mapato yatokanayo na ukodishwaji wa Mashamba ya Mikarafuu na ongezeko la idadi ya watalii wanaotembelea maeneo ya hifadhi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 70.61 bilioni (TZS23.7 ni fedha za matumizi ya kazi za kawaida na TZS 46.90 bilioni ni fedha za kazi za maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tano za Wizara. Kati ya TZS 23.70 bilioni, mishahara ni TZS 17.63 bilioni, matumizi mengineyo ni TZS 4.49 bilioni na TZS 1.58 bilioni ikiwa ni ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Wakala wa Tafiti za Mifugo na Wakala wa Matrekta. Kwa upande wa fedha za maendeleo TZS 46.90 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 44.15 bilioni ni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 2.75 bilioni kutoka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). (Angalia kiambatisho Nam. 8).

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi April, 2018 Wizara imepata TZS 26.30 bilioni ambapo (TZS 20.10 bilioni ni kwa kazi za kawaida na TZS 6.20 bilioni ni kwa kazi za maendeleo). Kati ya fedha hizo TZS 20.10 sawa na asilimia 85 ya makadirio, mshahara ni TZS 14.50 bilioni, matumizi mengineyo ni, TZS 4.18 bilioni na ruzuku TZS 1.42 bilioni. Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo Wizara ilipata TZS 6.20 bilioni sawa na asilimia 13.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo TZS 4.75 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 1.45 bilioni kutoka SMZ. (Angalia kiambatisho Nam. 9). Kushuka kwa kiwango cha fedha za maendeleo kumetokana na kuchelewa kwa kuanza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji wenye ukubwa wa hekta 1,524 pamoja na kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa Soko la Samaki la Malindi. Matangazo ya zabuni ya kutafuta Wakandarasi wa ujenzi huo tayari yameshatoka kupitia vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi.

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepata mafanikio yafuatayo:

a) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na vyanzo 11 vya Wizara ya Kilimo kufikia TZS 8.15 bilioni mwaka 2017 ikilinganishwa na TZS 4.93 bilioni mwaka 2016.

b) Ufunguzi wa masoko matatu ya bidhaa za Kilimo huko Konde, Tibirinzi kwa Pemba na Kinyasini kwa Unguja pamoja na ukarabati wa vyumba vya baridi katika Soko la Mombasa (Unguja) na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi na Usarifu wa Mazao Pujini (Pemba). Ujenzi huo umegharimu TZS 4.6 bilioni.

c) Kuimarika kwa kilimo cha mpunga kwa kutumia teknolojia ya SHADIDI (mbegu kidogo na maji kidogo) katika mpunga wa umwagiliaji maji na kuongeza uzalishaji kutoka tani 2.5 hadi 6.8 kwa hekta. Vile vile kuimarika kwa matumizi ya miundombinu ya umwagiliaji maji *(drip irrigation)* katika mazao ya matunda na mboga hekta 100 pamoja na matumizi ya *green house.*

d) Kukamilika kwa matengenezo ya ghala ya akiba ya chakula liliopo Malindi Unguja lenye uwezo wa kuhifadhi wastani wa tani 900 za mchele.

e) Kuimarika kwa utoaji wa huduma za matrekta na zana zake kwa ununuzi wa matrekta mapya 20 na 10 msaada kutoka Ubalozi wa Libya, vile vile Wizara imepokea zana tofauti kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Jumla ya ekari 7,088 zimelimwa katika mabonde ya mpunga katika msimu wa masika 2018 kutokana na jitihada hizi za matrekta.

f) Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mboga hadi kufikia tani 11,891.97 mwaka 2017 kutoka tani 10,347.29 mwaka 2016 na matikiti kutoka tani 16,163.87 hadi kufikia tani 20,787 mwaka 2017.

g) Jumla ya wafanyakazi 35 wamepatiwa mafunzo ya usarifu wa vanila, vile vile Wizara imewahamasisha wakulima wa maweni kuendeleza kilimo cha pilipili hoho kwa Wilaya ya Kusini Unguja. Aidha, wastani wa tani tatu (2 matunda makavu na 1 tangawizi), pilipili manga kilo 165, mdalasini kilo 2,270, pilipili kichaa kilo 24.5 na vanila kilo 50 zimesarifiwa nje ya nchi kupitia kampuni ya *Zenj Spice Company Limited*.

h) Mhe. Naibu Spika, faida nyengine iliyopatikana ni kushajihika kwa wakulima wa alizeti na kuongezeka kwa ukamuaji wa mafuta ya alizeti kufikia lita 2,578.6 ikiwa Pemba pekee tumezalisha tani 2,117 na Unguja tumezalisha tani 461.6 tu.

i) Wizara inachukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambapo tafiti zinaendelea kufanyika kupitia Taasisi yetu ya Utafiti wa Kilimo kwa mazao ya mizizi na mpunga. Aidha, Wizara imepata mradi mpya wa *Climate Smart Agriculture* wenye thamani ya TZS 171,600,000 Milioni unaofadhiliwa na *USAID* kwa ajili ya mashamba ya mfano kwa utoaji wa elimu na utoaji wa taarifa za mabadiliko ya tabia nchi.

j) Kuongezeka idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi zetu za misitu na bahari kutoka 47,000 kwa mwaka 2016 na kufikia watalii 53,870 mwaka 2017. Huo ni mchango mkubwa sana katika kuongeza idadi ya watalii.

k) Vile vile kuimarika kwa uhifadhi na utalii katika Kituo cha Utalii Masingini *(Zanzibar City Park)* kwa kuongeza miundombinu ikiwemo mkahawa, zizi la wanyama pori na huduma za watalii ndani ya hifadhi.

l) Jumla ya miche 1,597,382 (1,364,267 imezalishwa Unguja na 233,115 imezalishwa katika misitu huko Pemba). Aidha, mikarafuu na matunda mengine imeoteshwa katika vitalu vyetu vyote vya Serikali. Aidha, uhamasishaji katika vitalu vya watu binafsi umefanikiwa kwa kuwezesha kuotesha wastani wa miche 2,000,000. Miti hiyo imepandwa katika maeneo ya wazi, maskuli na maeneo yaliyochimbwa mchanga ambayo tunaendelea kuyahifadhi.

m) Wizara imeimarisha huduma za utafiti, kinga na tiba na uzalishaji wa mifugo kwa kuongeza vifaa katika Maabara ya Mifugo Maruhubi vyenye thamani ya USD 10,000 (TZS 22,440,000). Vifaa hivyo vimefadhiliwa na washirika wetu ambao tumewaalika washirika wa *FAO*. Vile vile, Wizara imepata msaada wa mtungi wa kuzalisha gesi ya *nitrogen* kutoka Shirika la Atomiki *(IAEA)* wenye thamani ya EUR 25,732 (TZS 65,000,000) kwa ajili ya kuufanyia matengenezo mtambo huo. Aidha, jumla ya ng'ombe 1,250 wamepandishiwa kwa sindano.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna mafanikio makubwa katika kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kuzalishia Vifaranga vya Samaki *(Korea Zanzibar Friendship Marine Hatchery Center)* ambayo ina uwezo wa kuzalisha vifaranga milioni 10 vya samaki, majongoo 70,000 na kaa 50,000 kwa mwaka; kituo hicho kimegharimu jumla ya fedha USD Milioni 943,935.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuanzishwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar *(ZAFICO)* kwa kutumia mashirika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo nachukua fursa hii kuyapongeza sana kwa jitihada zao za kukamilisha fedha za kuianzisha hii *ZAFICO* ikiwemo (*ZSTC*, Bandari, *ZSSF* na Shirika la Bima) kwa mtaji wa jumla TZS 7.0 Bilioni. Aidha, bodi imeteua eneo lilioko Malindi tayari limekabidhiwa kwa kampuni pamoja na utaratibu wa kununua meli mbili za uvuvi umeanza kutoka nchini Srilanka na Maldives visiwa vya Ujerumani.
Vile vile katika maendeleo mengine jumla ya vikundi 114 vya wafugaji wa samaki vikiwemo vya Waheshimiwa Wawakilishi na wakulima wa mwani wamepatiwa mafunzo bora ya ufugaji wa mazao ya baharini Unguja na Pemba.

Katika mafanikio haya Mheshimiwa pia kuna kupitia Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania, jumla ya vijana 26 walipata fursa ya kuingizwa katika meli za kigeni kwa lengo la kujifunza uvuvi wa bahari kuu. Vile vile wavuvi vijana 25 wamepelekwa Chuo cha Uvuvi Mbegani Bagamoyo kujifunza uvuvi wa kisasa.

Naomba sana Mheshimiwa Wawakilishi wako wawe tayari katika uvuvi wa Bahari Kuu ambapo tunatarajia kuwa na meli nyingi sana zitakazosajiliwa hapa na kuweza kuvua samaki waliopo ambao hivi sasa wanaibiwa ndani ya Bahari Kuu.

Mhe. Naibu Spika, mafanikio mawili ya mwisho ilikuwa ni Wizara iwepo katika hatua ya mwisho kukamilisha Mpango Mkuu wa Uvuvi Zanzibar, pamoja na sensa ya uvuvi kupitia mradi wa *SWIO fish*. Pia, kwa kushirikiana na *FAO* imekamilisha utafiti juu ya kujua maeneo yenye wingi wa samaki katika bahari ya Tanzania na taarifa za utafiti huo zimeanza kufanyiwa kazi na matokeo yake yatatangazwa hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe nilikuwa shahidi katika kutizama tafiti hizo na nilifuatana kwa kushirikiana na mwenzangu Wizara ya Mifugo na Uvuvi kule jijini Dar es Salaam, jumla ya TZS 10,935,850,159 zimepatikana baada ya kukaguliwa na kusafirishwa nje tani za mwani 5,089 na tani 990 za madagaa zenye thamani ya TZS 22,157,130 kupitia kampuni mbali mbali. Hii inaonesha namna gani Wizara ya Kilimo inaweza ikachangia pato la Taifa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mafanikio mengi yanayopata 19 ambayo nimeyaeleza naomba maelezo hayo ambayo yapo kwa kina zaidi na yanapatikana katika kitabu chetu kutoka ukurasa wa 11 hadi 16 yasomeke kama yalivyo katika *hansard* ya Baraza lako Tukufu.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI MWAKA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia programu zake kuu tano (5) na ndogo kumi na tatu (13) ulikuwa kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo inayojumuisha programu ndogo nne; Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji, Programu ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo, Programu ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo, Wakala wa Matrekta ya Serikali na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe (UCL) ambazo zinatekelezwa kwa pamoja na Idara za Umwagiliaji Maji, Kilimo, Uhakika wa Chakula na Lishe, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo kiliopo Kizimbani.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji hii inatekelezwa kupitia Idara ya Umwagiliaji Maji na ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini kwa kutoa taaluma za uzalishaji na kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, kushajihisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji maji.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

a) Upimaji kwa ajili ya uwekaji umeme *(3 phase)* katika mabonde ya Kibonde mzungu, Koani, Banda maji, Mchangani, Dobi, Machigini na Ole umefanyika;

b) Jumla ya mita 870 za mitaro ya umwagiliaji maji zimejengwa kwa kiwango cha saruji (Makombeni 200, Kibokwa 200, Mangwena 110, Uzini 130, Bumbwisudi 200 na Mtwango 30);
c) Jumla ya pampu nne zimetengenezwa Bumwisudi 2, Cheju 1 na Kibokwa 1;
d) Ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua *(rain wáter harvesting)* umefanyika katika bonde la Muyuni hekta 5, Kisima mchanga hekta tano (5) Unguja na mabonde ya Kiongweni na Msaani hekta 10 kwa Pemba ambapo kupitia wakulima 129 (Unguja 50 na Pemba79) wamenufaika.
e) Wakulima 1,800 katika skimu 10 za umwagiliaji maji wamepatiwa elimu ya teknolojia ya SHADIDI katika uzalishaji wa mpunga inayotumia mbegu na maji kidogo ambayo inaongeza uzalishaji wa zao hilo.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS 27.15 bilioni ambapo TZS 1.41 bilioni (TZS 1.06 bilioni mishahara na TZS 350.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu ilitarajia kupata TZS 25.74 bilioni ambapo (TZS 740.00 milioni kutoka SMZ na TZS 25.00 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo mkopo kutoka *EXIM BANK KOREA.* Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 1.32 bilioni sawa na asilimia 93.6 ambapo (TZS 881.64 milioni mishahara, TZS 255.35 milioni kwa matumizi mengineyo na TZS 180 milioni fedha za maendeleo kutoka SMZ).

Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Chuo cha Kilimo Kizimbani, lengo ni kuimarisha na kuendeleza Tafiti za Kilimo na Maliasili pamoja na kuimarisha uwezo wa Chuo cha Kilimo Kizimbani na kuongeza wataalamu katika fani ya Kilimo na Mifugo.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2017/2018, tunaomalizia programu imetekeleza shabaha zifuatazo:

a) Uzinduzi rasmi wa Baraza la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar umefanyika;
b) Tafiti 4 (1 mpunga, 1 migomba, 1 kunde na moja mboga kwa Unguja na tafiti 2 (1 muhogo na 1 *sunflower*) kwa Pemba zimeanzishwa;
c) Mafunzo ya ndani kwa watafiti 25 (wanaume 14 na wanawake 11) yametolewa;
d) Rasimu ya kwanza ya muundo wa utumishi *(scheme of service)* imekamilika na inasubiri kuidhinishwa na Baraza la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 Taasisi ya Utafiti iliombewa jumla ya TZS 2.16 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.96 bilioni mishahara na TZS 200.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 taasisi imepata TZS 1.76 bilioni (TZS 1.63 bilioni mishahara na TZS 134.10 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 81 ya makadirio kwa miezi hiyo niliyoitaja.

Programu Ndogo ya Mafunzo ya Kilimo (Chuo Cha Kilimo Kizimbani)

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani (programu) kina jukumu la kutoa mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 programu imetekeleza shabaha zifuatazo:

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

a) Mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi 201 (ngazi ya Stashahada 67 na ngazi ya Astashahada 134), kuchukua wanafunzi wapya 169 (ngazi ya Stashahada 67 na ngazi ya Astashahada 102) na waliohitimu masomo 59 (ngazi ya Stashahada 27 na ngazi ya Astashahada 32);
b) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeridhia kazi ya kupima, kuchora na kugawa maeneo kwa kazi za maendeleo katika eneo la RAZABA, kazi hiyo inafanywa na Shirika la Nyumba *(NHC);*
c) Wakulima 170 (100 Bumbwisudi, 20 Muyuni na 50 Makombeni) wamepatiwa mafunzo ya uzalishaji bora wa mpunga kupitia mradi wa *TANRICE* na wameweza kupata mavuno ya wastani wa tani sita (6) katika hekta moja. Pia wakulima 316 na mabwana/bibi shamba 8 katika skimu za Makombeni, Micheweni, Dobi na Tibirinzi - Pemba na Bumbwisudi, Muyuni na Cheju - Unguja wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 programu iliombewa TZS 782.70 milioni (Ruzuku) kwa kazi za kawaida (TZS 672.80 milioni Mishahara na TZS 109.90 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 chuo kimepata TZS 730.80 milioni (TZS 642.70 milioni mishahara na TZS 88.10 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 93 ya pato lote.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo inatekelezwa kupitia Idara ya Kilimo ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalamu kwa wakulima.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018, program kupitia Idara imetekeleza yafuatayo:

a) Tani 1,800 za mbolea (900 ya kupandia na 900 ya kukuzia), tani 170 za mbegu na lita 17,400 za dawa ya kuulia magugu zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima Unguja na Pemba kwa ajili ya kilimo cha mpunga. Aidha, tani 88,134 za mazao ya kilimo kutoka na kwenda Tanzania Bara na nje ya nchi zimekaguliwa kwa lengo la kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao kuingia nchini;
b) Tani 9.5 za vitunguu thomu zilirudishwa India kutokana na kuwa katika hali ya kutoweza kutumika. Tani 11 za ndizi kutoka Tanzania Bara zilikamatwa na kuangamizwa kutokana na kuwepo karantini ya usafirishaji wa migomba kutokana na maradhi ya “mnyauko” ambayo

yameathiri kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa ndizi Tanzania Bara na nchi nyengine za Afrika Mashariki.
c) Jumla ya masanduku 12,080 ya tungule yenye thamani ya TZS 1.20 bilioni zimesafirishwa na kupelekwa Tanzania Bara.
d) Mikutano 11 ya maandalizi na ufuatiliaji mipango ya maendeleo ya kilimo imefanyika kila Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS 5.00 bilioni (TZS 3.10 bilioni mishahara na TZS 1.90 bilioni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 4.35 bilioni (TZS 2.52 bilioni mishahara na TZS 1.83 bilioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 87 ya makadirio.

Programu ya Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekelezwa kupitia Wakala wa Serikali wa Matrekta na Zana za Kilimo ambapo ina jukumu la kutoa huduma za matrekta kwa wakulima, sekta binafsi, taasisi na kuhamasisha matumizi bora ya matrekta na zana za kilimo.

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

a) Jumla ya matrekta 23, majembe 17 ya kulimia na majembe 10 ya kuburugia yametengenezwa na kupelekwa mabondeni kwa ajili ya kuwahudumia wakulima wa mpunga;
b) Jumla ya matrekta mapya 20 yamenunuliwa na matreka 10 ya msaada yamepokelewa kutoka Libya;
c) Matengenezo ya ofisi, karakana pamoja na mashine yamefanyika;

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS 300.00 Millioni ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia April, 2018 imepata TZS 257.50 sawa na asilimia 86.

Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula Na Lishe

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekeleza kupitia Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe ambapo ina jukumu la kuhakikisha uwepo wa chakula wa lishe bora kwa jamii pamoja na kutoa tahadhari za mapema juu ya upungufu wa chakula unapojitokeza nchini. Programu ilitekeleza yafuatayo:

Utekelezaji wa Shabaha kwa Mwaka 2017/2018

a) Wanajamii 7,043 kutoka Shehia 101 (Unguja 44 na Pemba 57) za Wilaya ya Kaskazini ‘A’, Micheweni na Chake Chake wamepatiwa mafunzo ya afya na lishe bora;
b) Ukarabati wa ghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula umekamilika na matayarisho ya ununuzi wa vifaa, samani za ofisi na chakula (mpunga) zinaendelea;

c) Ripoti 4 juu ya hali ya chakula na lishe nchini imetolewa na kusambazwa kwa wadau;
d) Ripoti ya hali halisi ya upatikanaji wa chakula kwa Wilaya zote za Zanzibar imekamilika na inatarajia kuwasilishwa katika wilaya husika hivi karibuni;
e) Matayarisho ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Masoko (*Market Information System*) na Bei za Vyakula yameanza na kazi inaendelea.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 programu hii iliombewa jumla ya TZS 455.61 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 236.81 milioni Mishahara na TZS 218.80 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 340.85 milioni (TZS 187.09 milioni mishahara na TZS 153.76 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 75 ya makadirio.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Naibu Spika, programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, maliasili zisizorejesheka, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao sambamba na kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu yetu. Idara inaratibu kazi zake kupitia programu kuu ndogo zifuatazo za Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu na Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu

Programu hii lengo lake ni kusimamia na kuhifadhi misitu, wanyama pori pamoja na mazingira yao.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Maendeleo ya Uhifadhi wa Rasilimali programu ilitekeleza yafuatayo:

a) Kukamilika kwa kanuni za usimamizi na uhifadhi wa misitu na wanyamapori zikiwemo Kanuni ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani, Kanuni ya Hifadhi za Maumbile (Ngezi na Masingini) na Kanuni ya Uhifadhi wa Kimataifa wa Wanyama Waliohatarini Kutoweka *(CITES);*
b) Hekta 25.5 zimepandwa miti katika mashamba ya Serikali kwa msimu wa vuli (Dunga 3.5, Chaani 2 na Masingini 1 na 19 miti ya mikoko) na hekta 210 katika mashamba ya Serikali, maeneo ya wazi, kando kando mwa barabara na maeneo yaliyochimbwa mchanga katika msimu wa masika 2018;
c) Mazizi 10 ya wanyamapori yametambuliwa ambayo yamebainika kuwa na aina nne za wanyama (reptilia 32, samaki 6, mamalia 38 na ndege 27);
d) Doria 104 (56 Unguja na 48 Pemba) zimefanywa na kukamata matukio 92 ya ukataji miti, utumiaji wa msumeno wa moto na matukio 13 yaliripotiwa Polisi, kesi 2 zilifikishwa

mahakamani. Aidha, jumla ya misumeno ya moto 233 (126 Unguja na 107 Pemba) imekamatwa;

e) Miche ya misitu, mikarafuu na matunda 1,597,382 (1,364,267 Unguja na 233,115 Pemba) ilioteshwa katika vitalu vya Serikali;
f) Wafugaji 962 wa nyuki walitambuliwa (524 wanawake na 438 wanaume). Aidha, jumla ya tani 5.3 za asali zimezalishwa kwa mwaka 2017 (Unguja 1.7 na Pemba 3.62);

Mhe. Naibu Spika, programu hii iliombewa jumla ya TZS 2.58 bilioni. (TZS 2.45 bilioni mishahara na TZS 131.92 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 2.09 bilioni (TZS 2.01 bilioni mishahara na TZS 84.13 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 81 ya makadirio.

Programu Ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka

Mhe. Naibu Spika, programu hii lengo lake kuhifadhi na kusimamia matumizi ya maliasili zetu zisizorejesheka.

Utekelezaji wa shabaha kwa mwaka 2017/2018

a) Hekta 7 (4 Zingwezingwe na 3 Manga Pwani) zimepandwa miti ya misitu msimu wa Vuli 2017/2018;
b) Doria 55 (35 Unguja na 20 Pemba) zimefanywa na kukamata matukio 59 ya uchimbaji na usafirishaji maliasili zisizorejesheka yanayojumuisha (33 Mchanga, 6 Kifusi, 5 Gari za Ng'ombe, 4 Kokoto, 2 Mawe, 5 Matofali ya Jasi na 3 Udongo);
c) Kesi ya kughushi nyaraka za malipo ya mchanga inaendelea mahakamani kwa kushirikiana na *ZAECA* ambapo magari 4 yanaendelea kushikiliwa, jumla ya TZS 82,000,000 zimelipwa ikiwa ni faini;
d) Rasimu ya Sera na Sheria ya Maliasili zisizorejesheka zimeandaliwa na kuwasilishwa ngazi ya Wizara kwa mapitio zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS 191.16 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 155.35 milioni kwa matumizi mengineyo, sawa na asilimia 81.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

a) Programu ndogo ya uzalishaji mifugo
b) Programu ndogo ya utabibu wa mifugo

Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo ililenga kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Utekelezaji wa Shabaha za Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2017/2018

a) Mitambo 2 ya *biogas* imejengwa Bungi na Ubago kwa Unguja;
b) Jumla ya kuku 72,531 walipatiwa chanjo ya ugonjwa wa Mahepe Unguja na Pemba;
c) Jumla ya mbwa 2,326 na paka 369 walipatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa *(Rabies)* na wengine 91 (Mbwa 35 na Paka 56) walifungwa uzazi;
d) Wanyama 51,411 walioogeshwa (ng'ombe 17,241, mbuzi/kondoo 5,334, mbwa 2,264, paka 338, Punda 132, kuku 26,100 (Dusting) na sungura 2.
e) Wanyama 72,045 wametibiwa maradhi tofauti (ng'ombe 12,213 mbuzi/kondoo 6,190 mbwa 2,815 paka 885, kuku 49,794, sungura 103 na punda 45);
f) Jumla ya ng'ombe 1,250 walipandishwa kwa sindano Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo hizi ziliombewa jumla ya TZS 2.11 bilioni kati ya fedha hizo (TZS 1.86 bilioni mishahara na TZS 250.00 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 programu zimepata TZS 1.72 bilioni (TZS 1.54 bilioni mishahara na TZS 182.59 milioni kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 82 ya makadirio.

Programu Ndogo ya Wakala wa Tafiti za Mifugo –*ZALIRA*

Utekelezaji wa Shabaha za Programu ya Wakala wa tafiti za Mifugo 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, Wakala wametiliana saini na Chuo cha Mafunzo kukarabati majengo ya ofisi kuu ya *ZALIRA* Kizimbani;

a) Watafiti wawili wamepatiwa mafunzo ya uandishi wa miradi ya utafiti;
b) Kukamilika kwa utafiti wa uzito wa ng'ombe na nyama ambapo matokeo ya awali yanatarajiwa kutolewa mwezi wa Juni, 2018;
c) Ukarabati wa mabanda ya kufanyia tafiti za kuku na mbuzi unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Juni, 2018;
d) Rasimu ya Mpango Mkakati wa *ZALIRA* umetayarishwa na unapitiwa na wadau.

Mhe. Naibu Spika, programu hii iliombewa jumla ya TZS 500.00 milioni kwa ajili ya ruzuku. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 434.05 milioni sawa na asilimia 87 ya makadirio.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji.

Programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

a) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari.
b) Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini.

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, programu ndogo hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

a) Jumla ya doria 174 zilifanyika, kati ya hizo, doria 50 ni za kuangalia leseni za vyombo vya uvuvi na doria 124 za ukaguzi wa tiketi za wageni ziliendelea kufanyika kisiwani Mnemba, Kizimkazi na Fumba;
b) Taaluma ya uhifadhi ilitolewa kwa kufanya mikutano tisa (9) kwa kamati za uvuvi maeneo ya hifadhi nchini;
c) Utafiti wa kujua kiwango cha samaki katika maji ya ndani unaendelea kufanywa kwa awamu, ikiwa pamoja na kujua aina za samaki tulionao kupitia mradi wa SWIOFish. Aidha, maeneo mapya ya hifadhi ya Tumbatu *(TUMCA)* na Changu Bawe *(CHABAMCA)* yameanzishwa na mipaka ya hifadhi kongwe za *MIMCA* na *MENAI* imefanyiwa marekebisho;
d) Mafunzo ya ufugaji wa kaa na majongoo yalitolewa kwa washiriki 34 (wanawake 13 na wanaume 21), mafunzo hayo yalihusu njia bora za ufugaji, ujenzi wa uzio kwa ajili ya kufugia majongoo na vizimba vya kufugia kaa; na programu ilisimamia utekelezaji wa mradi mmoja wa *SWIO fish***.**

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2017/2018, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Hifadhi za Baharini iliombewa TZS 10.84 bilioni kati ya hizo TZS 1.16 bilioni ziliombwa kwa kazi za kawaida (mishahara TZS 848.71 milioni na matumizi mengineyo TZS 158.40 milioni), TZS 9.83 bilioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS 290.00 milioni ni kutoka SMZ na TZS 9.54 Bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia April 2018, Programu imepatiwa TZS 851.68 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 73 ambapo (TZS 724.65 mshahara na TZS 127.03 matumizi mengineyo). Aidha, programu imepata TZS 1.44 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 90.00 milioni kutoka SMZ, sawa na asilimia 15 ya makadirio.

Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Mazao ya Baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Utekelezaji wa Shabaha za Programu Ndogo ya Ufugaji wa Mazao ya Bahari kwa Mwaka 2017/2018

a) Wafugaji wa mazao ya baharini 52 wamepatiwa mafunzo ya mwezi mmoja kuhusu ufugaji wa chaza, kaa, majongoo na samaki;
b) Wizara imesaidia ujenzi wa miundombinu ya mabwawa na kuwapatia pampu wafugaji wa samaki;
c) Wizara inaendelea na utaratibu wa zabuni wa ununuzi wa gari maalum ya kusambazia vifaranga vya samaki Pemba.
d) Jumla ya tani 10,455.01 zenye thamani ya TZS 7.19 bilioni za mazao ya baharini yalisafirishwa nchi za nje ikiwemo pweza, mwani, dagaa, chaza na samaki.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya ufugaji wa mazao ya baharini iliidhinishiwa TZS 2.86 bilioni kati ya hizo TZS 157.19 milioni kwa kazi za kawaida. TZS 2.70 bilioni kwa kazi za maendeleo ambapo TZS 200.00 milioni ni kutoka SMZ na TZS 2.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 109.42 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 2.5 bilioni kwa kazi za maendeleo, sawa na asilimia 91 ya makadirio.

KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR *(ZAFICO)*

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la Kampuni ya Uvuvi ni kuanzisha uvuvi wa kibiashara kwa kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya uvuvi na kuelekeza nchi yetu katika uchumi wa Buluu na kuweza kuvua samaki katika bahari kuu.

Utekelezaji wa Shabaha Kampuni ya Uvuvi ya *ZAFICO* 2017/2018

Kampuni imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kukamilika uzinduzi wa bodi ya kampuni ya *ZAFICO*
b) Kuanza utaratibu wa kutayarisha Mpango wa Kibiashara wa Kampuni.
c) Utayarishaji wa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Kampuni.
d) Kuanza utaratibu wa ununuzi wa meli ya uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar *(ZAFICO)* inategemewa kutumia Jumla ya TZS 7.0 bilioni zitakazochangiwa na mashirika ya ndani ya Zanzibar ikiwemo *ZSSF, ZSTC,* BIMA na Shirika la Bandari.

PROGRAMU YA UTAWALA, MIPANGO NA USIMAMIZI WA KAZI ZA WIZARA

Mhe. Naibu Spika, programu hii inayojumuisha programu ndogo tatu ambazo zinasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Ofisi Kuu Pemba.

Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara

Mhe. Naibu Spika, dhumuni la programu hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti. Idara pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Programu imetekeleza yafuatayo:

a) Mapitio ya Rasimu ya Será ya Kilimo (2002) ya Zanzibar yamefanyika pamoja na kupata maoni ya wadau kwa Unguja na Pemba;
b) Mpango Mkakati wa Wizara (2017-2020) umeandaliwa na umekamilika;
c) Mapitio ya Sheria ya Uhifadhi na Utibabu wa Mimea yamekamilika na inasubiri maoni ya Mwanasheria Mkuu;
d) Kusimamia utekelezaji wa programu na miradi ya Programu ya *MIVARF;* Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga - *ERPP,* Mradi wa *(ZANRICE)* na Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo;
e) Utayarishaji wa programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *Z-ASDP* umeanza na utaendelea mwaka 2018/19 ambapo Mshauri Muelekezi kutoka *FAO* atasaidia utayarishaji huo;
f) Tathmini ya vikundi 119 kwa ajili ya kupatiwa mikopo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. Aidha, jumla ya Tsh. Milioni 108,000,000 zimetolewa mkopo kwa vikundi 54 vya uzalishaji wa mazao ya mboga na matunda;
g) Jumla ya miradi mitano (5) mipya imeanzishwa kwa lengo la kuendeleza sekta ya kilimo na maliasili ikiwemo Mradi wa Kuunganisha Sekta Binafsi katika Kilimo *(Agri Connect),* Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu *(Aflatoxin),* Mradi wa Kilimo cha Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi *(Climate Smart Agriculture),* Mradi wa Matunda na Mboga na Mradi wa Uimarishaji wa Usimamizi na Matumizi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani;
h) Kukamilika kwa kalenda ya upandaji na uvunaji wa mazao pamoja na utoaji wa Jarida la Kilimo toleo namba 17;
i) Uundaji wa Baraza la Utafiti kwa Sekta ya Kilimo umekamilika.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya TZS 9.82 bilioni. TZS 547.20 milioni kwa kazi za kawaida ambapo (TZS 338.06 Milioni mishahara na TZS 209.13 milioni matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo program ilitarajia kupata TZS 8.63 bilioni kwa miradi ya maendeleo TZS 1.52 bilioni kutoka SMZ na TZS 7.11 bilioni kutoka washirika wa maendeleo. Hadi kufikia April, 2018 programu imepata jumla ya TZS 449.27 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 82 ambapo (TZS 282.93 milioni mishahara na TZS 166.34 milioni matumizi mengineyo). Aidha, programu imepata TZS 4.49 bilioni kwa miradi ya maendeleo, TZS 1.18 bilioni kutoka SMZ na TZS 3.31 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo, sawa na asilimia 52 ya makadirio.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya utawala na uendeshaji imetekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Madhumuni ya programu hii ni kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu pamoja na mazingira mema ya kufanyia kazi. Aidha,

programu inaratibu masuala mtambuka ikiwemo Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

Utekelezaji wa Shabaha Mwaka 2017/2018

a) Watumishi 419 wamepatiwa maslahi yao ikiwemo likizo na ubani wa wafiwa kwa Unguja na Pemba;
b) Jumla ya magari 63, trekta 54 na pikipiki 217 zimehakikiwa na mashamba/nyumba (madiko) 34 yamepatiwa hatimiliki;
c) Jumla ya wafanyakazi 24 wanaendelea na masomo ya udaktari wa wanyama nchini China, nfanyakazi mmoja (1) Urusi na wafanyakazi 42 wanaendelea na masomo katika fani tofauti ndani na nje ya nchi;
d) Maonesho ya kilimo katika kuadhimisha siku ya chakula duniani yalifanyika kuanzia tarehe 10/10/2017 hadi tarehe 17/10/2017.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2017/2018, programu ndogo hii iliombewa jumla ya TZS 2.36 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.70 bilioni mishahara na TZS 660.00 milioni kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 programu imepatiwa TZS 2.18 bilioni (TZS 1.43 bilioni mishahara na TZS 752.73 milioni kwa kazi za kawaida) sawa na asilimia 92.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba

Mhe. Naibu Spika, programu hii inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, lengo lake ni kuratibu na kusimamia kazi na rasilimali za Wizara kwa kufuata misingi ile ile ya Sheria. Programu hii ndogo inatoa huduma za utumishi za Wizara, kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Programu hii iliombewa jumla ya TZS 4.14 bilioni (TZS 4.07 bilioni mishahara na TZS 62.09 milioni ni matumizi mengineyo). Hadi kufikia April, 2018 programu imepata TZS 3.52 bilioni (TZS 3.29 bilioni mishahara na TZS 234.01 milioni matumizi mengineyo) sawa na asilimia 85.

CHANGAMOTO

Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada za Wizara na Serikali kwa ujumla, kulikuwa kumejitokeza baadhi ya changamoto kama ifuatavyo. Changamoto hizi nazo zimechukuliwa hatua katika kukabiliana nazo kama ifuatavyo:

a) Uchelewaji wa upatikanaji wa pembejeo, matrekta na michango ya wakulima katika huduma za kilimo.

b) Ongezeko la ukataji wa miti na matumizi ya misumeno ya moto.

c) Ukosefu wa ardhi na upatikanaji wa mitaji ya kuwavutia vijana katika sekta ya kilimo.

d) Kiwango kikubwa cha mvua kutoka milimita 276 mwaka 2016 hadi kufikia milimita 670 mwaka 2017, ikilinganishwa na kiwango cha mvua zilizonyesha miaka minane iliyopita.
e) Kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu.

f) Kushuka kwa bei na mripuko wa maradhi ya mwani.

g) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika uwekezaji wa kilimo.

h) Upungufu wa wataalamu katika kada maalum.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na uchelewaji wa upatikanaji wa pembejeo na michango ya wakulima katika huduma za kilimo, wizara imo katika mchakato wa kusaini Mkataba wa Maelewano *(Memorandum of Understanding)* na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) katika uzalishaji wa mbegu bora na imesaini *MOU* na taasisi ya *TOSTI* ya Tanzania Bara kupitia Taasisi za Utafiti wa Kilimo kwa lengo la uthibiti ubora wa mbegu zinazozalishwa hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na changamoto matumizi mabaya ya misumeno ya moto. Wizara inasimamia utekelezaji wa kanuni ya upigaji marufuku misumeno kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Serikali za Wilaya na Mkoa.

Kulikuwa na changamoto ya ukosefu wa ardhi na upatikanaji wa mitaji ya kuwavutia vijana katika sekta ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na mfuko wa uwezeshaji na *TGT* inaendelea kwa pamoja kuwahamasisha na kuwawezesha kwa kuwapatia mikopo yenye riba nafuu. Vile vile programu ya *MIVARF* imeiwezesha baadhi ya vikundi kwa uzalishaji wa mazao kwa kuwapatia mashine za usarifu. Aidha, kwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania *(TADB)* imeainisha na kutathmini vikundi mia moja kumi na tisa (119) kwa lengo la kuvipatia mikopo.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na changamoto ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kama nilivyoeleza hapo nyuma wizara inaendelea na tafiti mbali mbali na kutoa elimu ya kilimo na umwagiliaji maji kwa mpunga na mazao mengine ya pamoja ili kuhakikisha wakulima wanavuna maji ya mvua.

Changamoto ya kuendelea kuwepo kwa uvuvi haramu wizara inashirikiana na Kamati ya Uvuvi na Wilaya katika kudhibiti na kuimarisha ulinzi katika maeneo ya Hifadhi ya Bahari ikiwemo *MENAI, MIMCA, PECA.* Aidha, wizara nayo imeongeza jitihata ya kuweka hifadhi za *TUMCA* na *CHABAMCA* kwa ajili ya kuimarisha ulinzi zaidi katika maeneo ya uvuvi.

Kushuka kwa bei na mripuko wa maradhi ya mwani kama ilivyoelezwa na Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda hapo jana katika bajeti yake hili ni la Wizara ya Kilimo itakuja kutoa jibu. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imekamilisha utafiti wa maradhi ya mwani kwa kushirikiana na *FAO* na kubaini ya kwamba maradhi hayo yanatokana na mabadiliko ya tabia nchi (kupanda na kushuka kwa joto katika maji ya bahari na matumizi ya mbegu rejea ya aina moja ya mwani). Aidha, Serikali imo mbioni

katika juhudi za kuwapatia vihori 20 wakulima wa mwani ili waweze kwenda kina kirefu kidogo na kupanda aina ya mwani.

Katika changamoto iliyoshirikisha udogo wa Sekta binafsi katika kutoa huduma za kilimo kwa tathmini.

Mhe. Naibu Spika, kutathmini mchango wa sekta wizara katika maendeleo ya kiuchumi, Wizara inaendelea kushirikiana pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza kilimo.

Changamoto katika upungufu wa wataalamu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaendelea na utekelezaji wa kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake nafasi za masomo katika fani maalumu zinazohitajika kila mwaka kulingana na hali ya fedha inavyoweza kuruhusu pamoja kuajiri wataalamu kupitia nafasi zilizowazi.

Mhe. Naibu Spika, utelekezaji wa Programu za Wizara ya kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2017/2018 changamoto nilizozieleza na hatua zilizochukuliwa katika muongozo huo kuzitekeleza changamoto hizo zinaonekana vizuri kabisa palipoanzia ukurasa wa kumi na sita (16) hadi arubaini na mbili (42) ambazo naliomba Baraza lako Tukufu kuzichukua *hansard* hizo na kuziweka kama zilivyo kwenye kitabu cha hotuba yangu.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU PPB KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

MAKADIRIO YA MAPATO 2018/2019

Mhe. Naibu Spika,kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara pamoja na jitihada kubwa iliyofanya mwaka jana wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS 12.50 bilioni kutoka vianzio vyake vya Unguja na Pemba (kama inavyooneysha kiambatisho nam. 10).

MAKADIRIO YA MATUMIZI 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa ajili ya kuwasilisha baraka na bajeti ya Wakulima, Wavuvi, Wafugaji Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 inatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu tano kama zilivyo mwaka jana ambazo ni:

a) Programu ya Maendeleo ya Kilimo.
b) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka.
c) Programu ya Maendeleo ya Mifugo.
d) Programu ya Maendeleo ya Uvuvi na
e) Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo kwa wakulima wake, wavuvi na wafugaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutekeleza programu hizo kwa mwaka wa fedha wa 2018/19 Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 62.62 bilioni ambazo nawaomba sana waheshimiwa wako wazipitishe bila ya tatizo lolote. Kati ya fedha hizo TZS 23.23 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS 14.45 bilioni Mishahara, TZS 5.66 bilioni matumizi ya kazi za kawaida na TZS 3.13 bilioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta (kama kinavyoonesha kiambatisho Nam. 11).

Kwa upande wa fedha za maendeleo jumla ya TZS 33.73 bilioni ni kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS 5.65 bilioni kutoka kwa serikali yetu tukufu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kiambatisho Nam. 12 inaonesha hivyo.

Wizara katika kuendeleza kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejiwekea malengo yafuatayo:

Kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka tani 39.683 kadi kufikia tani 45,000 katika eneo la ekari 33,800 (20,800 zikiwa Pemba na 13,000 zikiwa Unguja).

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kuyaeleza haya kwa kina ili kuweka sawa suala zima lile linalosema kwamba Zanzibar tunaweza tukajitosheleza kwa mpunga na *statement* iliyokuwepo katika Baraza lako. Hivyo, tumeziweka ekari hizo bado tunaendelea na jitihada ya kuimarisha kilimo cha mpunga.

Lakini vile vile kuwezesha kuotesha miche 2,500,000, kuendeleza uzalishaji wa minazi, alizeti na viungo ikiwemo vanila, pilipili hoho, manjano, tangawizi na nyenginezo. Vile vile kupitia Wakala wa Matreka wizara itaendelea kutoa huduma za matrekta na zana za kilimo ambapo kwa k0uchimba na kuburuga ekari 21,000 (ikiwa 13,000 Unguja na 8,000 Pemba).

Lakini vile vile kuanzisha mashamba ya mbegu za miche ya minazi (ekari 3 Unguja na ekari 3 Pemba). Kukamilisha utaratibu wa Chuo cha Kilimo Zanzibar kujiunga na *SUZA* pamoja na kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Tunategemea chuo chetu kujiunga na *SUZA* ili kiweze kutoa mafunzo yenye shahada za juu zaidi.

Mheshimiwa vile vile kuna kutoa taaluma ya mbinu bora za ufugaji na usarifu wa mazao ya baharini kwa vikundi 144 Unguja na Pemba pamoja na kuzalisha na kusambaza vifaranga milioni 10 vya samaki, 50,000 kaa na 70,000 majongoo kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi kupitia Kampuni ya *ZAFICO* na kuendeleza wavuvi vijana kuvua katika kina kirefu cha maji pamoja na kuwawekea miundombinu bora kupitia Kampuni ya *ZAFICO*.

Lakini pia kuna kuimarisha huduma za utafiti wa kilimo pamoja na kinga, tiba na uzalishaji wa mifugo. Aidha, kufanya tafiti ili kutambua maeneo ya uvuvi yenye idadi kubwa ya samaki.

Mhe. Naibu Spika, mwisho ni kuendelea na Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane Unguja na Kuanzisha Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani huko Pemba. Naomba nichukue fursa hii kuwaalika waheshimiwa wako wote wa Baraza lako la Wawakilishi siku ya nane nane kushiriki katika maonesho hayo ya kilimo.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo imegawika katika programu ndogo nne ambazo ni:

a) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji.

b) Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo.

c) Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

d) Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ya Maendeleo ya Kilimo inaombewa jumla ya TZS 19.11 bilioni kati ya fedha hizo TZS 3.25 bilioni matumizi mengineyo, TZS 4.56 bilioni ni Mishahara na TZS 2.30 bilioni ni kwa ajili ya Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani na Wakala wa Huduma za Matrekta. Vile vile, Programu inaombewa jumla ya TZS 9.0 bilioni kwa Miradi ya Maendeleo TZS 8.5 bilioni kutoka kwa Washirika wetu wa maendeleo na TZS 500 milioni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji Maji kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji hekta 200 (150 Unguja na 50 Pemba) pamoja na hekta 520 kupitia mradi wa *EXIM BANK* wa Korea.

b) Uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa umwagiliaji mabonde ya Chaani, Mwera, Mwanakombo, Kianga na Weni.

c) Kuchangia utekelezaji wa mradi wa *ERPP* kwa uungaji umeme wa laini kubwa katika mabonde ya Kibondemzungu, Mchangani, Koani na Bandamaji kwa Unguja na Dobi, Ole na Machigini kwa Pemba.

d) Ulipaji wa fidia ya mazao kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji Zanzibar katika mabonde ya Makwararani na Mlemele kwa Pemba na Kinyasini, Kilombero na Chaani kwa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS 10.11 bilioni ambapo TZS 7.11 Mshahara, TZS 400.00 milioni kwa matumizi mengineyo. Aidha TZS 500.00 milioni fedha za maendeleo kutoka SMZ na TZS 8.5 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo *EXIM BANK.*

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019, programu ndogo hii ina sehemu mbili ambazo ni Utafiti na ile ya Mafunzo ya Kilimo. Programu ndogo hii inalenga kutekeleza yafuatayo:

a) Kufanya tafiti nne (4) mpya za (mpunga 1, muhogo 1, mboga na mazao ya viungo) na kuendeleza tafiti sita za zamani.

b) Kukarabati jengo moja la ofisi Matangatuani Pemba na kuanza ujenzi wa uzio wa kuzunguka eneo la Kizimbani, kukarabati nyumba za wafanyakazi za Kizimbani na Matangatuani na kununua vifaa na madawa kwa ajili ya maabara mbili (2) ziliopo.

c) Lakini vile vile ni kuimarisha rasilimali watu kwa kufundisha watafiti 10 mafunzo ya muda mfupi;

d) Kushiriki katika Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane, Siku ya Chakula Duniani, Maonesho ya Biashara na katika Sherehe za Mapinduzi;

e) Kukamilisha Mapitio ya Sheria Nam. 8 ya Taasisi ya Utafiti, kukamilisha Muundo wa Utumishi *(Scheme of Service)* wa Taasisi na Kupitia Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo;

f) Kufanya ziara moja ya kujitambulisha na kubadilishana uzoefu na taasisi kama yetu Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 Taasisi ya Utafiti inaombewa jumla ya TZS 2.24 bilioni (TZS 1.92 bilioni Mshahara na 315.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa Mwaka 2018/2019

a) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi wapya 230 (100 ngazi ya Stashahada na 130 ngazi ya Astashahada);

b) Kukamilisha utaratibu wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kujiunga na *SUZA*;

c) Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mpunga katika skimu ya huko Uzini na Kianga kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II*;

d) Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji na wa kutegemea mvua kwa wakulima 100. Mafunzo haya yatatolewa kwa kushirikiana na mradi wa *TANRICE II.*

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu inaombewa TZS 928.00 milioni ikiwa ni Ruzuku kwa kazi za kawaida (TZS 812.70 milioni Mishahara na TZS 115.30 milioni matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Kilimo Mwaka 2018/2019

a) Kununua na kusambaza tani 200 za mbegu ya mpunga, tani 650 za mbolea (*TSP* tani 150 na *UREA* tani 500), tani 20 za mahindi, tani 10 za mtama, lita 5,000 za dawa ya kuulia magugu na lita 400 za dawa ya kunasia nzi waharibifu wa matunda.

b) Kutoa elimu ya uzalishaji katika zao la mpunga kupitia mabonde 10 ya mpango (6 Unguja na 4 Pemba).

c) Kufuatilia uzalishaji wa mpunga katika eneo la ekari 33,800 (20,800 Pemba na Unguja 13,000).

d) Kusambaza mbegu ya muhogo na viazi lishe kwa wakulima 500.

e) Kutoa huduma za utibabu wa mimea, karantini na ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi ikiwemo karafuu

f) Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo vanila, pilipili hoho, manjano, tangawizi na pilipili manga katika hekta tano za mashamba ya mipira Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu inaombewa TZS 3.68 bilioni kwa Kazi za Kawaida ikiwa TZS 1.70 bilioni ni Mishahara na TZS 1.98 bilioni kwa matumizi mengineyo**.**

Shabaha Zitakazotolewa na Wakala wa Matrekta na Maendeleo ya Huduma za Kilimo kwa Mwaka 2018/2019

a) Kusimamia na kurahisisha upatikanaji na matumizi ya zana za kisasa za kilimo zitakazopelekea kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

b) Kutoa huduma za matrekta na zana zake kwa wakulima, sekta binafsi na taasisi nyengine.

c) Kutengeneza matrekta na zana zake na kuhakikisha kuwepo kwa vifaa vya kazi na vipuri kwa ajili ya huduma.

d) Kutoa mafunzo kwa madereva 20 (14 Unguja na 6 Pemba) na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wasimamizi wa huduma za matrekta mashambani.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS 1.37 bilioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 644.70 milioni ni mshahara na TZS 725.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhakika wa Chakula na Lishe kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Naibu Spika**,** mwaka wa fedha 2018/2019, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuendeleza mafunzo ya lishe kwa wanajamii katika shehia 100 za Wilaya za Micheweni, Chake Chake na Kaskazini 'A'.

b) Kufanya matayarisho (michoro na *BOQ*) ya ukarabati wa ghala moja liliopo Pemba kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

c) Kufuatilia hali ya chakula nchini.

d) Kuandaa mikutano ya wadau kuhusiana na masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

e) Kuratibu uendeshaji wa ghala la akiba ya chakula Unguja pamoja na kuweka vifaa na mchele tani 600;

Mhe. Naibu Spika, programu hii mwaka wa fedha 2018/2019 inaombewa jumla ya TZS 777.8 milioni kwa kazi za kawaida (TZS 227.8 milioni Mshahara na TZS 550.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASLIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni:

a) Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu.
b) Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ya Maendeleo ya Misitu inaombewa jumla ya TZS 2.43 bilioni kwa kazi za kawaida ambapo TZS 1.93 bilioni ni mishahara na TZS 500 milioni matumizi mengineyo.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Naibu Spika**,** mwaka wa fedha 2018/2019, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuotesha miche 2,500,000 (1,000,000 mikarafuu; 1,000,000 misitu; 200,000 minazi na 300,000 ya matunda na viungo) katika vitalu vya Serikali.

b) Kuhamasisha wafugaji 200 wa nyuki juu ya usarifu wa bidhaa za asali, kukabiliana na wadudu wavamizi katika mizinga pamoja na kuwaorodhesha kwa lengo la kujua idadi yao na tani za asali zinazozalishwa.

c) Kufanya mapitio ya mikataba 18 ya usimamizi wa misitu ya jamii *(CoFMA)*.

d) Kuhamasisha uwekezaji na kutangaza vivutio vya utalii wa kimaumbile ndani na nje ya Zanzibar ili kufikia watalii 45,000.

e) Kufanya doria 500 katika maeneo ya maliasili kwa lengo la kudhibiti matukio ya uhalifu.

f) Kufanya utafiti na tathmini ya matumizi ya rasilimali za misitu ya jamii.

g) Kuyatambua na kusajili mazizi ya wanyama pori pamoja kukamilisha kanuni za kusimamia mazizi ya wanyama hao.

h) Kutayarisha muongozo wa uhifadhi wa Makobe katika kisiwa cha Changuu.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu hii inaombewa jumla ya TZS 2.07 bilioni kwa kazi za kawaida (TZS 1.93 bilioni ni mishahara na TZS 143.00 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka kwa Mwaka 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, programu hii ina lengo la kuhifadhi na kusimamia maliasili zisizorejesheka kwa kuratibu maeneo yote ya uchimbaji mawe, kokoto, mchanga, udongo pamoja na matofali ya mawe. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka kwa Mwaka 2018/2019

a) Kurejeshea kwa kupanda miti hekta 40 katika maeneo ya uchimbaji.

b) Kukamilisha Sera na Sheria ya Maliasili Zisizorejesheka.

c) Kufanya utafiti juu ya namna bora ya urasimishaji na usimamizi katika uchimbaji wa kifusi, mawe na usagaji wa kokoto.

d) Kutathmini mazao na vipando vilivyopo katika maeneo yatakayopendekezwa katika kuchimbwa mchanga.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019 programu ndogo hii inaombewa jumla ya TZS 357.00 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Mifugo ina jukumu la kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Mhe. Naibu Spika, programu hii imegawika katika programu ndogo mbili:

a) Programu Ndogo ya Uzalishaji Mifugo
b) Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ya Maendeleo ya Mifugo inaombewa jumla ya TZS 3.66 bilioni ikiwa TZS 1.68 bilioni Mshahara, TZS 300.00 milioni kwa matumizi mengineyo. Aidha, imeombewa TZS 828.9 milioni ikiwa ni Ruzuku na TZS 856.00 milioni ni fedha za programu ya miundombinu ya mifugo.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Uzalishaji wa Mifugo kwa Mwaka 2018/2019

a) Kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mifugo.
b) Kupandisha ng'ombe 4,000 kwa sindano (Unguja 2,000 na Pemba 2,000);
c) Kujenga mitambo 4 ya *biogas* Unguja na Pemba;
d) Kuimarisha malisho kwa kupanda majani katika maeneo ya Maruhubi, Kizimbani na Chamanangwe;
e) Kuwaendeleza madaktari wa mifugo vijijini (*CAHWS*) pamoja na kusimamia maduka ya pembejeo za mifugo zilizoanzishwa na Programu ya *ASDP-L.*
f) Kutoa elimu na kuziendeleza skuli za wakulima za mazao na mifugo.
g) Kushajihisha ujenzi wa vituo vya ukusanyaji na usarifu wa maziwa kwa mafugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo hii ya Uzalishaji wa Mifugo inaombewa jumla ya TZS 1.054.5 bilioni, kati ya fedha hizo (TZS 198.5 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TZS 856.00 milioni ikiwa ni fedha za programu ya miundombinu ya mifugo).

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo kwa Mwaka 2018/2019

a) Kuchanja kuku 600,000 dhidi ya ugonjwa wa mahepe Unguja na Pemba;
b) Kuchanja mbwa 11,000 dhidi ya kichaa cha mbwa (8,000 Unguja na 3,000 Pemba);
c) Kutoa huduma ya maabara ya mifugo;

d) Kuimarisha huduma za kinga na tiba.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya TZS 1.78 bilioni kwa kazi za kawaida ambapo TZS 1. 68 bilioni Mishahara na TZS 101.5 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu Ndogo ya Wakala wa Tafiti za Mifugo

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu ndogo ya Wakala wa tafiti za Mifugo (*ZALIRA*) inalenga kuratibu na kuendeleza tafiti za sekta ya mifugo.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Wakala wa Tafiti za Mifugo

a) Kuimarisha miundombinu ya Wakala wa Taasisi ya Utafiti;
b) Kuimarisha mahusiano ya Taasisi za ndani, Kikanda, Kitaifa na Kimataifa na wadau wa Sekta ya Mifugo;
c) Kuwapatia mafunzo watafiti 12 (9 Unguja na 3 Pemba);
   Kufanya tafiti sita (6) za Mifugo Unguja na Pemba;
d) Kuchapisha na kuhifadhi taarifa na matokeo saba ya utafiti; na
e) Utayarishaji wa Sheria ya Uanzishwaji Taasisi ya Utafiti wa Mifugo.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Wakala wa tafiti za Mifugo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, inaombewa jumla ya TZS 828.90 milioni ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini (TZS 303.90 milioni ni mshahara na TZS 525.00 milioni kwa matumizi mengineyo).

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu hii inaombewa jumla ya TZS 20.76 bilioni (TZS 790.99 milioni ni Mishahara**,** TZS 450 milioni ni matumizi mengineyo. Mheshimiwa TZS 3.92 bilioni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ na TZS 15.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo).

Programu Ndogo ya Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya mazao ya baharini inalenga kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo hii:

a) Kutoa taaluma ya mbinu bora za ufugaji na usarifu wa mazao ya baharini kwa vikundi 144 Ungujaa Pemba;
b) Kuzalisha na kusambaza vifaranga vya samaki na mazao mengine ya baharini kwa wananchi;

c) Kusambaza vifaa kwa vikundi 30 vya wakulima na usarifu wa zao la mwani na vikundi 3 vya wafugaji wa samaki pamoja na ununuzi wa vihori 20;
d) Kukusanya taarifa za uvuvi wa bahari kuu kwa kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika u vuvi huo;
e) Kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kuendeleza kazi za uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ndogo **ya** kuimarisha ufugaji wa mazao ya baharini inaombewa TZS 284.6 milioni kwa matumizi mengineyo**.**

Programu Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi za Baharini

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na hifadhi za baharini inalenga kuendeleza uvuvi wa kienyeji na kusimamia rasilimali za baharini kwa matumizi endelevu. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu ndogo hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi 8 ili kuimarisha taaluma za uvuvi;
b) Kuimarisha doria shirikishi 174 katika maeneo ya hifadhi Unguja na Pemba;
c) Kuimarisha uvuvi unaozingatia uhifadhi wa mazingira wa kamati 88 za uvuvi Unguja na Pemba;
d) Kusimamia ujenzi wa soko kuu la samaki linalojengwa diko la Malindi; kulenga kwenda katika uvuvi wa viwanda *(Semi Industrial)* kwa lengo la kupata tija zaidi na kuinua kipato cha mvuvi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ndogo hii inaombewa TZS 20.48 bilioni (TZS 790.99 milioni ni mishahara, TZS 165.4 milioni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TZS 3.92 bilioni kutoka SMZ kwa miradi ya maendeleo na TZS 15.6 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Aidha, kwa mwaka 2018/19 program itasimamia miradi ya *SWIOfish* na Mradi wa Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini. (Angalia kiambatisho nam. 13 & 14)

PROGRAMU KUU YA MIPANGO NA UTAWALA WA KAZI ZA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Mipango na Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi kwa ustawi wa sekta za kilimo na kuwafanya wafanyakazi wafanye kazi katika mazingira mazuri.

Programu imegawika katika program ndogo tatu nazo ni:

a) Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti
b) Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi;
c) Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi Kuu ya Pemba.

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu ya Mipango na Utawala inaombewa jumla ya TZS 17.26 bilioni **(**TZS 6.10 bilioni ni mshahara, TZS 1.20 matumizi mengineyo, TZS 380.0 milioni ni kwa miradi ya maendeleo kutoka SMZ na TZS 9.63 bilioni kutoka kwa Washirika wetu wapendwa wa maendeleo).

Programu Ndogo ya Mipango na Usimamizi wa Kazi za Wizara

Mhe. Naibu Spika, Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za mipango sera na utafiti kwa maendeleo ya sekta za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2018/2019, Programu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

a) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili; na kwa wale wote ambao wameuliza swali yatapatikana hapa kwa mwaka 2018/2019;
b) Kufanya tafiti tatu (2 Pemba) za kiuchumi na kijamii kuhusu mwenendo wa ushiriki wa vijana katika kilimo Unguja na Pemba;
c) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera na Programu za kupunguza umaskini katika kilimo na kuongeza kipato cha wakulima;
d) Kufanya ziara za Ufutiliaji na tathmini za kazi za wizara M&E
e) Kushiriki katika mikutano sita (6) ya mashirikiano na Wizara za Sekta ya Kilimo Tanzania Bara, kikanda, kimataifa na Kitaifa;
f) Kufanya mikutano minane (8) ya Kamati ya Utafiti;
g) Kuendelea na utayarishaji wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar *Z-ASDP*;
h) Kuendelea kusimamia Programu na Miradi yote iliyo chini ya Wizara

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Mipango inaombewa jumla ya TZS 10.75 bilioni (TZS 343.7 milioni mishahara, TZS 400.00 milioni kwa matumizi mengineyo, TZS 380.0 milioni kutoka SMZ kwa ajili ya Miradi ya maendeleo na TZS 9.63 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo). Aidha, kwa mwaka 2018/19 program itasimamia miradi ya *MIVARF*, *ERPP*, *ZANRICE*, *Agri-Connect*, *Aflatoxin*, *Climate Smart Agriculture* na Mradi wa Matumizi ya Misitu ya Mwambao. (Angalia kiambatisho 15, 16, 17 & 18).

Programu ya utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo maliasili mifugo na uvuvi

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya utawala na mafunzo ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta za kilimo, misitu, mifugo na uvuvi.

Shabaha Zitakazotolewa na Programu Ndogo ya Utawala na Mafunzo kwa Mwaka 2018/2019

a) Kutoa maslahi kwa wafayakazi 1,200 na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi;

b) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma Wafanyakazi 67 wanaoendelea na masomo na 35 wapya**.**
c) Udhibiti na ufuatiliaji wa mali za serikali, ambazo zinaonekana zimezagaa sana.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya utawala na mafunzo, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, inaombewa jumla ya TZS 2.52 bilioni kwa kazi za kawaida, TZS 1.83 bilioni ni mishahara na TZS 688.00 milioni kwa matumizi mengineyo.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo na shughuli zote za sekta ya kilimo, maliaisli, mifugo na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango ya Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Programu hii inaombewa kutumia jumla ya TZS 3.37 bilioni sawa na TZS 3.30 bilioni mishahara na TZS 70.00 milioni ni matumizi mengineyo.

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaomba kuidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 62.62 bilioni kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019,

Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka *hansard* sawa, huu ni muhtasari wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaomba kuidhinishiwa jumla TZS 62.62 bilioni kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kati ya fedha hizo TZS 23.23 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS 14.45 bilioni itakuwa ni kwa mishahara, TZS 5.66 bilioni matumizi ya kazi za kawaida na TZS 3.13 bilioni ikiwa ni Ruzuku kwa ajili ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo wizara imeidhinishiwa jumla ya TZS 39.39 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 5.65 bilioni ni kutoka Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar na TZS 33.73 bilioni ni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

SHUKRANI

Mhe. Naibu Spika, baada ya uwasilishaji naomba nitumie nafasi hii tena kuzishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika juhudi za kuendeleza Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Hifadhi ya Maliasili Zetu na kuwajali wakulima, wakwezi na wavuvi. Katika taasisi hizo zikiwemo nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Mauritius, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Oman na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya kilimo nchini. Vile vile nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *ICRAF*, *IFAD*, *UNDP*, *FAO*, *JICA*, *UNICEF, WFP, USAID, KOICA, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, Rockfeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation, GIZ, WAP, WHO,* Shirika la Mionzi la Ulimwengu (*IAEA),*

Indian Ocean Rim, *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* na Umoja wa nchi za Ulaya *(EU).* Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado unauhitajika ili tuendeleze sekta ya kilimo nchini.

Vile vile, tunazishukuru taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili, Mifugo na Uvuvi zikiwemo *ZSTC*, TAHA, UWAMWIMA, ZAIDI, *COSTECH*, *Milele Foundation, Kilimo Trust, CARE,* Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania Bara, *CARI*, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ushirikiano ya Afrika Mashariki, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya Tanzania, Taasisi ya Sayansi ya Baharini, *State Oceanic Administration* (*SOA*) ya China, *Heifer Project Tanzania, Zanchick, ZAASO, ZSPCA* na *WIOMSA.*

Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wanakamati za hifadhi za maliasili zetu kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mifugo na mazao ya baharini, pamoja na mazingira magumu waliyonayo na wanayokabiliana nayo. Mwenyezi Mungu atawasaidia. Aidha, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo, Dk. Makame Ali Ussi pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Maryam Abdalla Juma Mabodi pamoja na manaibu wake wawili wa Wizara ya Kilimo, Afisa Mdhamini WKMMU, pamoja na Wakurugenzi wa Idara, Taasisi na Asasi zote za Wizara hii; watumishi wote wa wizara pasi na kuwasahau wadau wote wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa shabaha za wizara kwa mwaka 2017/2018 kwa mafanikio makubwa. Ni matarajio yangu vile vile kuwashukuru sana Wizara ya Fedha kwa kuweza kutupa bajeti hii kwa mashirikiano makubwa na Idara ya Mipango. Aidha, ni matarajio yetu Wizara ya Kilimo kwamba, tutaendelea kushirikiana tena katika utekelezaji wa majukumu ya wizara na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa napenda kuishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa mara nyengine kwa kuanzisha mfumo mpya wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa kazi kwa vipindi vya robo mwaka badala ya utoaji wa fedha kwa kila mwezi. Hatua hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa sana utekelezaji wa malengo ya wizara kwa wakati na ufanisi mkubwa ambao umepatikana. Hongera sana Mhe. Waziri wa Fedha. Vile vile napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, Vikosi vya SMZ, wapiga kura wangu wa Jimbo la Amani na wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi kwa mashirikiano yao makubwa ambayo wanaendelea kutupa.

Mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii iliyo ndefu sana ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nawaomba Wajumbe wako wote wa Baraza hili la Wawakilishi na kuwashukuru kwa kunisikiliza na sasa naomba kutoa hoja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa tumwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. *(Makofi)*

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Moani ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambae ametujaalia kufika hapa kwa mara nyengine tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba tena Mwenyezi Mungu akuzidishie wewe Mhe. Naibu Spika busara, hekma na uadilifu katika kutuongoza na sisi, pia atujaalie tuendelee kuwa na nguvu na ari ya kuitekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, pamoja na malengo tuliyojipangia ili tuweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ujasiri wake wa kutekeleza vyema jukumu zima la uongozi wa nchi hii sambamba na jitihada anazochukua za kuendeleza sekta ya kilimo na sekta nyengine hapa nchini. Aidha, tunatoa shukurani za dhati kwa Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa busara zake na ushauri anaompatia Mhe. Rais katika utekelezaji wa mambo mbali mbali kwa ustawi wa nchi na wananchi wetu. Kadhalika, tunamshukuru Mhe. Balozi kwa kusimamia vyema shughuli za Baraza hili akiwa ni kiongozi wa shughuli za serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mkosefu wa shukrani endapo nitashindwa kuthamini juhudi zinazochukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hususan kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato kwa kukusanya zaidi ya asilimia 165 ukilinganisha na mwaka uliopita.

Hili limechangiwa zaidi na usimamizi mzuri wa kuhakikisha uvujaji wa mapato unadhibitiwa hususan mapato ya uchimbaji mchanga. Kamati inaisisitiza wizara isije ikalewa sifa wanazopewa na badala yake kuongeza juhudi na maarifa ya kuibua mbinu mbadala zitakazohakikisha zinawafikisha katika malengo yaliyopangwa kwa mwaka huu wa fedha wa 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kwa huzuni kubwa napenda kuwapa pole wananchi wetu wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kutokana na maafa ya mvua za msimu huu wa masika zilizoathiri mali, makaazi ya wananchi wetu pamoja na kusababisha baadhi ya watu kupoteza maisha. Kwa niaba ya Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo nasi hatuna budi kuwaomba wananchi hao wawe na moyo wa subira na uvumilivu hasa katika kipindi hiki kigumu. Aidha, naiomba serikali na Taasisi binafsi kuendelea kuchukua juhudi za kuwajali na kuwathamini wananchi hao kwa kuwapatia misaada ya hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, Kwa heshima na taadhima, kwa kutambuwa mchango na ushauri mkubwa katika kutekeleza kazi za kamati hii, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti;
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamu Mwenyekiti;
3. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe;
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe;
5. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe;
6. Mhe.Ussi Yahya Haji - Mjumbe; na
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe.

Aidha, Kamati yetu pia inafanyakazi kwa kusaidiana na Makatibu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu. Kwa heshima naomba niwatambue Makatibu hao ni:

1. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu
2. Ndugu Said Khamis Ramadhan - Katibu

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu ilipitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Fungu L01 la Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tarehe 04/05/2018 baada ya kuelekeza kufanyiwa marekebisho kutokana na kuwepo utofauti katika jumla ya Makadirio ya Matumizi ya shilingi 2.54 bilioni ambapo jumla ya shilingi 65.16 bilioni yaliainishwa katika Makadirio ya Matumizi ya Kitabu cha Mswaada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya mwaka 2018/2019 ambacho Kamati ilikabidhiwa na Afisi katika ngazi ya Kamati na jumla ya shilingi 62.62 bilioni iliyoainishwa ndani ya kitabu cha Hotuba ya Waziri. Tofauti hiyo imesababishwa zaidi na fedha hizo kuhamishiwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya ulipaji wa maslahi ya wafanyakazi waliogatuliwa kutoka Wizara hii ya Kilimo.

Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba niwasilishe mbele ya Baraza Lako Tukufu maoni ya Kamati yetu kuhusiana na Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, **k**iujumla, bajeti ya makusanyo ya mwaka huu ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeongezeka maradufu ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Kwa mwaka 2017/2018, wizara hii ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 4.93 bilioni ukilinganisha na makadirio ya mapato ya shilingi 12.50 bilioni ya mwaka ujao 2018/2019 sawa na ongezeko la shilingi **7.57** bilioni ya makadirio ya mapato.

Hii inaonesha wazi kwamba kiwango cha makadirio ya makusanyo waliyopangiwa Wizara hii ni kikubwa sana kwani ni zaidi ya mara mbili ya kile kiwango walichopangiwa mwaka jana ukiachia mbali kuvuka lengo la mkusanyo kwa kukusanya shilingi **7.7** bilioni. Kamati inaishauri Serikali iangalie vizuri makadirio ya makusanyo waliyoipangia Wizara hii kwani inaonekana wazi sio rahisi kufikia lengo hilo kwa asilimia mia moja hasa ukizingatia hakuna vyanzo vipya vya mapato ilivyoongezeka.

Mhe. Naibu Spika, la kushangaza, pamoja na kuongezewa kiwango cha mapato yanayohitajika kukusanywa na wizara hii lakini wamepunguziwa matumizi. Mwaka huu Wizara hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 62.62 bilioni ukilinganisha na shilingi 70.61 bilioni za mwaka jana. Hii ni sawa na punguzo la shilingi bilioni 8. Kwa vile Wizara ya Kilimo ndio uti wa mgongo unaotegemewa na wananchi wetu katika sekta husika za kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, punguzo hilo litakuwa na athari kwa kipato cha wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, **s**ambamba na hilo, Kamati yetu ilipata mashaka kidogo ilipokuwa ikipitia kwa undani makadirio ya mapato ya Mauzaji ya Mazao na Miche kinachokusanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - Kizimbani. Chanzo hiki kilipangiwa shilingi 20,000,000 milioni kwa mwaka jana ambapo mwaka huu kimepangiwa kukusanya shilingi 70,000,000 milioni sawa na ongezeko la shilingi 50,000,000 milioni**,** baada ya kukitathmini chanzo hiki cha mapato, Kamati iliona Wizara imepangiwa fedha nyingi kuliko uhalisia wake. Kamati inaishauri serikali kuyaangalia upya makadirio ya makusanyo ya chanzo hicho cha mapato kwa kupanga kiwango kinacholingana na uhalisia wa upatikanaji wa mapato kupitia chanzo hicho.

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imegundua kwamba kuna wakulima wengi wameathiriwa na mvua za masika zilizokuwa zikiendelea kwa kuharibu maeneo wanayatumia kwa kilimo pamoja na mazao yao kutokana na kujaa kwa maji. Aidha, kuna miundombinu mingi ya barabara ambayo nayo imeharibika inayowasaidia wakulima wetu kusafirishia mazao yao kutoka maeneo wanayolima. Kamati yetu inaishauri Wizara hii ya Kilimo kukaa na Taasisi zinazoshughulikia Maafa na utengenezaji wa miundombinu ya barabara ili kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuwapatia wakulima wetu fedha kidogo kufidia athari waliyoipata ili wakulima wetu waweze kupata faraja kutokana na hasara inayowakabili.

Mhe. Naibu Spika, suala la uimarishaji wa kilimo cha umwagiliaji maji katika nchi yetu ni jambo la msingi ambapo Wizara ya Kilimo imekuwa ikilifanyia kazi kwa juhudi kubwa hususan katika kuimarisha kilimo shadidi. Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuongeza uzalishaji wa mpunga kutoka tani 2.5 kwa mwaka jana hadi tani 6.8 mwaka 2017/2018 kwa hekta kwa kutumia kilimo cha teknolojia ya Shadidi. Kamati inaishauri Wizara hii kuendelea na juhudi hizo za kuwahamasisha wakulima wetu ili waweze kuhamasika na kulima zaidi kilimo hicho cha kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wizara hii ya Kilimo ya kununua matrekta mapya 20 na kupokea matrekta mengine 10 kutoka nchi ya Libya, bado wakulima wetu

wanakabiliwa na changamoto ya kutolimiwa eka zao za mpunga kwa wakati na hatimae huambulia kupata mavuno machache. (*Makofi*)

Kamati imeelezwa na wataalamu wa Kilimo kwamba, ili sekta ya kilimo ipige hatua kwa kuwa na matrekta ya kutosha basi kunahitajita yapatikane matrekta 80 ambapo serikali yetu tayari imeshaingia Mkataba na Kampuni ya kutengeneza Matrekta (Mahindra) iliyopo nchini India wa kuipatia nchi yetu Matrekta 100. Hivyo, tunaiomba serikali yetu sikivu kuharakisha upatikanaji wa nyenzo hizo ili wakulima wetu waepukana na kilimo cha jembe kongoroka mpini. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati yetu ilipokuwa ikipitia Makadirio ya Matumizi ya Programu hii ya Maendeleo ya Kilimo iligundua kwamba Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo haikupangiwa pesa, Kwa kuthamini na kutambua umuhimu wa Wakala huo hususan katika kuwasaidia wakulima wetu kulimiwa na kuburugiwa mashamba na eka zao za kilimo cha mpunga, kamati iliishauri wizara hiyo kuipangia pesa za kutosha Wakala huo ili uweze kuleta faraja kwa wananchi wetu. Hatimae Wakala huo ulipangiwa jumla ya shilingi 1.38 bilioni ambazo japo kwamba hazitoshi lakini angalau wataweza kuendelea kutekeleza majukumu yao waliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, katika Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo kuna Programu Ndogo ya Umwagiliaji Maji ambayo imepangiwa kutumia fedha kidogo shilingi 10.11 bilioni kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukilinganisha na shilingi 27.15 bilioni za mwaka 2017/2018. Kamati ilielezwa kwamba fedha hizo zitatumika katika ujenzi wa miundombinu ya maji. Hata hivyo, Kamati yetu ilitaka kujua miundombinu hiyo itajengwa wapi na kwanini kifungu hicho kimepungua kwa takriban shilingi 17.04 bilioni. Punguzo hili ni kubwa pamoja na kwamba fedha nyengine zitafidiwa kupitia mradi wa Maendeleo unaofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo ambapo utegemezi wa fedha hizo hauna uhakika zaidi. Kwa kuelewa umuhimu uliowekwa na Serikali yetu ya kuhimiza kilimo cha kibiashara cha umwagiliaji maji, ni busara kifungu hicho kikaongezewa bajeti ili kiedane na utekelezaji wa azma hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu pia ilihoji kifungu kinachotoa Huduma za Utibabu wa Mimea na Karantini na Ukaguzi wa Mazao (HL01010303) kwamba kimepangiwa fedha nyingi mno shilingi 113.11 milioni kwa mwaka huu 2018/2019 ukilinganisha na shilingi 3.06 milioni za mwaka jana 20017/2018 sawa na tofauti ya shilingi 110.04 milioni. Fedha hizo zinaonekana kuwa nyingi pamoja na kwamba matibabu hayo yanafanyika nchi nzima.

Mhe. Naibu Spika, wakulima wetu ni masikini sana ambao wanahitaji msukumo wa hali ya juu kutoka Serikalini ili kuimarisha kilimo kwa lengo la kujipatia kipato bora kitakachowasaidia wao wenyewe, familia zao na Taifa letu. Katika kuhakikisha hilo linafanyika, kamati yetu inaendelea kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa utekelezaji mzuri wa shabaha ya ununuzi wa tani 900 za mbolea ya kupandia mpunga na tani 900 kwa ajili ya kukuzia mpunga, tani 170 za mbegu na lita 17,400 za dawa ya kuulia magugu ambazo zimesambazwa Unguja na Pemba.

Pamoja na juhudi hizo, bado kuna changamoto kubwa inayowakabili wakulima wetu ya kukosa baadhi ya pembejeo hizo. Kamati yetu ilithibitisha hilo ilipotembelea bonde la Pangeni na kukuta msongomano wa wakulima wakifuatilia ugawaji wa dawa za kuulia magugu. Kamati yetu

haikuridhishwa na utaratibu uliokuwa ukitumika kwani dawa hizo zilikuwa zikitolewa kwa wakulima wa Pangeni na kuwaacha wakulima wa Kilombero na Upenja wakilalamika. Aidha, hao wakulima waliopatiwa dawa hizo walipatiwa nusu ya mahitaji yao. (*Makofi*)

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Mhe. Naibu Spika, Programu Kuu hii inayo Programu Ndogo ya Wakala wa Tafiti za Mifugo inayohusiana kufanya Tafiti za Mifugo (kifungu kidogo SL010303). Mwaka 2017/2018 kifungu hicho kinaonekana hakijapangiwa fedha lakini mwaka 2018/2019 kimepangiwa shilingi 829 milioni. Kamati ilitaka ufafanuzi na kuelezwa kwamba masuala ya tafiti za mifugo zimeundiwa Idara yake na fedha za kutekeleza shughuli hiyo zitapatikana katika Idara husika. Kamati inashauri Idara hiyo ipangiwe fedha za kutosha kwani bila ya kufanyika tafiti za mifugo, Wizara haitoweza kupiga hatua mbele kwa vile mifugo yetu inasumbuliwa na maradhi ya aina tofauti.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu imeshangazwa na kusikitishwa sana na vitendo vya baadhi ya watendaji wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushindwa kutekeleza baadhi ya maagizo na maelekezo ya Kamati na Viongozi wao, hili limetokea baada ya Waziri wa Kilimo aliyepita Mhe. Hamad Rashid Mohammed kuridhia na kukubali kuipeleka Kamati Bagamoyo kwenda kuliangalia Shamba la serikali lililobadilishwa matumizi yake kutoka shamba la Mifugo na kuwa Maeneo yaliyopimwa, kuchorwa na kugaiwa kwa kazi za Maendeleo. Ni matumaini ya Kamati kwamba kama ingepata fursa ya kwenda kuliona shamba hilo, baadhi ya changamoto zingeweza kutatuka kutokana na maelekezo na ushauri ambao kamati ingeutoa.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaendelea kuitaka wizara kwamba bado haja ya Kamati kulitembelea shamba hilo ni ya msingi ili kuweza kujua rasilimali za serikali zinatumikaje, zinahifadhiwa vipi na kuendelezwa katika mazingira ya aina gani. Kwa vile Kamati yetu inafikia ukingoni, tunaishauri Kamati ijayo ya Fedha, Biashara na Kilimo iitake Wizara ikamilishe ahadi hiyo ili Kamati hiyo iweze kupata fursa ya kulitembelea eneo hilo na kuishauri serikali yetu ipasavyo kwa kile watakachokiona na sio kukaa na kusubiri maelezo ya watendaji wa wizara pekee. Tunaitanabahisha wizara kwamba fedha nyingi za wakulima na Wakwezi wa nchi hii zimetumika na zinaendelea kutumika katika uimarishaji wa shamba hilo. (*Makofi*)

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, Katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa na wavuvi wenye ujuzi wa kuweza kuvua uvuvi wa Bahari Kuu, wizara imefanikiwa kuwaingiza katika meli za kigeni vijana 26 ili kupata uzoefu wa namna ya uvuvi huo unavyofanyika. Aidha, wavuvi vijana 25 wamepelekwa Chuo cha Uvuvi Mbegani - Bagamoyo kujifunza mbinu za uvuvi wa kisasa. Huu ni mwanzo mzuri ambao Wizara yetu ya Kilimo inahitaji kupongezwa ili rasilimali tulizonazo Zanzibar ziweze kuvunwa na kutumiwa kwa kuwanufaisha Wazanzibari wenyewe na sio kuwaachia watu wengine kunyonya utajiri wetu. Kamati inaitaka wizara kuwatumia ipasavyo vijana hao kwa maslahi ya Taifa letu na sio kuwawacha wakazagaa mitaani baada ya kupata ujuzi wao.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaipongeza Wizara ya Kilimo kupitia Kampuni ya Uvuvi kwa kuanza vyema utekelezaji wa majukumu yake kwani tayari Bodi imeshaundwa na kuingiziwa

shilingi 2.2 bilioni kati ya jumla ya shilingi 7.0 bilioni za mtaji kutoka kwa Washirika wake yaani *ZSSF*, *ZSTC*, Shirika la Bima la Zanzibar na Shirika la Bandari kulingana na mgao waliokubaliana. Fedha hizo zimeelekezwa katika ununuzi wa Meli mbili za uvuvi zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua wavuvi sita na kubeba tani 43 za samaki. Wizara tayari imeanza taratibu za zabuni na tayari zimeshatolewa. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuwa makini katika ununuzi huo kwa kununua meli zitakazokuwa mpya zenye thamani halisi ya fedha zinazohitajika.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalishia vifaranga vya samaki kiliopo hapo Maruhubi. Kuwepo kwa kituo hicho kutaleta faraja kubwa kwa wafugaji wetu wa samaki kuweza kupata vifaranga vya uhakika kwa lengo la kuwafuga kibiashara. Mradi huu ni mkubwa uliogharimu dola za kimarekani 943.94 milioni na unauwezo wa kuzalisha vifaranga milioni 10 vya samaki, majongoo 70 elfu na kaa 50 elfu. Kamati inashauri kwamba kwa vile huu ni mradi unaohitaji kuendelezwa hata baada ya kuondoka wawezeshaji, ni vyema Serikali ikahakikisha inakuwa na watendaji pamoja na wataalamu wa kutosha watakaomudu kuvaa viatu vyao ili mradi uweze kuishi na kutupatia faida kwa kipindi kirefu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa kazi za Kamati kwa mujibu wa kanuni zetu, Kamati ilitembelea kikundi cha wafuga pweza kiliopo Mtende Mkoa wa Kusini Unguja na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wananchi hao kwa kuwachangia shilingi 1,500,000/- ili waweze kutatua changamoto zinazowakabili. Kamati iligundua kwamba changamoto kubwa iliyopo katika kikundi hicho ni kukosa shughuli ya kufanya baada ya kumaliza uvunaji wa pweza wanaowafuga. Kamati yetu imekichangia kikundi hicho na kuwashauri waanzishe utaratibu utakaowawezesha kupata shughuli ya kufanya baada ya kufunga uvunaji wa pweza ikiwemo kulima kilimo cha migomba na mazao mengine. (*Makofi*)

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na wizara kwa upande wa Unguja za kuanzisha na kuuendeleza utaratibu mpya na mzuri wa kulipia malipo ya Mchanga Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*). Kupitia utaratibu huo, kamati inawataka viongozi na watendaji wa wizara hii kuanzisha utaratibu huo katika Kisiwa cha Pemba. Kadhalika, Kamati imeitaka Wizara kuutumia utaratibu huu katika Rasilimali nyengine za mawe, kifusi na kokoto ili mianya ya uvujaji wa mapato ipungue kama si kuondoka kabisa na serikali kujiongezea mapato kwani inaonekana mapato mengi yanapotea katika eneo hilo. Aidha, kamati yetu inaiomba Serikali iwe inazifuatilia Bei elekezi za mchanga inazozitoa ili ziweze kufuatwa kikamilifu na wauzaji pamoja na wanunuzi wa mchanga huo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imeshuhudia ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya kuni linalotokana na ukataji mkubwa wa miti. Pamoja na juhudu za wizara za kutoa mafunzo ya kuhimiza matumizi ya nishati mbadala pamoja na kufanya doria 104 zilizopelekea kukamata matukio 92 ya ukataji miti, matukio 13 ya ukamataji misumeno ya moto, kuwasilisha kesi mbili Mahakamani pamoja na kukamata misumeno ya moto 233 Unguja na Pemba lakini bado miti inakatwa sana kwa kutumia misumeno ya moto. Takwimu zinaonesha matumizi ya nishati ya

kuni kwa mwaka huu yamefikia mita za ujazo 23,114 ukilinganisha na mita za ujazo wa 19,532.25 za mwaka jana. Kwa kweli takwimu hizo zinatishia kupotea kwa uoto wetu wa asili. Sambamba na hilo, Kamati katika kutekeleza majukumu ya kikanuni, ilitembelea msitu wa mikoko uliopo Ukongoroni na kushuhudia magogo ya mikoko iliyokatwa na kuona eneo hilo limebakia kuwa tupu kama uwanja. Hali hiyo inasababisha maji ya bahari kupata mwanya wa kuvamia katika maeneo ya ardhi yanayotumiwa kwa kilimo na makaazi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, la kushangaza, baadhi ya viongozi wa serikali akiwemo Sheha wa Shehia ya Ukongoroni alikuwa mbele kutetea wananchi wake kwamba hawana kazi ya kufanya isipokuwa kujihusisha na ukataji wa mikoko kwa ajili ya utengenezaji wa kuni na tanu za mkaa. Viongozi wa namna hii ndio wanaoisababishia serikali yetu kuonekana haichukui juhudi yoyote katika harakati za kupambana na uharibifu wa mazingira. Kamati yetu inaishauri wizara inayoshughulikia Tawala za Mikoa kumchukulia hatua stahiki Sheha wa Shehia hiyo ya Ukongoroni. (*Makofi*)

Aidha, kamati inaitaka Wizara ya Kilimo kuchukua hatua za kudhibiti matumizi ya misumeno ya moto kama ilivyofanya Kisiwani Pemba. Kadhalika, Wizara isimamie ipasavyo Sheria ya Uhifadhi wa Maliasili za Misitu namba 10 ya mwaka 1996 pamoja na Kanuni zake ikiwemo kupiga marufuku usafirishaji wa kuni kutoka shamba kuja mjini. Hatua hizo kama zitatekelezwa kikamilifu, basi uteketezaji wa mikoko Zanzibar utabakia kuwa historia.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

Mhe. Naibu Spika, katika programu hii, kuna kifugu kinachotoa Huduma ya Ununuzi wa Vifaa vya Ofisi (HL01050101) ambacho mwaka jana kilipangiwa pesa nyingi shilingi 269.63 milioni ambazo hazikukidhi kikamilifu mahitaji ya upatikanaji wa vifaa vya kutosha katika Wizara hii, lakusikitisha mwaka huu ndio kimezidi kupunguziwa bajeti. Wakati Kamati yetu ilipokuwa ikipitia kifungu hiki kilikuwa kimepangiwa shilingi 10.31 milioni sawa na upungufu wa shilingi 259.32 milioni. Tunaishukuru Wizara kwa kukiangalia upya kifungu hicho na hatimae kukiongezea fedha hadi kufikia shilingi 50.32 milioni kama inavyoonekana katika kitabu tulichokabidhiwa. Pamoja na marekebisho hayo, Kamati yetu bado inaieleza Wizara kwamba kifungu hicho kinahitaji kuongezewa tena bajeti vyenginevyo Wizara inaweza ikakosa hata fedha za kununulia vifaa vya kutosha vya kuandikia na kuishia kukopa jambo ambalo litaleta picha mbaya kwa Wizara hii na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaipongeza tena Wizara hii kwa kufufua matumaini mapya ya kuyaendeleza mashamba ya mpira ambayo yalikuwa yanatumika kiholela na kuikosesha Serikali mapato. Kwasasa Wizara ya Kilimo imepanga kuyaendeleza mashamba hayo kwa kupanda mazao mbadala yakiwemo pililimanga na vanila na kuondosha dhana iliyokuwepo kwamba mashamba hayo yamezeeka na mipira iliyopo inahitaji kukatwa. Matumizi hayo yatayaongezea thamani mashamba hayo na kuweza kutumika tena kwa manufaa ya Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Rashid Ali Juma; Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Makame Ali Ussi; Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao pamoja na mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia wakati wote wa kupitia na kujadili Bajeti ya Wizara hii. Kwa vile wao ni Viongozi wapya katika Wizara hii, Kamati inawaeleza kwamba "***wasiwe na sifa kama ya muhogo ambapo ukiwa mtamu sana watu watautafuna mpaka waumalize na ukiwa mchungu sana watu watashindwa kuutumia".***

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muiunge mkono bajeti hii ili tumuwezeshe Waziri kwenda kutekeleza na kufanikisha yale waliyojipangia katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019 na baadae nasi tupate fursa ya kuja kumuhoji kwa kile alichoingiziwa na matokeo halisi ya kile alichokitekeleza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo naunga mkono hoja. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamida Abdalla Issa, sasa Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Kwa hivyo, mchangiaji wetu wa mwanzo atakakuwa Mhe. Ali Suleiman Ali atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na ajitayarishe vile vile Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2018/2019 ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. WWaziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuhakikisha kwamba Zanzibar tunafaidika na chakula na *inshaallah* itafika siku hatutaagizia nje chakula cha mchele. Lakini pili, niwashukuru sana Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa hotuba yao nzuri ambapo imetueleza mengi ya mafanikio na matatizo huu ndio utaratibu ambao tunautaka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba hotuba hii ni muhimu na kama ilivyojieleza katika kitabu hichi nitatafuta nafasi mbili tatu nizieleze ili kujua nini cha kuongeza. Kwanza,

niipongeze Wizara ukurasa wa 10 mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2017/2018 kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, imesema hivi *paragraph* 21. "Mhe. Naibu Spika, mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilikadiriwa kukusanya Tanzania Shilingi Bilioni 4.93, lakini hadi kufikia April, 2018 Wizara imekusanya Bilioni 8.15."

Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya ni ongezeko la asilimia 165. Hapa lazima tuwapongeze wenzetu. Lakini kwa bahati nzuri hapo hapo ikaja katika ukurasa wa 42 wakasema kwamba pamoja na juhudi hiyo iliyofanya haijatosheleza wizara imeweka makadirio *paragraph* ya 63 makusanyo ya Bilioni 12.50. Mimi hii naunga mkono kwa asilimia 100 Mheshimiwa tena naona bado kidogo kwa sababu wizara yetu hii ina rasilimali nyingi za kutosha, wana bahari, maliasili ya miti, wana mambo mengine mchanga, mawe, kokoto, na mengineyo. Kwa hivyo, mimi nasema hichi kilichowekwa si kibaya lakini kwa upande wangu nawapongeza waingie katika mapato haya na waongeze zaidi ili kiwango chetu cha fedha kiongezeke. Kwa hivyo, hapa nasema kwamba kwa maoni yangu naipongeza wizara kwa kulifikiria hilo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, suala kubwa tunalozungumza hapa ni kilimo, kilimo ni uti wa mgongo wa nchi, kwa hivyo tuseme tu kwamba pamoja na juhudi za wakulima wetu wametuonesha njia katika maonesho yaliyopita kwamba Zanzibar tunaweza kuwa na kilimo cha kutosha na wananchi wake wakafaidika. Kwa hivyo, mimi niviombe vyombo vyote vinavyohusika na kilimo, vikosi vyetu, wananchi na wana ushirika wa vikundi mbali mbali wajitahidi katika kuhakikisha kwamba kilimo kinaongezeka siku hadi siku.

Lakini kilimo kuna aina tofauti ya kilimo chetu au vilimo vyetu, kuna kilimo cha mvua, kilimo cha umwagiliaji na kilimo cha mboga mboga, niseme tu kwamba kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana kuhakikisha kwamba tunaongeza pato katika wakulima wetu na mahitaji yanaongezeka zaidi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili liangaliwe pamoja na juhudi yako tumeiona, matrekta tumeyaona, lakini pia tumesema tu kwamba tuombe zaidi tuongeze matreketa kama kamati ilivyosema. Vile vile wizara imesema vyema kwamba tutaongeza matrekta ya kutosha ili wananchi wetu walime kutokana na wakati tunaokwenda nao.

Mhe. Naibu Spika, tumezungukwa na bahari kila siku suala hili hulizungumza sana, tuna rasilimali bahari kwa upande wetu wa Zanzibar ambapo tuna miaka 54 hatujaitumia ipasavyo. Nyuma kidogo tulikotoka tulikuwa na Kampuni ya Uvuvi sijui *ZAFICO* na wakati huo vilikuja vyombo sijui vya Ujerumani walitumia uwezo wao kwenda katika bahari angalau ya kati kwa vyombo vyao, sio bahari kuu hapa hapa lakini wanasogea mbali. Wakati huo ilikuwa samaki wa kutosha wanawapata Wazanzibari walikuwa wanafaidika na wafanyakazi walikuwa wengi wanafaidika, wachuuzi walikuwa wengi walaji tulikuwa tunapata nafuu ya kupatikana samaki hao.

Lakini bahati mbaya hatukuweza kuendeleza kwa kipindi kile liliondoka sasa hivi niipongeze wizara kwamba inarudisha tena *ZAFICO* na ina malengo kwamba lazima kwenda bahari kuu. Mimi hili napongeza nataka tu Mwenyezi Mungu akitujaalia tufanikiwe ili faida ipatikane, tuna wananchi wetu wengi vijijini ni wavuvi, tuna wafanyakazi wengi akina baba na akina mama ni

wachuuzi, kwa hivyo tuseme tu kwamba wakiongezeka samaki pato la nchi litaongezeka lakini na wananchi wetu watafaidika kwa njia moja au nyengine.

Leo Mhe. Naibu Spika, samaki ni mgumu kumnunua kwa mnyonge, samaki unakwenda wakati mwengine unamtizama huwezi kumnunua. Lakini la kushangaza narudia pale pale bahari imetuzunguka kwa hivyo twende mbio kwa wahisani wetu watu wamaendeleo ambao tunawategemea, twende nao sambamba ili pato letu la samaki liongezeke katika nchi yetu na kuongeza fedha za nchi yetu katika pato hilo.yo

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze tena wakulima wetu kwa kazi nzuri wanayofanya ukianza mazao mengine ya mihogo, viazi vitamu, unakwenda kwenye mpunga si haba *Alhamdulillah* tumeula tumeona. Lakini zao la mboga mboga tunawapongeza kwa dhati watu wetu hawa kwa juhudi kubwa walionesha katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kipindi cha nyuma karibu hapa sio zamani sana matikiti ulikuwa huyanunui hapa yanatoka Bara, leo Wazanzibari wanaweza kuyasafirisha nje na wanasafirisha, kwa hivyo tuamini kwamba kumbe tunaweza tukifuata taratibu za wataalamu wetu wa kilimo, matikiti yamekuwa mengi wananchi wamefaidika ajira imeongezeka. Kwa hivyo mimi niseme tu kwamba hili zao la mboga mboga tuliongeze kwa juhudi zetu zote.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwenye tungule wenzetu Bara wanaita nyanya, leo tungule zimeongezeka zipo nyingi za kutosha nafikiri zinakwenda Bara sasa hivi kama sikosei kuna baadhi ya wakati. Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba wakulima wetu tunawapa nyenzo na taaluma zaidi ili waongeze ufanisi katika shughuli zao hizo.

Lakini ukiacha hilo Mhe. Naibu Spika, narudia tena watu wetu wanaoishi katika maeneo ya vijijini pwani huko, kwa mfano vijiji vyetu vya Uroa, Kiwengwa, Michamvi, Bwejuu, Makunduchi na kwengineko wale wakulima wa juu tunaita, kilimo cha juu maana yake ni watu ambao wanalima pilipili hoho. Pilipili hoho Mheshimiwa zina fedha lakini ngumu kwa sababu siku ya kwenda kuvuna labda uvae *gloves* inaweza kukusaidia lakini vyenginevyo utakuwa hulali kucha mikono yako italala ndani ya maji kwa muwasho unaopata au joto.

Kwa hivyo, niiombe sana wizara itafute kilimo kitakachowasaidia wananchi wetu katika maeneo hayo. Kilimo cha asili kizuri sana na pilipili zina soko nje. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili aliangalie litatufaa. Lakini wale wakulima wetu wanaolima ndimu hasa maeneo ya Bwejuu na Dongwe bado ni rasilimali na nathubutu kusema kwamba ukenda marikiti ndimu unazozikuta asilimia 80 zinatoka Bwejuu.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akawatembelea wakulima wale akatafuta utaratibu mzuri. Zamani ilikuwa ndimu unaitafuta huoni hata ya dawa lakini leo ukienda marikiti *time* yote unazikuta za kutosha. Kwa hivyo, tuwape njia tuwatafutie utaratibu kama kuna soko la Bara kwanza tutosheke sisi halafu wasafirishe ndio wakati tunaokwenda nao.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo bado ni kilio kikubwa kwa wananchi wetu zao la mwani, kilimo hichi kiliogopwa sana. Wananchi wetu tukiangalia kwamba vianzio vingi vya

mapato hasa akina mama hawana uwezo kwenda kutafuta pweza kule mwambani, pweza zamani wakati sisi wadogo ukitoka hapa ukienda kama pahala padogo tu unapata pweza, ukivuka mto kidogo tu unapata pweza lakini leo huwapati, mwenye vioo anazamia ndio atakuta pweza huko nje ya bahari kuu. Kwa hivyo, vile vianzio vyao vimepotea lakini bahati nzuri ukaja mwani ambao umekosa bahati, sawa sawa na chumvi ubora wake wote haina thamani, lakini thamani inayo maana bila ya chumvi chakula hakina ladha.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri ili twende vizuri wananchi wetu wale tuwatafutie mbinu, naamini kwamba tutahangaika kweli kweli na wataalamu wetu mbali mbali basi zao la mwani linaweza kuwa na bei. Mimi sitegemei kila siku shilingi 300/=, 400/= hata nauli huipati. Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Waziri hili na wataalamu wake wafanye bidii kutafuta njia wapi litapatikana soko la kudumu ambalo litawainua kwa kiwango kikubwa wananchi wetu wa vijiji vyetu vya pwani.

Mhe. Naibu Spika, zamani pia narudia tena kulikuwa wananchi wetu walikuwa wana vianzio vya makumbi wanaita vyazu, sijui vyeo, hivyo vianzio vya kuotea makumbi watu wanasuka kamba. Leo Mheshimiwa hakuna vianzio vile kwa sababu tumezidiwa kuna utalii na mambo mengineyo, kwa hivyo vyano vyote vile vimeondoka havipo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wananchi wetu asilimia 80 au 90 akina mama wanategemea mwani, tufanye bidii mimi naamini tukitembea tutapata faida, tukikaa juu ya meza tu hapa hapa hupati faida. Watu wanasema tembea uone mambo, kwa hivyo nimwambie Mhe. Waziri watendaji wake tutafute njia hizo ambazo zitatunusuru kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kwangu nimuombe sana Mhe. Waziri wakati wetu tuliokuwa nao mabadiliko ya hali hewa watu wanasema tabia nchi, mimi sijui hali ya nchi najua hali ya hewa tu, mazingira yanapatikana kutokana na hali ya hewa iwe tabia nchi katika kamusi ya Kiswahili tutakuja kulitafuta baadae. Mhe. Naibu Spika, tukiri kwamba wakati wetu huu umebadilika kutokana na hali ya hewa tunayokwenda nayo, tutafute njia madhubuti nini tufanye na wananchi wetu wapate taaluma wakati gani unafaa kwa kilimo hichi na wakati gani haufai. Kwa sababu wananchi wengi wanaona baada ya siku chache wanapata hasara kuliko faida, lakini naamini kwamba kama wataalamu wetu watafuatilia utaratibu mzuri na wataelimishwa wakulima wetu watapata faida kuliko hasara.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele nimeikubali hotuba hii ya Mhe. Waziri na naiunga mkono kwa asilimia mia moja, nashukuru ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali, sasa hivi mchangiaji anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na ajitayarishe Mhe. Hidaya Ali Makame na atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kutupatia uzima wa afya kwa sote pamoja na ndugu zetu wote wa Tanzania pamoja na waislamu wote duniani. Mhe. Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii

ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Mhe. Rashid Ali Juma kwa mwaka 2018/2019. Hata yeye mwenyewe Mhe. Waziri anasema kama leo tumevaa koti sare kwa maana sisi ni ndugu.

Mhe. Naibu Spika, nimesimama kuchangia wizara hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa sababu kusema la ukweli mtu azungumze uwazi kabisa wizara hii sina uzoefu nayo hata kidogo. Maana yake mimi sijawahi kupitia fani ya uvuvi, kilimo, wala maliasili na mambo mengineyo, lakini nitaongea kwa sababu ya wananchi wangu nitajitahidi kidogo ili nitoe haya machache ambayo nimeandika kuwazungumzia wananchi wangu.

Mhe. Naibu Spika, jambo la mwanzo twende kwenye suala la kilimo cha mwani. Mhe. Naibu Spika, wananchi wangu kipindi cha nyuma waliniita nikazungumza nao wakaniambia kwamba kazi wanayoifanya kwenye kilimo cha mwani ni kubwa sana, wanahangaika asubuhi hadi jioni na wengine mpaka magharibi na kazi ile ni ya kuchezea maji, inawaathiri sana hasa ukanda wa Pwani Mchangani, Kandwi na sehemu nyenginezo katika Jimbo langu la Chaani.

Mhe. Naibu Spika, lakini wakanieleza zaidi ugumu wa ile kazi na hali halisi wanayokuja kuipata katika malipo pale wanapofanya ile shughuli ya kuvuna. Waliniambia wanapata kwa kilo moja ya mwani shilingi 500, wakati wao wanatengeneza zao lile kwa muda mrefu na kazi wanayoitumia ni kubwa, lakini faida yake siku ya kuvuna ni sawa sawa na ziro kwao wao. Sasa wengi wameamua kwamba waache uvuvi wa mwani kwa sababu hauna faida kwao. Lakini mimi sikuwashauri waache, nikawaambia waendelee tutaiomba serikali na naamini serikali kwa kupitia uongozi wa Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atawafikiria kama alivyowafikiria watu wa karafuu. Watu wanaovuna karafuu fedha walikuwa wanalipwa fedha ndogo mwanzo katika kipindi cha nyuma, lakini sasa hivi wanapewa pesa nyingi kwa mujibu wa kilo.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili la mwani wananchi wote kwa ujumla Zanzibar nzima wanaojishughulisha na zao la mwani uwafikirie sana ili kiwango chao kiwe kikubwa katika mauzo ya kilo moja, badala ya shilingi 500 angalau ipande kwenye shilingi 1,500 au shilingi 3,000 ikiwezekana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, naomba nichukue fursa hii kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti aweze kuendelea na shughuli yetu hii ya leo. Mhe. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, karibu kwenye kiti chako. Nilikuwa naendelea na suala la kilimo cha mwani, nikamshauri Mhe. Waziri kwamba aweze kuangalia kwa Zanzibar nzima kuweza kuwapandishia fedha kwa kilo moja ya mwani kuweza kupanda kutoka shilingi 500 hadi angalau shilingi 1,500 au 3,000 kwa kilo, ili na wao waweze kujisikia kwa kazi ngumu wanayoifanya waone matunda yake.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hivyo hivyo ningemuomba Mhe. Waziri apange siku maalum ya kuja kuongea na wananchi wangu kuhusiana na masuala haya ya mwani na masuala yote ya kilimo

katika Jimbo langu la Chaani, yeye mwenyewe atakuja kusema lini nafasi yake ili aweze kuzungumza nao.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia jimboni kwangu vile vile eneo la Kikobweni kwendea Kandwi pale Kwa Mkorea kuna miti ile miembe mingi kwa upande wa kulia na kushoto imepangana hivi na kuna njia katikati. Wananchi wangu Mhe. Waziri walikuwa wanaomba kwamba miti ile upande mmoja wachukue wizara na upande mmoja waachiwe wao ili waweze kujiendeleza katika kijiji cha Kikobweni. Wanapata tabu sana wanaona ile miti iko katika maeneo yao, lakini cha kushangaza ni kwamba mavuno yale yote wanachukua wizara yako. Sasa ningeomba na mimi mwenyewe kwa kupita Mhe. Mwakilishi wao kwamba miti ile angalau uigawe ili wananchi wangu wapate nusu na wizara yako iweze kupata nusu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningeishauri serikali kwamba wasimamie sana kwenye masuala ya mazao ambayo yanachumwa au yanalimwa ambayo hayajafikia kiwango cha kulimwa au kuchumwa. Tumeona sasa hivi vitu vingi kama embe, nazi na vitu vyengine watu wanachukua wanakwenda kuchuma ambapo bado wakati wake haujafika, na hata ukiangalia ile ladha ya lile tunda au lile zao inakuwa haipo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la uvuvi wa samaki. Hapa tumo ndani ya kisiwa Mhe. Mwenyekiti, lakini ajabu kubwa ni kwamba Zanzibar nyama, kuku na vitu vyengine ni rahisi kuliko samaki. Kilichotakiwa ndani ya Zanzibar hii ni kwamba samaki ndio awe rahisi, ukiangalia kilo ya nyama ni shilingi 9,000, kuku kilo moja unampata kwa shilingi 6,500. Lakini ukienda kununua kilo moja ya samaki Zanzibar shilingi 20,000 au 22,000. Sasa nchi kama hii au kisiwa kama hichi ambacho kina samaki wengi, walitakiwa wananchi wawe samaki ndio rahisi kuliko nyama, kuku na vitu vyenginevyo. Samaki ndio mwenye afya peke yake kuliko kuku na nyama, samaki ni kitu ambacho kizuri kabisa lakini watu wanyonge wanashindwa kula samaki wakati nchi yao ni kisiwa na kuna samaki wengi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia jambo kubwa ambalo linanisikitisha kwa kupitia wizara hii ni kwamba sasa hivi Zanzibar tunakula samaki wa peduu, tunakula kuku peduu na samaki peduu wakati hichi ni kisiwa hatujafikia hatua hiyo, sisi tuna samaki wa kutosha kuweza kula samaki *fresh* ambao wananchi wetu wanaweza kwenda kuvua, lakini kutokana na unyonge wao hawana maboti ya kufika bahari kuu, samaki wa uvuvi unakuwa ni mdogo leo tunakula samaki wa peduu. Inawezekana samaki wale wale tunaokula pengine wamevuliwa hapa hapa kwenye bahari ya Zanzibar na ya Tanzania kwa jumla halafu tunauziwa sisi.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri waangalie vipi wataweza kuwanunulia maboti hata kwa njia ya mkopo Zanzibar, ili wananchi waweze kwenda kuvua wenyewe bahari kuu, na badala yake kuwazuwia wavuvi wale ambao mnawapa leseni kwenye meli kubwa kuja kuvua samaki ndani ya nchi yetu, halafu kwenda kwao wakaja wao wao wakaanza kutuuzia samaki, hakuna faida kabisa kwa upande wa Zanzibar kwamba zile meli zinazovua katika bahari kuu kuweza kuwaachilia. Wanavua samaki wengi, mapato madogo na wanafaidika wao. Samaki nchi za nje wanauzwa hali sana, na hii watakuja kutumalizia samaki wetu. Kwa hivyo, ni vyema serikali ikajipanga kununua meli wakawapa wananchi wakaenda kuvua wazalendo, ili sisi

wenyewe tukafanya biashara ya kuuza hapa pamoja na kufanya *exportation* kwenda kuuza huko kwengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikia kwamba serikali imejipanga kununua meli mbili kubwa za uvuvi kwa ajili ya wananchi. Mimi niipongeze wizara na serikali kwa ujumla kwa jitihada zao wanazofanya kwenye masuala haya ya mapoti na masuala ya matrekta na mambo mengineyo tumeona. Lakini ningeomba hizi meli mkazigawa basi mkazipanga kwamba kila mkoa ziwepo kwanza, kwa sababu leo mkinunua mbili Zanzibar nzima kuna mikoa sita, kama sikosei mikoa sita au saba. Sasa angalau basi mngeanza na saba hata kwa njia ya mkopo basi kila mkoa mkapeleka eneo moja watu wakaanza kufanya kazi hii ya uvuvi kuliko kuanza na mbili, lakini inawezekana meli hizi ghali ndio maana mkaanza na mbili, wewe mwenyewe Mhe. Waziri utakuja kuzungumzia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo nataka kulizungumza na hili Mhe. Waziri ndio ambalo aje anijibu kisahihi kabisa wamefikia wapi na watafanya vipi, la sio hivyo nitazuwia kifungu cha suala hili kwenye wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kijana mmoja ndani ya Jimbo langu la Chaani ameiba mchanga gari zaidi ya 60 Chaani Ketwa. Huyu jamaa anaitwa Babla, cha kushangaza ni kwamba wakati ule wa mchanga ghali Zanzibar basi aliweza kwenda kuchukua mchanga ule akaiba gari zaidi ya 60, na vijana wako waliwahi kwenda kufika usiku wakati ule saa 6:00, wakaambiwa kwamba huyu mtu anaiba wakaenda kuvamia wakamkamata. Yule kijana akataka kumalizana nao kwa njia ya pesa wale vijana wako wakakataa, na hilo niwapongeze kabisa, maana yake aliwa-*offer* shilingi 600,000. Sasa hadi hivi leo mwenye lile shamba, kwa sababu Chaani Ketwa kuna mchanga mzuri kama uliokuwepo Donge, mpaka hivi leo yule mwenye shamba analalamika barua kwako wewe zimeshafika, isitoshe kuna shimo kubwa zikija mvua anaweza mtoto yeyote akadumbukia akafariki, na mchanga ule umekwenda kuuzwa katika sehemu ambayo kusema la kweli wala sitaki kuitaja maana yake itachafua hali ya hewa nzima.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje aniambie kwamba huyu mtu mmemchukulia hatua gani mpaka sasa hivi. Kwanza aweze kwenda kuurejesha ule mchanga akaliziba lile pengo la lile shimo alochukua. Lakini pia mkamshughulikie ipasavyo kwa mujibu wa sheria za nchi kuweza kuiba maliasili bila ya kuwa na kibali na bila ya kuwa na utaratibu wowote na kuweza kwenda kuuza mchanga ule ambao kwa thamani ya wakati ule gari 60 ni zaidi ya milioni 25,800,000. Yule bwana alilipwa na mtu fulani *engineer* fulani ili aweze ku-*supply* mchanga na akawa ana-*supply* mchanga na akawa anauza vile vile kwa watu wengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri suala hili ndio peke yake ambalo mimi tutakuwa hatutofahamiana na waziri pindipo nitakapokuwa sijapata majibu ya kutosha na sahihi. Ninachotaka ni kwamba huyu mtu achukuliwe hatua na hivi karibuni kakamatwa anaiba kifusi Chakatu Kandwi. Hiki kifusi kilichoanza kuchimbwa juzi cha kujenga barabara ya Chaani, yeye tayari keshaanza kuiba gari za kifusi kakamatwa juzi saa 6:00 na pia taarifa hii aje aniambie imefikia wapi Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeiomba serikali iweze ku-*control* kwa hali ya juu masuala ya ukataji wa minazi Zanzibar. Minazi inapungua kwa wingi, madafu sasa hivi yamezidi kuwa hali, dafu moja sasa hivi kuna sehemu unanunua shilingi 1,000 na kuna sehemu shilingi 1,500 ni mambo ya ajabu sana kwa mujibu wa minazi tuliyokuwanayo Zanzibar, basi dafu moja lilitakiwa liuzwe shilingi 250.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala vile vile la msitu wetu wa Chaani Masingini ambalo Mhe. Mtumwa atakuja kulizungumza yeye anafahamu zaidi, kwa sababu pia ni mwananchi wangu, japokuwa pia yeye ni mwakilishi, lakini ni mwananchi wangu wa Jimbo la Chaani namuachia yeye aje alizungumzie suala hilo, atalielezea vizuri ili na wengine waweze kupata nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwa kuwa wizara hii mimi sio mzoefu sana nai- *support* kwa asilimia 80 na hiyo asilimia 20 sitaki kumuonea, lakini aje anijibulile swali ambalo nimemuuliza la kuweza kuibiwa jimboni kwangu kifusi pamoja na mchanga ili niweze kumrudishia asilimia 20 yake.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi anazozifanya ni nzuri, Naibu Waziri wake na watendaji wote kwa jumla pamoja na serikali nzima kwa jitihada wanazochukua kuweza kununua matrekta na masuala ya meli za uvuvi. Kwa kweli mkiweza kuleta meli za uvuvi kwa wananchi basi mtaweza kuwasaidia sana, kwa sababu wao ni wanyonge hawawezi kumiliki mashine wala boti. Kwa hivyo, nyinyi serikali na kwa sababu serikali ni ya wananchi na wananchi ndio wanaoitegemea serikali, basi vitu hivi tungeomba sana mufanye kwa njia yoyote haraka iwezekanavyo, ili wananchi waweze kufaidika kuliko kuwafaidisha watu wengine ambao wanatoka nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi naunga mkono kwa asilimia 80 kama nilivyosema na asilimia 20 nitakuja kumdai Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame, atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.
Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya makadirio ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitoanza na pongezi ndani ya wizara hii leo, moja kwa moja nitaanza na michango yangu kutokana na maelezo ya Mhe. Waziri ndani ya hotuba yake hii, nikienda mno leo naweza kuzuwia fungu la mshahara wa Mhe. Waziri hata Mhe. Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza moja kwa moja nakwenda kwenye ukurasa wa 59 Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki maelezo haya humu Mhe. Waziri katusomea hapo asilimia mia, tumeyaona na tumefahamu baadhi ya ufafanuzi ambao umetolewa humu. Mhe. Mwenyekiti, kukosa na wazee wa zamani, mimi humu kila nikiangalia leo naona kiza, hususan suala la wavuvi wetu, kifupi suala zima linalohusu uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, muhogo bila ya samaki hauliki, hususan Ramadhani hii hata mwezi wa kula mchana, bila ya samaki hata tambi huwezi kula. Kwa hivyo, tuone kwamba kuna umuhimu

mkubwa sa samaki na tukiangalia kwenye mitandao yetu au kwenye vyombo vyetu vya habari ukifungua tu ile *TV* kama inataka kuanza taarifa ya habari au kama kulikata matangazo, basi kitu cha kwanza kinachokuja mtu na kidau na bahari. Kwa sababu nchi yetu imezungukwa na bahari, lakini pia asilimia kubwa sana ya wananchi wetu waliomo ndani ya nchi hii ni wavuvi na wakulima. Kwa hivyo, kwa vile wananchi wetu wengi sana ni wavuvi na wakulima kwa asilimia kubwa. Mwenzangu pale Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kaongea kwamba ndani ya nchi yetu hii suala la samaki lina kipaumbele zaidi na kila mwananchi afahamu kweli nchi yetu inahusika na suala la uvuvi na kilimo pia na mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi moja tu hapa palikuwa pana maoneshao ya siku ya chakula duniani, lakini ambayo yaliandaliwa na Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na hata humu kwenye hotuba yake Mhe. Waziri pia katuambia kwamba siku ile ilifanyika haya maonesho na kila mwenye nafasi aliyefika alikwenda akaona jinsi gani yalivyoandaliwa maonesho haya.

Pia Mhe. Mwenyekiti, ndani ya nchi yetu hii kuna matamasha mbali mbali ambayo yanakuwa yanafanyika. Mimi huwa napata mashaka sana kuona kwamba matamasha yale yanafanyika ndani ya nchi hii, nchi hii ikiwa ni ya wakulima, wakwezi na wakiwemo na wavuvi. Sioni vile vitu ambavyo vinahamasishwa kama ni utamaduni wetu Wazanzibari, hususan kuhusiana na masuala ya vyakula vya asili, zikiwemo mboga mboga, lakini hata hivi vitoweo ambavyo vinapatikana katika bahari zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia sana kuhusu suala la uvuvi na vitoweo. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ningemuomba sana Mhe. Waziri, haya maonesho endapo yatakuwa yanaendelea, basi tuone ni jinsi gani wanajiandaa kama wizara kuliweka hili suala la maonesho kwa vyakula vya asili vya Mzanzibari, vikawa vinaoneshwa ndani ya maonesho yale na likawepo banda maalum kwa ajili ya uvuvi tu na maeneo ya samaki na vitu vyote vinavyopatikana ndani ya bahari yetu hii.

Pia likawepo banda kwa ajili ya vyakula vya mboga mboga vya wakulima wetu wanavyovilima ndani ya nchi hii vinavyopatikana vyote. Jinsi gani tunaweza kuvitumia kwa mapishi, lakini hata kwa kula. Kwa sababu hii ndio mila yetu na ndio utamaduni wetu, tutakapokuwa tunautangaza ule utamaduni wetu basi hata wale chipukizi wanaokuja au wale ndugu zetu ambao wanazaliwa sasa hivi, hapo baadae hawatokuja kupata shida kuuliza hiki ni chakula gani na hiki ni chakula gani, huyu ni samaki gani na hiki ni nini. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunayaona haya mambo kwamba hili suala ni kama limewekwa nyuma kwa ufupi, kwa sababu humu ndani ya Baraza nasema kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe, hawamjui hata samaki puju yukoje, samaki changu yukoje, samaki kangu yukoje, yeye anajua samaki ni samaki na dagaa ni dagaa. Kwa hivyo, itafikia kipindi mwanafunzi pia yumo ndani ya chumba cha mtihani anataka kujibu mtihani wake wa *biology* na masuala ya sayansi, akawekewa picha ya samaki pale akaja akaandika huyu ni dagaa kwa sababu hawamjui wala hawajui nini kinachoendelea ndani ya kitabu kile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili suala lina umuhimu wake ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulipewa kamusi hili hapa, kamusi hili lina maelezo mengi kuhusu Kiswahili chetu na tamaduni zetu, humu pia kuna picha ambazo zimeorodheshwa na majina

yake. Kuna picha za samaki wengi humu, lakini kuna picha za vyakula mbali mbali vya asili, shelisheli likaandikwa shelisheli, fenesi likaandikwa fenesi. Lakini kuna samaki humu msusa kaandikwa mkizi, puju kaandikwa changu, jodari yaani ni tofauti. Kwa hivyo, kuna muonekano kwamba hili suala la kufuatilia juu ya masuala haya bado liko nyuma na halijapewa kipaumbele hususan kwa wavuvi wetu hawa. Kwa sababu tukisoma humu ndani ya kitabu pia tunaona kwamba maelezo yaliyokuwemo kuhusu wavuvi wetu na suala la uvuvi ni kidogo sana kuliko maelezo yanayohusiana na kilimo, suala ambalo ni zuri kwa upande wa kilimo, kwa sababu kilimo ndio kila kitu. Lakini tukishalima tukishapata muhogo na mchele ubwabwa tupate na samaki ili tuweze kutowelea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeiomba sana wizara Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuambie ni taratibu gani watazichukua kuweka haya masuala ya maonesho ya vyakula vyetu vya asili, lakini pia na haya masuala ya uvuvi na kilimo jinsi gani watu wajifunze, jinsi gani watu wafanye ili kuweza kuwahamasisha na hata wale watoto waliokuwepo huko mitaani ambao bado wanaendelea wako katika marika madogo.

Mhe. Mwenyekiti, huku kwenye maelezo yake Mhe. Waziri pia kaeleza kwamba kuna vifaa vitapatiwa vikundi 30 vya wakulima na usarifu huu wa zao la mwani. Kaeleza hapa kuna vikundi vitatu vya ufugaji wa samaki, pamoja na ununuzi wa vihori 20. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka Mhe. Waziri aje anieleze tu, hivi vihori 20 vitapewa hawa wakulima au hawa wajasiriamali ambao wanahusika na suala la uvuvi, kama ni suala la kwenda kuvulia hivi vihori au ndio kwa hawa wakulima wa mwani, ili wavitumie kwa suala lao la kuzalisha mwani na kuweza kufanya hizo huduma za kwenda kupanda mwani. Kwa sababu kama tunavyokijua kihori, kihori ni kijitumbwi kiduchu ambacho mvuvi mmoja tu anafaa kuingia mle. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama watapewa wale wakulima kwa ajili ya kwenda kuvuna mwani au kupanda mwani sidhani kama vihori 20 vinaweza vikatosheleza kwa vikundi hivyo 30, au tuseme wakulima 20 utakayempa kila mmoja sidhani kama inaweza kusaidia kwa sababu kihori ni kiduchu sana. Hata uwe mwani pengine akipata polo tatu au polo nne itabidi apakie moja moja apandishe juu kutokana na ukubwa na uwezo wa hichi kihori. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri na hapa aje atufafanulie kidogo ili tuweze kujua.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la kilimo. Mhe. Mwenyekiti, kilimo ndio uti wa mgongo na kama tunafahamu zaidi kuna kumbukumbu kubwa ukifungua redio pale kusikiliza wakati Mhe. Rais anataka kutoa hotuba yake, basi kuna wimbo pale huwa unaimbwa na wimbo huu nadhani ulipoanza kuimbwa tangu sisi wengine hata mayai yetu hayajakuwepo, yaani hatujazaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wana *Uda Jazz Band* waliimba “Kilimo cha kufa na kupona ndio ngao yetu”. Kwa hivyo, kama ndio ngao yetu basi tukiendeleze kilimo ili tuweze kunufaika, na kilimo hicho kiwe endelevu kwa sababu kilimo ndio uti wa mgongo. Sasa kama kilimo ndio uti wa mgongo tunawaona wakulima wetu jinsi wanavyohangaika au jinsi wanavyopambana kuhakikisha kwamba kilimo kinaendelea ndani ya nchi yetu. Lakini wakulima hawa inafika hatua wanavunjika moyo kutokana na mambo mbali mbali au changamoto mbali mbali zinazowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, wakulima wamejikita sasa hivi kwenye sekta tofauti za umwagiliaji, lakini pia hata za mboga mboga na kila kitu. Lakini tukiwaangalia hawa wakulima wa mazao haya ya *spice* ambao hasa wanapatikana katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi na kwengineko baadhi yao wanavunjika moyo kutokana na masoko. Kwa hiyo, tuiombe sana hapa Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda walione suala hili na wakati kila siku humu ndani tunalizungumza kila inapofika hatua.

Mhe. Mwenyekiti, zao la pilipili manga, zao la kungumanga, zao la vanilla, ni mazao ambayo ukiangalia kwa nje yaani kiufupi utaona ni suala la kawaida lakini ni mazao ambayo bei yake au ile kuipata yake lile zao mpaka uhakikise kwamba lile zao tayari limeshafikia hatua wakati gani wa kuuza, lina muda mkubwa na kuweza kulifanyia ile kazi. Kwa sababu uanze kuyachunga tangu maua, lifikie mpaka hatua ya kupea na kuiva kwa hatua ya matumizi ni hatua kubwa. Lakini tunaliona zao lile lile wenzetu nchi nyengine wananufaika kwa mazao yale kwa nini sisi ndani ya nchi yetu hii ambayo tunayalima mazao yale hatuwezi kufaidika nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri awaangalie wakulima hawa wa mazao ya pilipili manga, kungumanga, pia na vanila ambayo hatuilimi sana, lakini na sisi sasa tunashajihika kwa sababu tumeona kwamba vanila bei yake nayo iko juu zaidi na pia kiwango chake cha kulima, yaani zile *process* zake za kulima ni rahisi zaidi. Kwa sababu mvanila unaota juu ya mti wowote, ukiweka mchungwa baadae ukiweka mvanila chini unakwenda zake unaota vizuri na unazaa. Lakini hata ukitafuta mjenga ua ukipandishia mvanila unakuja zake vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini wakulima hawa wawe hawanufaiki na baadae waone kama hivi vilimo havina tija, havina manufaa kwao wakati ni vilimo ambavyo watu wanafaidika na nchi za wenzetu tunaona kwamba jinsi gani wanavyofaidika na hivi vilimo, na jinsi gani nchi zao zinaendelea vizuri zaidi, kuwa na maendeleo zaidi kwa wakulima lakini hata wale wanunuzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi suala hili kwa kweli huwa linaniuma sana na linanivunja moyo sana. Kwa sababu mimi nikiwa kama mkulima nimezalikana na wakulima na nafungua macho nawaona wazee wangu ni wakulima na mpaka hivi sasa wanaendelea na ukulima huo. Lakini sijaona ile tija wala yale mafanikio ambayo wanayapata. Pilipili manga hapa petu sasa hivi imefikia shilingi 30,000 kilo moja, lakini anashughulika mwananchi na shamba lake anakuja mkodishwaji anakodi shamba zima kwa shilingi 200,000 wakati yeye akishakuvuna anakwenda kuuza nusu polo anarudi hapa ana zaidi ya milioni. Hii ni hasara na hasara hii inawakuta wakulima hawajui jinsi gani wao wanaweza kupambana na wakaweza kufikia hatima au kuweza kufikia lile lengo la yale mazao yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili akalisimamia na wakafikiwa hawa wakulima wetu wakaweza kupewa elimu na kuweza kufahamishwa juu ya mazao haya, au juu ya ukulima huu ambao wanaendelea nao na wao wakaona faida ya kilimo chao. Kwa sababu wanaonufaika ni wengine sio wao, wao siku zote unawakuta wako katika hali duni na hali ya kiumaskini, hali ya kwamba wao kumbe wawe ni matajari kuliko hata wale wanaokuja kuchukua huku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme kwamba nimpongeze sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake kwa kuwa pamoja kwa sababu Mhe. Waziri ni mvuvi, lakini Mhe. Naibu Waziri ni mkulima, kwa hivyo wao wawili wakikaa pamoja wakishirikiana na watendaji wao nina hakika ndani ya nchi yetu hii baada ya miaka miwili mafanikio mazuri sana tutayaona. Kwa sababu wao ndio wanajua jinsi gani mkulima anatakiwa awe na jinsi gani mvuvi anatakiwa afanye kazi zake. Kwa hivyo, washirikiane wakae pamoja na watendaji waone jinsi gani wanaweza kuwafanikisha au kuwaenzi watu hawa na kuwaendeleza kiuchumi zaidi waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Wajumbe hii wa Kamati wamesema Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri wasiwe watamu kama muhogo, mimi nawaambia wawe watamu kama muhogo mtamu kwa sababu muhogo mtamu ukiula sana baadae unalewa, ukishakulewa basi unakuwa huna nguvu. Kwa hivyo na wao wawe wazuri wawe watamu kama muhogo mtamu kwa sababu watufahamishe watuelekeze yale mazuri mpaka tulewe hasa. Tujue kama kweli tuna Waziri na Naibu Waziri majembe ambao wanahusika na suala hili la kilimo na uvuvi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi niseme naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja 100 na hayo maelezo mengine niliyotaka ufafanuzi Mhe. Waziri aje anipe ufafanuzi mzuri bila ya hivyo baadae nitapiga buti hata kama nimeunga mkono. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Hidaya Ali Makame kwa mchango wako, Mwenyekiti wa Vijana kutoka Kaskazini Unguja. Sasa nilimtaja Mhe. Simai Mohammed Said lakini ataanza Mhe. Suleiman Sarahan Said na atafuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Mtumwa Suleiman Makame ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za kuendeleza kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, pia nimpe pongezi sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi katika jitihada zake za kusimamia sekta zote lakini ikiwemo hii kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na upandaji wa miche hasa mikarafuu. Mhe. Mwenyekiti, miche ya mikarafuu Mhe. Rais alijitahidi sana katika kuinadi ili iweze kupandwa mingi lakini mara hii katika ugawaji wa miche ilikuwa haikutosheleza kabisa. Kwa hivyo, wananchi walihamasika sana lakini miche haikutosha. Nimuombe waziri kwamba ajaribu kufanya mbinu nyengine ya ziada ya kuhamasisha zaidi maana yake wananchi wanahitaji mikarafuu sana.
Mhe. Mwenyekiti, namuomba waziri katika suala la ukodishwaji wa mashamba ya mikarafuu kule Pemba inatupa tabu sana kwa wananchi wetu na hili suala Mhe. Rais ameshalitolea ufafanuzi sana kuhusu masuala ya kumalizana na watu hawa, lakini hapajulikani ukweli uliopo lawama zinaongezeka siku hadi siku. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri hili suala la mikarafuu ya eka pamoja na wale waliokodishwa kupata mafao yao likajulikana nini hasa ukweli wenyewe, maana yake utasikia huku kwamba masuala haya yameshafanyiwa utaratibu lakini ukenda kwa wananchi bado malalamiko yapo.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri hili suala linatupa tabu sana kule Pemba. Kwa hivyo, hebu uje uliweke sawa ili wananchi tufahamu sisi wanaotwambia wananchi ni ya ukweli au si ya ukweli kwamba kuna watu wameshakodishwa mikarafuu lakini mikarafuu yao

waliyokuwa wanahangaika nayo pesa zao hawajalipwa mpaka leo, sasa sijui kama ni kweli au ndio mambo yenyewe. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri kama una uhakika uje kutupa majibu, kama huna hili suala ningekuomba ukaenda Pemba ukalifanyia utafiti ukaweza kulijua.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kuwapongeza Wizara ya Kilimo kwa kweli sasa hivi kilimo kimeongezeka hasa cha matunda katika visiwa vyetu hivi, matikiti, matango, tungule na mambo mengi sasa hivi uagiziaji ni mdogo sana hasa nikisemea katika eneo la Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tungule zimekuwa nyingi sana na vitu vingi vya mazao haya yanapatikana vizuri na kwa bei nafuu sana na unayapata mpaka kwa vi-*carry*, hili nilipongeze sana. Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni na haki yake mpeni.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokizungumzia zaidi ni kwamba kilimo hasa upande wa Pemba hakijafanyiwa utafiti wa kutosha na kama kimefanyiwa utafiti au kama tunakielewa basi sasa hivi tubadilikeni. Mhe. Mwenyekiti, kule Pemba tunalima kwenye mabonde, tunalima sehemu za juu. Mheshimiwa tunamvua za masika, lakini tulikuwa na mipunga mingi ya dizaini ya kizamani ikiitwa sijui kilangawa, ringa, ilikuwa inachukua zaidi ya miezi sita katika uvunaji wake, lakini sasa hivi kutokana na mvua tulizonazo tumeona kwamba kuna kilimo cha shadidi ambacho cha muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mabonde ndio tunayotegemea kwa kulima lakini mvua zinapokuja zinakokoa kila kitu. Ningeomba sasa hivi tukawa tunabadilisha kilimo tunaweza tukaweka kilimo cha shadidi, niliwahi kuona kule Makombeni mpunga ulivyonawiri vizuri, na tunaweza tukawa tunavuna mara tatu kwa mwaka, kuliko kuvuna mara mbili au mara moja kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana nimeona hapa una matrekta unaleta au yameshafika, lakini nikuombe kwamba ulimaji wa matrekta katika maeneo ya vuli la kule Pemba twende sana na msimu wa mvua kutokana na hali halisi, tuweze kuichukua kabla ya mvua hazijanyesha ili tuweze kupanda na kuvuna mvua inapokuja iwe tayari mabonde yale hayana kitu. Kwa hivyo, tuweze kucheza na mvua ambazo sasa hivi zina gharka na kuweza kupoteza kilimo. Ningekuomba sana ukakaa na wataalamu wako mkaichezesha hii misimu ya vuli na mvua ya masika tukaweza kupata kilimo na hasara ikawa ndogo kutokana na matatizo yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niende na hili shamba la *spice* ambalo lipo hapa Kizimbani. Mheshimiwa hili shamba la *spice* mimi sijui historia yake lakini nikikuuliza wewe unaweza kujua historia hili limejitengeneza wenyewe kwa rehema ya Mwenyezi Mungu limepandwa au likoje. Lakini ningeshauri kama ile ni mfano mzuri sana Mheshimiwa na Pemba nakumbuka Mhe. Aboud Jumbe nafikiri kama sikosei alileta kilimo cha hiliki na kikafanikiwa kwa upande fulani kulimwa limwa. Lakini sasa kule Pemba sijaona eneo lililotengwa au linalofanyiwa ukarabati wa kuwa kama la eneo la Kizimbani tukaweza kulitengeneza likawa eneo hili. Lisipotufaa sisi litawafaa wanaokuja. Kwa hivyo, kama kuna uwezekano au umeshafanya na utaalamu wako, basi Pemba kuna rutba nyingi sana ningeomba upande wa *spice* Mhe. Waziri ukajaribu kulitolea ufafanuzi kama tayari mipango yako imeshakuwa mizuri ukaweza kuliangalia hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye uvuvi wa samaki. Mheshimiwa sasa hivi tumeshajipanga nimeona tutachukua boti kubwa ambazo zitavua samaki wengi au wakubwa na ni kweli hii

rehema ya Mwenyezi Mungu. Mhe. Mwenyekiti, sisi tumepata bahati kubwa sana ya bahari kuu na ina samaki wazuri na wengi, lakini Mhe. Waziri sisi tuna samaki ambao tunawaelewa sana, tuna samaki wa jodari, kambisi na samaki wengine ambao wana sifa nyingi sana. Sasa sijui kwa wataalamu wako wakati tutakapovua hawa samaki, tutakula wenyewe hapa hapa au tayari umeshatafuta soko la nchi gani ambao wanapenda samaki kabla hatujaanza kufanya utaratibu lakini soko letu liko tayari. Kwa hivyo ningeomba kama itakuwa utaratibu huo basi.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala hili la uratibu wa Pemba. Mheshimiwa Pemba kunakuwa na matatizo mengi sana ya mambo ya maposho na mambo ya wafanyakazi na hili ni eneo linajitegemea sana ukiliona katika fungu unasikia la uratibu Pemba. Wewe katika wizara yako hudaiwi na hawa maposho, posho lakini inakuwaje maana yake wakati tumeshapata bajeti tunaiendeleza bado ukasikia malalamiko ya mwaka wa pili, mwaka wa tatu ya maposho ya watu hayajalipwa. Kwa hivyo na wewe nikuombe kwamba utakapokuja unaweza ukaniambia ee bwana mimi sidaiwi na naendelea vizuri sawa hakuna tatizo Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niendelee Mhe. Waziri wewe ni dhamana sana wa afya ya chakula kwa nchi yetu hasa hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, unajua matatizo mengi yanayotokezea katika maeneo ya wenzetu tusione ajabu tunaiga, watu humu mishikaki sasa hivi imekuwa mingi na maeneo mengi, nyama hatujui zinatoka wapi, tusije tukachinjiwa paka au mbwa baada ya kuwa mengi. Sasa hivi tumekuwa na utaalamu wa mafriza kila pahala wewe njoo uchukue. Sasa ningekushauri au ningekuwa nakuuliza hawa wenye mabucha ya samaki, mabucha ya nyama ya kuku, unachinjiwa kuku hujui wanatokea wapi, wanaletwa kwenye susu au kwenye beseni wanauzwa, kuku wale huwajui wamekufa, kuku wale huwajui wanaumwa wewe unauziwa kuku. Sasa hawa wasije wakatupelekesha pabaya katika maradhi ambayo kuku akifa zile *point* zake ambazo hujui binaadamu zitamuathiri vipi, haidhuru anapikwa, lakini kuna wadudu wengine hawafi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama mtu anataka kuuza kuku wake achinjiwe pale marikiti waonekane, awaweke na beseni lake pale, kule kuchinjwa huko majumbani wakiletwa pale kwa sababu hakuna bucha ya kuku, watu wanachinja huko wanaleta, wakileta hatujui kuku wale wanakuwaje. Sisi tunaambiwa halali lakini kuku wenyewe hatujui wamekufa au wamekuwaje. Sasa ni shauri hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ng'ombe wapo wa kuibiwa, wapo waliokufa tunaita waliokufa, sasa ng'ombe akifa mtu anamchinja huko huko analeta mapande ya nyama. Ningeshauri sana tukasema hao wenye mabucha wakawa wanajulikana wananunua nyama vipi na wapi, na wewe Mhe. Waziri ukafanya ziara za kushtukiza kwenye yale mabucha au wale wataalamu wako wakaulizia nyama umenunua wapi, ulinunua lini, ikawa angalau kuna vitisho fulani, *otherwise* tutakula nyama hairidhishi au kwa usalama wetu inaweza ikatuletea matumizi mabaya.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine nyama ukiiweka kwenye friza bwana inakuwa na tabu zake tayari ile inakuwa imeshakomaa, usione inakuwa na mambo mengi ya kwamba ukiitoa kwenye ubaridi ni kuipika unakuja kuiona kwenye mambo ya kula ndio unaijua athari zake.

Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi sana nimeona mambo mengi ambayo ninayaona, lakini Mhe. Waziri sijaona eneo hata moja, si Unguja, si Pemba ambalo la kitalu maalum cha serikali au cha

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kinachoota mbegu kutoka nje au mbegu ya majaribio ukawa unaitwa kama mkulima kama nani ukaambiwa nenda ukaangalie kitalu hichi. Eneo la *space* la *centimetre* ngapi umetoa mpunga fulani, au umefanya kitu fulani tukaiga kutokana na mambo yale.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kipindi cha nyuma kama kule Pemba tulikuwa na ng'ombe wa maziwa Mtakata, walikuwepo na Chamanangwe, n'gombe anazaliwa pale lakini unaambiwa kwanza mama yake anatoa lita 20, mama yake anatoa lita 10,000. Kwa hivyo, wewe umlishe vizuri anatoa lita 10,000 imekuwa ni mifano mizuri, sasa hivi hatuna utaratibu ule unapewa ng'ombe hujui anatoa lita ngapi, anafanywa vipi, inakuwa kuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba na nyinyi mtuoneshe mfano Wizara ya Kilimo, zamani mpaka bwana shamba nae alikuwa na shamba lake, unakwenda kwa bwana shamba wako wa karibu na wewe unamuiga, lakini maprofesa wetu wote leo hawafanyi tena hiyo kazi. Sasa ningeomba basi kama maprofesa hawawezi nyinyi wizara muweze kuweka angalau na sisi tupitie kukagua kuangalia ile hali halisi ambayo ipo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kitabu chake humu amesema ana mpunga, anazalisha vipi, lakini hatwambii kwamba mita ngapi unaweza kuzalisha mpunga wa kiasi gani, ni kama vile watu unapokuta madaktari anakwambia mara hii tumezalisha watoto mia lakini waliokufa ni wawili tumepata mafanikio mazuri. Kwa hivyo ningeomba hilo liweze kuangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, tumepiga vita sana kuhusu suala la nyavu ndogo ambazo zinaharibu samaki wadogo wadogo ambao hawapati kukua, lakini sasa hivi hili suala limeachiwa ukienda kwenye minada samaki wadogo wadogo wamekithiri ina maana wale hawavuliwi kwa mshipi wanavuliwa kwa nyavu ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, wapo samaki maalum ambao wanajulikana hawa hawakui mmoja wapo akiwa ni dagaa na wengine wengine wapo kidogo, lakini unaweza kuwakuta vichangu au nguru wadogo kwenye mnada. Kwa hivyo, naomba hili suala la nyavu ndogo bado likawa linapigwa vita kutokana na samaki wadogo wadogo ambao wanakuwa na tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee niseme kwamba kuna udhibiti Marehemu Mhe. Mzee Abeid Amani Karume alizungumza sana kwamba tujenge padogo baadae tulime pakubwa, sasa hivi ardhi ya Zanzibar ni kujengwa mpaka ndani ya mabonde. Yale mabonde yako ya mpunga ambayo mwenyewe ulikuwa unaona raha ukipita na harufu nzuri ya mpunga sasa haipo, unakuta mtu katikati ya bonde katia nyumba anasubiri aje avuliwe na maji. Sasa Mheshimiwa lazima na serikali iwe kali katika kuzuia matatizo kama haya, tukisema tunaachia huru uhuru wakati mwingine unakuwa na matatizo yake. Kwa hivyo mimi ningekuomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni kisiwa cha nazi tatizo tulilonalo madafu yanauzwa ovyo ovyo. Sasa mimi nilikuwa nikuulize kwamba bado sheria ya madafu ipo, au tuangalie biashara kama dafu zuri kuliko nazi basi tuuzeni madafu tuache nazi, lakini kama nazi inahitajika sana basi ipigwe marufuku na mtu atakayechukuliwa hatua katika kuuza madafu kama sio madafu ya chakula, tunaharibu sana utamaduni wetu na pia itaondoka sana hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya mikarafuu kuna kipindi huwa inazaa sana na kuna kipindi inakuwa inapungua kutokana na msimu au matatizo yaliyopo. Lakini kulikuwa na matatizo ambayo yalizungumziwa kwamba mikarafuu haitakiwi kutiwa kipando chengine katika shamba, lakini sina uhakika wataalamu wako kama ni ukweli kuwa haitaki kupandwa na kitu chengine au kutokana na sababu za maradhi kama yatapata mti mwingine yanaweza yakaiathiri mikarafuu. Lakini mikarafuu mingi sasa hivi inalimiwa migomba, inalimiwa mihogo, inatiwa vitu vyengine. Sasa je, wizara yako kuhusu suala la uchumi huu wa uti wa mgongo, mikarafuu imeruhusiwa kulimiwa na vitu vyengine ndani yake au hakuna athari. Kama hakuna athari mimi sina tatizo na kama kuna athari basi hili suala la kuliangalia sana tusije tukaharibu maliasili yetu hii kwa matatizo madogo madogo ya muhogo wakati mashamba ya muhogo yapo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ni suala la bahari kuu ambayo tunayo lakini mara nyingi sana tunaibiwa samaki wetu na nchi nyengine hasa watu wenye meli kubwa. Mimi nikwambie tu kwamba ukiachia zao la karafuu, zao la bahari ni riziki ya Mwenyezi Mungu aliyotupa. Sasa pamoja na hizo boti zako ulizosema je, zina uwezo wa kwenda bahari kuu ili zikiwa kule nje zikawa ni moja ya walinzi wetu kwa sababu zinakuwa zinaangalia. Lakini pia ni uwezo wa kuchukua samaki wa aina ambayo wanahitaji ili kuja kuwaleta kwa manufaa yetu. Sasa ningeomba sana wakati unaamua kufuata suala hili ukijua kipimo chako cha bahari kwamba ina uwezo upi, maana yake nchi yetu sisi ukitoka pale Nungwi kwenye hoteli ukienda mita ishirini tu una bahari ya mita mia tatu kwenda chini. Kwa hivyo, tusije tukenda tukachukua boti ikawa boti ya mita kumi au kumi na tano. Ningekushauri sana katika ujenzi wa boti ndogo uwepo lakini katika ujenzi wa boti kubwa za kuilinda bahari yetu uwepo. Naomba sana suala kama hili likaweza kuangaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nalizungumzia ni maji ya mvua katika mito. Hatuna mito tena wala maziwa katika maeneo yetu, sisi tulikuwa tukikumbuka sana maeneo katika barabara yetu ama za Chamanangwe au barabara zetu unazokujia Mkoani ukianzia Kipapo, Mwanamashungi, Mwanatojo na maeneo mengine yalikuwa na mashimo makubwa sana msimu mpaka msimu yanachukua maji. Sasa *land* yote imekaa sawa na kuna uwezekano mkubwa sana wa kuweza maeneo yale kwenda na kijiko yakachimbwa yakaweza kutoa maji, maji yote yanakimbilia baharini, mvua ikinyesha leo siku ya tatu joto hakukaliki. Ningeomba kama kuna utaratibu kwa sababu ardhi inabakia kuwa wazi yachimbwe mashimo yale ili wakati wa mvua yaweze kutuliza maji ambayo yatasaidia kwa kila hali.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru kwa mchango wako Mhe. Suleiman Sarahan Said, sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said, atafuatiwa na Mhe. Mtumwa Suleiman Makame na Mhe. Makame Said Juma ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika wizara yetu hii muhimu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake aliyoisoma vizuri leo asubuhi ukifuatilia katika kila matamshi na neno

alilosoma hakuna hata sehemu moja alikohoa au alikosea kutamka neno akionesha umahiri wake. Lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati aliyesoma leo kwa niaba ndugu yangu Mhe. Hamida Abdalla Issa. Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Spika asubuhi ya leo kwa kuniunga mkono hoja yangu juu ya masuala ya pikipiki hizi na kunikubalia. Pia nichukue nafasi tena kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelezo mazuri na naamini ahadi yake aliyonipa leo itakuwa ndio sehemu moja kubwa sana ya kuwasaidia wananchi pamoja na vijana wetu na kuinusuru nchi hii katika kuingia janga hasa la kupoteza vijana waliokuwa chini ya umri kupata vilema vya maisha au kupoteza maisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nakuomba sasa kwa ruhusa yako niende kwenye mchango wangu moja kwa moja. Kwanza niseme moja kwa moja mimi siungi mkono hoja na nitazuia fungu kwa sababu ambazo nahitaji maelezo kutoka kwa waziri pengine atanipa maelezo ya kutosha lakini bado nitazuia fungu. Niseme kwamba Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni rafiki yangu lakini kwenye kazi ni kazi tu, kwa hivyo hapa sitogeuka mkono wa kulia nitakuwa nakuangalia wewe. Kwa sababu sitaki namuonea haya nitamzuilia fungu kwa upande mmoja, maana yake yeye nikimpiga ananikazia macho humu wakati mwengine. Kwa hivyo, nimwambie waziri mara hii kwenye suala hili hatukubaliani na wewe. Lakini najua mambo mengi wizara hii wamefanya mazuri na wizara hii ina umuhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika wizara ambayo ina watu wengi wana elimu basi ni wizara hii, hata humu ndani ukiangalia tuna madaktari wawili, tuna Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, wote ni wazoefu lakini pia wana uzoefu wa maeneo tofauti pia mbali ya kilimo. Sasa mimi nataka niseme vitu viwili, kwanza nataka niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri ambao ni MBM Mhe. Said Soud Said pamoja na Mhe. Juma Ali Khatib kwa kumsaidia Mhe. Rais hasa katika suala la zao la karafuu. Jana tulipata taarifa hapa tulizisikia kwamba zao la karafuu pia tumeweza kuzalisha tani 8,500,008 pesa ambazo zimenunuliwa ni bilioni 118 na ukiangalia takwimu kwa hizi ni nzuri sana. Kwa hivyo, mimi nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri, lakini pia kuwapongeza wote hasa Mhe. Rais mwenyewe kwa juhudi hizi. Nimuombe Mhe. Waziri naamini unanisikia kwamba yale mazuri ambayo yaliyofanyika katika suala la kuwasaidia wazee hasa wanaopatiwa pesa kila mwisho wa mwezi, basi rekodi hii katika suala la zao la karafuu wajaribu kuwaalika waandishi wa kimataifa kama *BBC, CNN*. Hii itasaidia kutangaza rekodi hizi ambazo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika zao la karafuu jinsi alivyoweza kuweka mageuzi ya haraka, kwanza katika kulilinda kwenye masuala ya miche, lakini pia kwa muda mdogo sana limeweza kuwaleta pia kuwa kimbilio na sehemu kubwa ya kuwasaidia wananchi wetu.

Halikadhalika nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja atueleze pia katika hizi fedha za bilioni 118 akishirikiana na Waziri wa Fedha na Mipango ambazo zimenunuliwa karafuu zinatusaidia vipi katika wananchi wetu ili wapate kusikia. Kwanza kwa upande wa Pemba mbona hatuzioni hizi fedha zikipitia katika mabenki yetu, hilo nataka tulielewe lakini tulifahamu kuna tatizo gani. Je, mashamba yamekodishwa kwa nini. Fedha ambazo serikali inanunua nyingi sana kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu juu ya karafuu hatuoni mageuzi, *speed* ambayo serikali inanunua hizi karafuu haziendi sambamba na mageuzi yale ukaona wananchi katika sekta ya ujenzi, lakini pia katika maisha yao ya kawaida. Kwa sababu fedha hizo ukiziangalia sasa hivi kwa muda wa zaidi

ya miaka kumi zinaweza zikakaribia pengine katika dola zaidi ya milioni 500. Sasa fedha hizo zote zimeingia katika maeneo ya Pemba katika ununuzi wa karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kumuomba Mhe. Waziri aje atueleze vizuri sana katika haya fedha ambazo zimetumika na serikali. Lakini halikadhalika alibebe na hilo pia la kuhakikisha kwamba sifa na juhudi ambazo zimechukuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ziweze kupaa katika anga za kimataifa na iwe ni mfano na tuone watu wanakuja hapa. Tumeona jinsi gani katika suala lile ambalo la kuwasaidia wazee limeweza kusifiwa vizuri na Aljazeera, *BBC* na maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili nataka nizungumze ambalo linauma sana, wananchi wangu ambao nawawakilisha hapa wanapigwa makwaju eneo la Ungujaukuu Kaebona ndio sababu moja kubwa sana inanitia huzuni na nikasema kwamba siungi mkono hoja na nitazuia fungu.

Mhe.Mwenyekiti, kwa mujibu wa katiba yetu ya nchi ukienda kwenye sura ya pili kifungu namba 8 kinasema hivi: "Itakuwa ni wajibu wa vyombo vyote vya serikali pamoja na vyombo vyengine vyenye uwezo pamoja na watu kutunga sheria kiutawala au uwezo wa kimahakama kufuata misingi ya uhuru, haki na amani".

Mhe. Mwenyekiti, kweli sisi kule kwa upande wa Mkoa wa Kusini Unguja eneo la Ungujaukuu Kaebona tunao msitu huu wa Jozani ambao umepakana na Huba ya Chwaka, na msitu huu umepakana na vijiji karibu tisa, kuna Kaebona, Chwaka, Charawe, Pete, Cheju na vyengine. Lakini Kamati ya Mazingira pamoja na Kamati ya Misitu walikubaliana kwenda kuokota hizi kuni kavu wapate japo mizigo miwili, mitatu, minne kwa wakati ambao unastahiki, lakini kuna dereva ambaye baadae Mhe. Waziri nitakupatia jina lake na pia kuna kiongozi mwengine wanakuwa wanachukua hatua ya kuwakamata wananchi na kuwapiga makwaju. Mkwaju maana yake ni bakora moja makwaju ni kuwatandika wananchi na hili mimi limenikera sana na naamini Mhe. Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili hawalijui hili kwa sababu mambo haya ya kupigapiga watu hawayapendi.

Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri sheria zipo hawa wananchi ni maskini, maeneo haya wamepakana nao kiasili miaka nenda miaka rudi wamerithi kwa babu zao, kama tunataka tuwageuze ili waujenge ufahamu mzuri zaidi na kuelewa katika masuala ya mazingira, basi tujaribu kuwatoa katika maeneo ambayo wanatumia ya asili kuwapeleka maeneo mbadala ili waweze kusaidiwa.

Mimi nimechukua juhudi za kutoa elimu katika masuala ya kuwapatia wananchi gesi, kutumia gesi hii ambayo tunatumia *LLG,* lakini pia tunaweza kuwasaidia vifaa tofauti katika kuhakikisha kwamba maisha yao yanakwenda vizuri. Mtu tumbo linakuuma njaa hasa kwa maskini ambaye maisha yake yeye mwenyewe hajui hata kesho mkono wake utakuwa anapata nini cha kwenda kula inakuwa ni vigumu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri suala hili utakapokuja unijibu vizuri ni kwa nini watu wako wanawapiga wananchi wangu, halafu utachukua hatua gani. Lakini tatu nataka ikiwezekana kwa muda ambao utakuwa muafaka wako wewe twende mimi na wewe mguu kwa mguu, pete na kidole kwenda kuona wananchi wetu ambao mimi nawawakilisha hapa

ili wakusikie na uniambie utaweza kuwasaidia vipi. *Otherwise* kama hapo leo nazuia fungu mpaka tutakwenda kwenye kura na kama nilivyosema sikuangalii wakati nasema maneno haya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo ukifungua kwenye ukurasa namba 13 wa kitabu wanasema kwamba juu ya biashara mafanikio yalipatikana katika mwaka 2017/18, tukienda kwenye kifungu G anasema katika eneo moja pilipili kichaa kilo 24.5 na vanila kilo 50 zimesafirishwa nje ya nchi kupitia Kampuni ya *Zenj Spice*. Kweli inawezekana jambo zuri katika kusafirisha nje lakini hebu niulize labda mimi sio mkulima najua Mhe. Hidaya Ali Makame ni mzoefu sana nitamfuata baadae anielimishe. Yeye ni mkulima na ameongelea kuhusu suala la muhogo, nimpongeze sana maneno yake leo yalikuwa mazuri sana alipoongelea kuhusu muhogo mtamu, niseme yeye pia alivyochangia leo maneno yake na mawazo yake yalikuwa mazuri sana kama muhogo mtamu wenyewe na sote tulilewa humu ndani. Sema muhogo wenyewe hauliki mpaka jioni maana yake sote tumefunga humu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kilo 24.5 za vanila hivi kweli ni mafanikio ya kuingiza katika kitabu hiki kutuletea hapa au waziri alitaka sisi tufahamu kwamba tayari wameanza kuuza pilipili kichaa halikadhalika wamesafirisha kilo 50 za vanila nje ya nchi. Sasa mimi naona hizi kilo na mafanikio kama haziendi sambamba labda waziri atakapokuja atufahamishe vizuri. Ni mategemeo yangu labda kwamba wameanza utaratibu wa kuanza kusafirisha pilipili kichaa, inawezekana lugha iliyokuwa hapa haijakaa sawa kwa hivyo utakuja utatueleza zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niulize swali la hawa mabwana shamba kuna tatizo moja ambalo inawezekana tunalo hatuliangalii ni *issue* ya jinsi tunavyoleta madawa lakini pia utaratibu mzima zinapoingizwa hapa Zanzibar. Kwa mfano, ukienda bandarini unapoleta kama hizi pembejeo na madawa kwa ajili ya maeneo tofauti ya Unguja na Pemba, watu wanapata tabu sana, kero zinakuwa nyingi sana, utaratibu inawezekana uliokuwepo una urasimu na unasumbua wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo *"Take care of the pence, then the pound will take care of themselves*". Maana yake kwamba wewe shughulikia visenti senti, ukienda navyo vizuri shilingi itajishughulikia wenyewe. Ni muhimu sana lazima tuangalie katika mzizi wetu watu wa chini tunapokwenda nao katika kuwasidia. Tunaongelea mambo ya juu juu mafanikio makubwa tunataka tuyafanye lakini huku chini tunakuwa tunajisahau. Kwa hivyo, hawa wananchi wa chini wanaofanya kazi kubwa sana katika kulima, kwenda kuvua lazima tuwatilie mkazo na tuhakikishe mambo yote ambayo yanaleta urasimu na kuleta kero tofauti katika maisha yao tunawaondolea.

Sasa mimi niombe katika masuala ya madawa mabwana shamba hasa kwa mfano sisi Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati, Jimbo langu la Tunguu wakulima wa Dunga, Bungi, kule Ungujaukuu tuna matatizo sana ya madudu tofauti, mimi madudu yenyewe sina uzoefu nayo lakini najua gharama wanayoipata kwenye machungwa, maembe wakilima sasa hawa wote lazima muwapelekee elimu ili waelewe.

Mhe. Mwenyekiti, kule Bara unakuta wakulima hawana elimu kubwa sana lakini wakati mwengine watu wanazalisha mazao mapilipili boga kama Baraza hili makubwa makubwa, ukiangalia mapilipili mazuri mazuri matamu. Lakini hapa kwetu tunazalisha vitu vidogo vidogo, leo ukienda kuvua unakuta samaki wadogo wadogo, kwa nini hatuwasaidii tukawapa nguvu zaidi

na sisi tukawa tunatamba tuko watu milioni moja na laki nne tukatenga fedha nzuri tukawasaidia wananchi wetu. Sasa niombe kwa mfano mimi mwenyewe kwa upande wangu Jimbo la Tunguu tuna mahusiano mazuri sana na Idara ya Uvuvi hasa Mkurugenzi wao ndugu yetu Mussa anatupa mawazo anakuja kutoa elimu hasa na kamati zetu za uvuvi na hizo juhudi aziendeleze katika Mkoa wa Kusini na maeneo yote ya Unguja na Pemba.

Mimi namshukuru sana na yeye pia ndie aliyenipa elimu hasa katika suala la nyavu kuweza kuwasaidia wananchi zile za inchi mbili. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri uwapatie wananchi zile nyavu zinazostahiki umemuona hapa Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa Chake Chake alivyoongea kuhusu nyavu, amesema tuna tatizo la nyavu, kwa nini hizi nyavu tusiwape wananchi wetu tukawasaidia zikawa bure, ili waende nazo wakavue mwisho wa siku samaki hawa tunakuja kula sisi tunakuwa tunapata lishe nzuri na tunakuwa tunaendeleza maisha yetu na tunaboresha afya zetu. Kwa hivyo, mimi niombe hizi nyavu au katika bei iliyopo wale ambao ni watu maskini kwenye maeneo hasa kaya maskini tuweze kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiri, jengine nataka nizungumze kuhusu *Zanzibar City Park,* Kituo cha Utalii Masingini. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa suala hili nikwambie mimi watoto wangu leo wamekwenda kutembelea *Zanzibar City Park* Masingini. Niombe sana kwamba msitu huu watu wa mjini wazidi kwenye *park.* Nimuombe na *AG* pia na yeye aende akatembelee na watoto wake kule, niwaombe ndugu zangu wote wajumbe waende wakatembelee maana yake kuna vitu vizuri vizuri hawa hawajafika. Najua mawaziri wanakuwa wako *busy* sana na pengine wao muda inakuwa hawapati, lakini niwaombe nao wakipata muda waende wakaangalie pamoja na wajumbe wengine wa Baraza. Misitu kama hii ni maeneo ya ku-*promote* hasa katika Kisiwa cha Kijani. Mhe. Mwenyekiti, leo ukipita Zanzibar maeneo yote barabarani kuna maduka ule ukijani ni sehemu moja muhimu sana, kwa hivyo hata wageni wanaokuja waweze kuangalia na kuona.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimalizie *issue* ya shamba la mipira. Mhe. Mwenyekiti, miti hii ninavyofahamu maisha yake ni miaka ishirini na tano tangu tulipopanda wakati wa uhai wa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, sasa bado yanaweza kuzalisha na muda gani, basi Mhe. Waziri aje kutuelimisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa suala la mwisho niseme tu kwamba Zanzibar tunajiita sisi *The Spice Island of Zanzibar,* yaani visiwa vyetu na sisi tunatumia kwa mambo ya *spices.* Sasa mimi niombe maeneo wawasaidie watu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na maeneo mengine yote kwamba hivi viungo kutumia tunapanda miti. Kwa mfano *lemon grass,* pale *Airport Terminal* mpya itakapokuja wawapandie miti ambayo itakayostahiki ukitoka nje ya *Airport* unaona kunanukia kama kuna *lemon grass* ambayo ni mchaichai, pengine kuna *cinnamon,* unaweza pengine ukaona *jackfruit*. Miti ambayo haitoleta ndege kutoa athari juu ya usalama na mazingira ya *Airport* yale ambayo yatakuwa na mvuto, na maeneo yote ya Unguja wanapotembea njiani basi watu wahimizwe wasaidiwe ili nchi yetu ya Zanzibar unapoingia iwe inapendeza Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyokaa hapo juu tunakuona ukiona uzuri wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai nakushukuru.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa nafasi uliyonipa na nimshukuru pia Mhe. Waziri, nitaunga mkono hoja iwapo nitapata mawazo yote na majibu yanayostahiki. Nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Simai kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Mtumwa Suleiman Makame, atafuatiwa na Mhe. Makame Said Juma na Mhe. Tatu Mohamed Ussi kama muda utaruhusu basi ajiandae.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa, naungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanallah Wataala* kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa na afya njema, vile vile kutujaalia kutupa nguvu na afya kuweza kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan na leo hii kuwa tuko katika siku ya kumi na tano. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie afya tuzidi kuimaliza funga yetu hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kututeulia viongozi wetu hawa wawili ambao ni wasimamizi wakuu wa Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa sababu wizara hii inashirikisha mambo chungu nzima ya kilimo, na wizara hii Mhe. Rais kawateua watu wawili ambao wana fani hiyo ya kilimo, kamteua Mhe. Waziri ambae ni mkulima na mvuvi, pia kamteua Mhe. Naibu ambaye ni msomi. Kwa sababu kilimo kinaendeleza mambo yote hayo ya uvuvi na usomi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi nina kidogo tu lakini pia nampongeza Mhe. Rais kwa kutuletea mapinduzi haya ya kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa kweli kilimo hichi kimewaneemesha wananchi wengi sana na kina faida kubwa sana kwa sababu wananchi wetu wanalima mwaka mmoja kwa misimu miwili. Lakini sasa bahati mbaya kuna wakulima wengine hawatumii kilimo cha umwagiliaji maji ambacho ni kilimo cha mabondeni wanatumia majembe ya matrekta. Sasa Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita nilichangia suala hili na Mhe. Waziri aliniahidi atalifuatilia lakini bahati mbaya kipindi kilichopita cha msimu huu pia wananchi wetu wamechelewa kulimiwa. Tatizo kubwa sana kwamba kilimo cha maeno ya juu ikifika mwezi wa Novemba wawe wameshalimiwa, lakini bahati mbaya inafika mwezi wa pili wakulima wale bado hawajalimiwa katika maeneo yao. Sasa wakulima wale wana masikitiko makubwa kwa sababu hawapati kuvuna mpunga ule ambao walioukadiria wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, zamani ilikuwa watu wanalima mbegu bora na nzuri sana ambazo ni mbegu za kialangawa, kijicho, kuna mbegu za vuli, kuna mbegu ya supa, kilimo hicho siku hizi hakipatikani kwa tatizo la ucheleweshaji wa kuwalimia wananchi wale wanaolima maeneo ya juu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wananchi wale wana masikitiko makubwa kwa sababu ilikuwa zamani wanalima mpunga huu wa mbegu hizi unakula bila ya samaki, wala hautaki nazi, ukipika mpunga wa mbegu ya supa harufu yake ukitoka nje unaisikia, lakini sasa hivi wanapanda mbegu ya nerika utoke hapo kwenye ukumbi wako husikii harufu yake. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anieleze kipindi hichi tunachoendelea nacho mwaka huu wamejipanga vipi kuwalimia wananchi hawa itakapofika Novemba, Disemba waanze kupanda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo naelekea kwenye kilimo cha muhogo, Mhe. Waziri ni mpya lakini sasa nakueleza kwamba kuna Jimbo la Nungwi eneo la Mjaja kuna wakulima wengi sana wanalima kilimo cha muhogo na eneo lile nina uhakika hulijui kwa sababu hujawahi kufika. Lakini ningekuomba ushirikiane na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi au hata mimi Mwakilishi wa Viti Maalum tukupeleke eneo la Mjaja ukawaone wananchi wa jimbo lile kule wanavyofanya kazi ya kulima muhogo ndani ya mawe. Muhogo ule kama alivyozungumza Mhe. Simai Mohammed Said kasema muhogo mtamu haujui lakini akenda Mjaja atauona muhogo mtamu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo naingia kwenye eneo la misitu kule Chaani ambalo linakaribia hekta 450 za misitu. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ unapokaribia wakati wa msimu wa kupanda anawachukua vijana wetu wanaelekea kule kwenda kupanda msitu ule. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililopo pale kwamba msitu ule ukishapandwa hawaupitii hata kuusaidia kupalilia, na kitu chochote kilichokuwa kinaatikwa kwenye ardhi lazima panaota gugu, ukishapanda baadae ufuatilie si hivyo mti ule unakuwa unakufa. Mhe. Mwenyekiti, eneo la Chaani Masingini ilikuwa kuna mtu ukisimama Kidodobaridi watu wa Donge huwaoni, au ukisimama pale unakwenda Mkokotoni na Cheju huoni, lakini sasa hivi ukienda eneo la Chaani Masingini ukisimama Kidodobaridi unaona mpaka Donge barabarani kwa sababu msitu ule haupo na haufanyiwi kazi kama ulivyokuwa unafanyiwa zamani.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa lililokuwepo kwenye msitu ule wafanyakazi sasa hivi kidogo, eneo kubwa lina urefu wa hekta 440 lakini kuna wafanyakazi wapatao kumi na tano. Je, eneo lile au msitu ule utaweza kuhudumiwa na wafanyakazi hao. Ningemuomba Mhe. Waziri eneo lile akalitembelea akaiona hali halisi ya msitu ule wa Chaani Masingini kwa sababu wananchi wa Chaani Masingini na Serikali ilikuwa inafaidika sana kwa msitu ule sasa hivi msitu ule haupo. Nakuomba Mhe. Waziri wewe ni mpya lakini usije ukageuka kama mung'unye kuona umeteuliwa tunakupasisha sana uzuri uzuri baadae ukageuka kama mung'unye ukawa mgumu. Mhe. Rais alikupa nafasi hiyo kwa kuwa alikuamini na ndipo alipokuteua, kwa hivyo nakuombeni msimuangushe Mhe. Rais mfanye kazi na majukumu aliyokupeni, majukumu hayo mmepewa sio mkae kitako juu ya kiti mzunguke na kiti, majukumu ya kilimo watu wa kilimo wako vijijini. Nakuombeni Mhe. Waziri pamoja na watendaji wako wote mfanye kazi ya kushuka chini kwa wananchi mkatekeleze majukumu yao wanayoyataka.

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo naingia kwenye vilimo vyetu hivi vidogo vidogo, sasa hivi tuna kilimo cha matikiti, mabiringanyi, tungule vilimo vile vyote sasa hivi wananchi wanatumia mbolea, akishaupanda mti wake haukui kama hujautia mbolea. Nakuomba na wakulima wale nao uwaingize kwenye kundi la kutoa mbolea sio mbolea zile muwe mnazitoa kwa wakulima wa mpunga na wakulima kama wale sasa hivi wanatumia mbolea ili kukuza yale mazao yao yawe mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nilikueleza mwanzo kwamba mchango wangu mimi ni mdogo tu. Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono hotuba hii lakini lile nililomuuliza Mhe. Waziri naomba aje anijibu swali langu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Mtumwa Suleiman Makame kwa mchango wako kutoka Kaskazini Unguja Nafasi za Wanawake, sasa naomba nimwite Mhe. Makame Said Juma, atafuatiwa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi na Mhe. Mussa Foum Mussa ajiandae.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo Alkhamis mwezi hamsataashara Ramadhan, Mwenyezi Mungu anijaalie kheri pamoja na wenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitaanzia masuala ya uvuvi kwa sababu ni fani yangu kubwa sana. Kwanza niishukuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa busara nzuri na mwelekeo mzuri inaowafanyia wavuvi wetu kuwa na hamasa na nguvu kubwa sana kwa sababu naijua serikali yetu inavyojitahidi na wavuvi wetu pamoja na wakulima katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na hivyo lazima tuzungumze changamoto za wavuvi wetu kwa sababu wavuvi wetu ni watu dhaifu kuliko watu wengi, sasa lazima tuwazungumze wizara hii iwaone kama na wao wana umuhimu mkubwa sana katika nchi yao kwa kile wanachokizalisha. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wavuvi hao hao ndio wanaobebeshwa mzigo mkubwa sana baada ya kuwahudumia watu lakini sasa na wao wanapewa kazi kubwa sana kwa kila watakachokifanya watu wale wale kuwasababishia kuwa na matatizo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza wavuvi ni watu waliokuwa na matatizo, upepo, mvua, jua linawakumba watu hao ambao wakati wote wanawahudumia watu walio juu almuradi wahakikishe watu wao wamepata kitoweo katika kula. *(Makofi)*

Lakini sasa tatizo lililopo kuthaminiwa ni kudogo, wanathaminiwa na serikali lakini kuthaminiwa kwao ni kudogo. Kwa sababu katika masuala haya ya uvuvi wengi hapa wanaothaminiwa katika orodha ya kitabu hiki msaada huu unakwenda sana katika wavuvi wa kombe, chaza na wengine wadogo wadogo, lakini wavuvi wa nyavu humu hawakutajwa. Kwa sababu wao ndio wanaozalisha sana lakini hawaonekani kama wao ni wazalishaji bora.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwenye utafiti huu sifikirii lakini naona kama utafeli kwa sababu serikali ina mpango mzuri wa kufanya utafiti katika bahari yetu na bahari yetu ina haja hasa ya kufanyiwa utafiti, lakini utafiti huu uende vizuri. Kwa sababu nia ya serikali ifanye utafiti wa maji madogo na maji makubwa, pia serikali hii ifanye utafiti wa samaki wetu ambao wako ndani ya bahari yetu. Mhe. Mwenyekiti, bahari yetu sana samaki wake wako ndani ya bahari, ni ndani sio nje, samaki wa nje ni haba sana katika bahari yetu ambao tunawapata sisi katika kuwatumia na ambao tutawauza katika masoko mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu ni watafiti lakini sijui wamesahau maana hata majina ya samaki humu wengine yamepandikizwa katika kitabu hiki, tufungueni katika maeneo ya samaki muangalie huyo pono na naamini nyote mnamuona, huyu sijui pono gani sifikirii wala hayupo hata katika jamii moja ya pono, katika jamii kumi na moja za pono sijawahi kumuona pono huyu. Namjua kama ni samaki gani lakini siwezi kumwita pono wala mfano wake, maana hao kolekole nimemuona mzuri tu lakini hakutaja ni kolekole gani, maana yake hawa kolekole nao wanafika zaidi ya aina kumi na moja, hao tasi nao usiseme, huyu mzia tena nao usiseme kama ni aina ngapi. Kwa ufupi wamewataja kama samaki sita tu lakini kitabu hichi nafikiria kama kilitungwa Bara maana yake wanyama ndio wengi, samaki ni kabila sita tu wengine hata majina yao hawakutambulika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwaboresha wavuvi serikali ipo haya ya kuwaboresha wavuvi wetu kwa namna mbali mbali, lakini hususan kuwaboresha katika miundo ya kisasa. Maana nakumbuka wavuvi tulikuwa na shida sana, zamani nakumbuka hao wavuvi wakubwa waliokuwa wakivua ambao hawa wamezidi kiwangwa walikuwa watu kumi na mbili, na tena hao wakihesabiwa kama leo hichi ndio chama kikubwa lakini tumebadilika. Sasa hivi chombo kimoja kinachukua watu zaidi ya mia moja na zaidi kwa sababu hali ya mazingira tayari watu wamefahamu na uvuvi wa kisasa na kuboresha uvuvi wa kileo. Ipo haja sasa hivi kubadilika, zamani mvuvi wa pweza akivua peke yake lakini sasa wavuvi wa pweza wanavua zaidi ya watu ishirini chombo kimoja. Lakini bado wavuvi hawajaboreshwa wanajiboresha wenyewe kwa kukuza mambo yao, lakini ipo serikali sasa ifanye mabadiliko, fedha hii inayotengwa kwa wavuvi isipelekwe tu kwa wavuvi wadogo wadogo hao ambao ndio wenye kufuga samaki wa maziwa ya kawaida au wengineo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuna tabia moja ya wachuuzi wetu kuidhalilisha nchi yetu na kuwakosesha wavuvi wetu uhalisia wa wale samaki wetu. Kwa sababu nakumbuka juzi moja tu nilitoka hapa nikaenda zangu nyumbani nimekutana na Mhe. Viwe Khamis Abdalla akasimama sehemu akanunua samaki, kufika pale Mhe. Viwe akaniuliza huyu samaki gani unamjua, nikamwambia samaki simjui, akaniambia aka wewe ni mvuvi humjui. Yule mchuuzi akamwambia huyo si mvuvi nikacheka namuangalia samaki simjui kwa sababu hivi unavyoniona kumuona tu samaki nimezama kuanzia Kusini mpaka nimefika Kaskazini sijamuona samaki huyu katika bahari zetu hizi za nje na za ndani hayumo. Samaki huyu hayumo hasa kabisa haya muulize ni samaki gani? Akamwambia ni kolekole, akamwambia ehee! kolekole huyo, alimwambia muulize kolekole gani? Akampa jina la kolekole Salehe. Loh! Nilisikitika sana nikasema kumbe kuna watu wanawapotosha hawa samaki, leo samaki huyu Tanzania yetu hii katika bahari hii hayupo lakini leo kaambiwa kapewa jina la samaki wetu wa Zanzibar.

Nikasikitika sana nikamwambia Mhe. Viwe Khamis Abdalla huyo samaki chukua tu lakini si samaki wetu wa bahari yetu hii sijawahi kumuona hata siku moja na wala hayupo. Akanambia wewe huwajui lakini yule baada ya kumwambia akamwambia huyo si mvuvi, akasema huyo Mkojani? Yule mchuuzi alinyamaza hakusema tena aliona huyu mtu labda ameshanigundua, siku ya pili nikamuuliza Mhe. Viwe yule samaki umemuonaje? Akanambia yule samaki hafai tena hafai na ni kweli, jamani tunakula samaki ambao si wetu na wala hawapo katika bahari yetu, lakini wakati hamumfahamu mtapata tabu sana na mtakula samaki ambao hawapo katika nchi yetu na wala hawana ladha. Naamini hapakosi kama watu wengine mmeshawahi kumla au mmeshamuona ni mweupe ana urinda hapa wa buluu huyo samaki muangalieni sio samaki wa bahari yetu, na hata mkenda kumla mtamuona kama huyo samaki sio wetu. Na bahari yetu kutoka Kusini mpaka Kaskazini basi samaki huyo hayuko hao wanaotuuzia samaki wale waulizeni vizuri. Wizara inastahili iwafuatilie hawa samaki itafika wakati tutakula vitu vilivyokuwa havimo katika mazingira yetu halafu waje watusababishie matatizo, waje wageni waseme Zanzibar ina samaki hawafai na kumbe samaki wale hawatoki kwetu wamepandikizwa tu katika nchi yetu na halafu wamepandikizwa majina ya samaki wetu. Samaki wetu mimi nafikiri wanajulikana.

Mhe. Mwenyekiti, watafiti wetu kama watakwenda watawaona katika sehemu mbali mbali basi natumai hawatapata tabu, wala wasiende bahari za nje hata humu humu bahari za ndani watawagundua samaki wote na bahari za nje maeneo ya matokeo ya jua natumai samaki wetu

watakuwa wameshamaliza kutoka ndani. Maana yake hawa samaki wanapishana unaweza ukamkuta samaki katika bahari yetu hii hapa ukenda Tanzania Bara samaki huyo hayupo, lakini unaweza ukaenda Bara ukamkuta samaki Zanzibar hayuko. Kwa mfano, tuna baadhi ya samaki wengi mnamjua, kuna samaki anaitwa makonge ya mtepa maana yake ni makonge ni marefu lakini hayana miba, tofauti na makonge ambayo yana miba Zanzibar hulioni, unaweza ukamaliza Zanzibar nzima na Pemba yake lakini samaki huyo humuoni isipokuwa utamuona Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kuna samaki wengine pia Bara hawako, lakini kama hujui hivyo unaweza ukasema samaki wote wapo tu. Sasa lazima serikali ifanye utafiti wa kutosha na ikifanya utafiti huu isifanye utafiti na wataalamu wa kisomo ifanye utafiti na wavuvi, kama haitawachukua wavuvi utafiti huu mara nyingi sana samaki mwengine mtamwita pono, mtamchukua samaki jina lake hamlijui mkamwita pono. Samaki huyu ninavyomfahamu mimi kwa kuwaambia wavuvi tu, au waliokuwa hawamfahamu kwa jina la kivuvi ana majina mawili, ana jina la Biti Sudi huyo samaki wenyewe anayeitwa pono, natumaini mkifungua kitabu mtamuona anaitwa Biti Sudi au kwa jina jengine anaitwa Gomviro. Sasa majina haya mawili utampata lakini ukisema kama umwite pono utakuwa mtihani na utawababaisha watu sana. Kwa sababu mimi nilipomsoma hapa niliangalia nikasema pono huyu kapatikana wapi dunia hii, au kapatikana katika bahari gani katika hawa watafiti wetu ambao wanajaribu kuwasoma samaki wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Makame Said Juma: *Inshaallah.* Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele wavuvi wetu kuboreshwa naiomba serikali wakati pesa hizi kama zilivyo ili kuwasaidia wavuvi basi iwatafutie zile mashine, siwaambii watafute nyavu kwa sababu nyavu utakazowatafutia vyovyote hatawafaidisha vile wanavyotaka. Kwa sababu kila mvuvi ana fani yake na kila uvuvi una aina yake, msifikirie kama wavuvi wote wanavulia nyavu tu, nyavu ni aina nyingi sana. Kuna wengine wanatafuta nyavu za kutega, wengine nyavu za kuvuta, kuna wengine wanatafuta nyavu za kawaida. Kwa sababu sisi wavuvi tunaweza tukachukua nyavu zaidi ya kumi chombo kimoja, tukikuta samaki hawa tunabadilisha nyavu, tukikuta hawa tunabadilisha nyavu, kwa kila samaki kuna namna yake ya kumvua sio kama samaki wote wanavuliwa kwa nyavu tu. Ile nyavu utakayoichukua basi unaweza ukaibadilisha mazingira pale pale kwamba hii kwa samaki huyu itabidi nimzamishie, kwa samaki huyu nimuwekee juu mpaka utakapomuona yule samaki mazingira yake alivyo, lazima uwajue namna zao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii iwasimamie wavuvi sana na ikiwasimamia iwaboreshe kwa kuwapa mashine. Serikali haina tabu kwa hivyo, lakini kwa kusema kama iwaboreshe kuwakagua kwa kuwaambia msivue dagaa. Hili Mhe. Mwenyekiti, nawaza haitakuwa faraja kwa wavuvi wetu, wavuvi wetu faraja yake ni kuboreshewa miundo mbinu ya kisasa, wapatiwe mashine, wapatiwe vyombo vya kisasa. Isipokuwa tu Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo moja ambalo serikali ikija ikilifanya sijui itakuwa vipi. Maana yake kuna meli ya uvuvi naambiwa itakuja haijaja, kuna watu wameambiwa wamekwenda kusomea katika fani ya uvuvi lakini sijui wametoka wapi katika dunia hii ya Zanzibar.

Maana yake sijasikia hata siku moja Kojani kumetolewa mtu mmoja kwenda kusomea angalau akaja kusomesha na wenziwe. Lakini namuomba Mhe. Waziri hili anifahamishe kidogo halafu ni watu wa aina gani, maana pengine wamechukuliwa watu chuoni wanasomea uvuvi wakawaambia kama ni wavuvi, sasa wakawakosesha wavuvi haki zao na wao wamesoma. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Makame Said Juma kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Tatu Mohamed Ussi atafuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa kama muda utaruhusu Mhe. Mohamed Said Mohamed ajiandae.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kunijaalia nikasimama mchana huu ili kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2018/2019 ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii wa Unguja na Pemba kwa jinsi wanavyofanya kazi zao katika kutumikia sekta hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo pamoja na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu unaanza kwenye Programu Ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Kilimo kama walivyozungumza kwenye kitabu chao kwamba ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara, kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri kwa wataalamu na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba wizara hii ndio kazi yake, lakini naiomba ili programu hii ifanye kazi zake vizuri na ili maendeleo ya kilimo yaweze kufanikiwa na yawe makubwa zaidi, basi niwaombe wataalamu wa kilimo kupita kwa wananchi kuwafunza au kuwapa elimu ya kilimo. Kwa sababu tumeona kwamba kuna baadhi ya wakulima wetu bado wanahitaji elimu kama vile miongo ya kulima, miongo ya kupanda, lakini hata katika utiaji wa pembejeo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja kwenye mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2017/2018. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze mafanikio hayo yaliyopatikana kuna kifungu (g) katika kitabu hiki ukurasa wa kumi na tatu ambacho kinasema jumla ya wafanyakazi 35 wamepatiwa mafunzo ya usarifu wa vanila.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nipongeze hatua hii, lakini katika kifungu hichi kuna mambo mengi yametajwa mfano kama vile tangawizi, pilipili manga, mdalasini na pilipili hoho, na yameanza katika wilaya moja ya Kusini Unguja. Sasa nilikuwa nashauri wizara kwa sababu mazao haya na tuna maeneo mengi ya sehemu za mawe, basi wizara kuendelea kuwapa mafunzo au kuwapa utaalamu wakulima wetu ili yaendelee kulimwa katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Kwa sababu tuna maeneo mengi ya maweni ambayo mazao haya yanakubali na kuota na kuzaa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije Programu ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba nije kifungu (a) ukurasa wa 39 kifungu cha 62 ambao kuna changamoto. Mhe. Mwenyekiti, tumeona

changamoto ya kwanza (a) inasema uchelewaji na upatikanaji wa pembejeo, matrekta na michango ya wakulima katika huduma za kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa nataka kujua ni huduma gani ambazo walikuwa wanatakiwa wachangie, na kama wametakiwa kuchangia je, wameelimishwa kama katika msimu wa kilimo hichi tunahitaji wakulima mchangie kiasi gani pengine au mnatakiwa mchangie kitu gani. Kwa sababu kuna baadhi ya wakulima wanakuwa hawajui, kwa hivyo ningeomba nijue ni michango gani ambayo wanatakiwa wachangie.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi hichi kuna mambo ya pembejeo. Mhe. Mwenyekiti, wakulima wengi wanakuwa wanalalamikia suala la pembejeo, mfano mbolea zinakuwa hazitoshi, sijui inakuwaje mbolea zile kutolewa kidogo na kusababisha malalamiko kwa wananchi wetu. Hivyo, naishauri wizara kuliangalia suala hili kwa ufanisi ili wakulima wetu wafaidike na pembejeo hizo kwa ajili ya kupata kilimo kilicho bora.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije tena kwenye changamoto kushuka kwa bei na mripuko wa maradhi ya mwani. Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunasikitika sana siku zote tumekuwa wanawake tukizungumzia suala la bei ya mwani, na kwa nini tunazungumza suala la bei la mwani kwa sababu wakulima wengi wa mwani ni wanawake. Sasa kwa kweli tukiona hivi ingawaje wizara imesema inachukua juhudi za kufanya utafiti na kupata kuongeza bei ya mwani. Kwa hivyo, naiomba wizara kuliangalia tena kwa jicho la huruma suala hili la bei ya mwani kwa sababu wakulima walio wengi ni wanawake na bei kwa kweli haitoshelezi mahitaji ni ndogo ukilinganisha na kazi zinazofanywa hata mwani huu ukapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 40 Matumizi Mabaya ya Misumemo ya Moto. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunasikitika sana suala hili la misumeno ya moto kwa sababu linapelekea uharibifu wa mazingira miti kukatwa na hata hali ya hewa inakuwa si nzuri. Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara hii inayohusika na maliasili na misitu kuliangalia vyema suala hili kwa sababu tunaona rasilimali yetu zaidi sasa hivi wapigaji makaa wanapiga makaa kwa kukata mikoko, sasa mikoko ikikatwa ni hatari matokeo yake bahari inakuja juu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kitengo hichi cha maliasili kuangalia sana suala hili la ukataji mbaya wa miti yetu ya mikoko.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo narudi kwenye ukurasa wa 17 kilimo cha umwagiliaji. Mhe. Mwenyekiti, nimeona maeneo ambayo yanashughulika na kilimo cha umwagiliaji maji nikiona eneo moja la kwetu Makombeni ambalo hili ni kweli linalima kilimo hichi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimshauri Mhe. Waziri kuona kwamba katika Wilaya ya Mkoani kuna maeneo mengine ambayo kilimo hichi kinaweza kulimwa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Idara hii ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji iangalie na mabonde haya yafuatayo:

Kuna bonde la Giriama lilioko Mtuhaliwa, kuna bonde la Mtakakaa lilioko Mtambile, lakini kuna bonde la Mizingani ambayo mabonde haya yakilimwa na wakulima wakipewa elimu basi wanaweza kufaidika na tukaweza kupata mazao ya kutosha na kuongoza uzalishaji wa mpunga. Nilikuwa naiomba wizara iangalie maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache tu kwa sababu mengine yameshazungumzwa sina haja ya kurudia rudia. Nasema niwapongeze tena watendaji wa wizara hii lakini niwaombe wasimamie vizuri utekelezaji wa majukumu yao. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Tatu Mohamed Ussi Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake kutoka Mkoa Kusini Pemba kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Mussa Foum Mussa, atafuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Masoud Abrahman Masoud ajiandae.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa ya kuchangia wakati huu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri. Vile vile niwapongeze Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kutuwasilishia hotuba hii ya kitabu chao hiki cha kilimo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kitabu chao ni kizuri sana isipokuwa kuna mambo tu kidogo itabidi tuyachangie ili kukiboresha kupata ule ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza kuchangia katika masuala ya kilimo na hasa nitakwenda katika hichi kilimo cha biashara. Mhe. Mwenyekiti, humu katika ukurasa wa 13 pamezungumzwa hapa kuna vilimo hivi naomba ninukuu kifungu J ili nipate kuchangia vizuri.

> "Jumla ya wafanyakazi 35 wamepatiwa mafunzo ya usarifu wa vanila, vile vile wizara imewahamasisha wakulima wa maweni kuendeleza kilimo cha pilipili hoho kwa Wilaya ya Kusini Unguja. Aidha, wastani wa tani tatu matunda makavu na moja tangawizi, pilipili manga kilo 165, mdalasini kilo 2,270, pilipili kichaa kilo 24.5 na vanila kilo 50 zimesafirishwa nje ya nchi kupitia Kampuni ya *Zenj Spice*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kwanza niipongeze hii hali kwamba jambo hili ni zuri, lakini katika kuchangia nataka niseme kwamba tukiangalia mipango yetu mizuri, lakini ndani yake kuna kasoro. Kwa mfano, ukiiangalia hii hali ya vilimo hivi vilivyosafirishwa kile kima kidogo, na kwa nini kiwe kidogo? Na hali yetu tukiifanya vizuri ile idadi ya usafirishaji itakuwa kubwa.

Kwa mfano hapa wameeleza kwamba wameshajihisha watu Wilaya ya Kusini Unguja wakipanda pilipili hoho. Kwa nini washajihishe Wilaya moja tu? Hapa ndio penye kesoro ilivyotokea kwa sababu pilipili hoho mimi nataka nijitolee mfano katika jimbo langu la Kiwani. Mimi fahamu zangu kwetu katika Shehia ya Muambe kunalimwa pilipili hoho. Mimi udogo wangu niliwahi kwenda kuchuma kibarua kama karafuu inavyochumishwa kibarua na pilipili hoho zamani ilikuwa inachumishwa kibarua. Mimi nimeshachuma pilipili hoho pishi moja pesa kumi na zilikuwa ziko nyingi. Leo hapa mnatwambia mmesafirisha pilipili hoho kilo 24.5 kupeleka nje. Ah! Hii ni kusema aibu, hapa hatujafanya kitu, hapa tunatakiwa tushajihishe wakulima ili watu walime hili zao.

Mhe. Mwenyekiti, mambo ya kufanya yapo mengi kwa mfano ukichukua hii vanila huu zaidi ya mwaka wa 20 tunaizungumza vanila. Nakumbuka kule kwetu kulikuwa kuna msitu unaitwa

msitu wa ulingo, kuliwahi kuja kufanyiwa utafiti wa kufanywa hii vanila lakini msitu ule watu wameumaliza vanila yenyewe wizara haikulishughulikia hili hili zao matokeo yake limepotea.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wakati mwingi mambo yetu tunapanga mazuri lakini utekelezaji sio. Kwa mfano, nije ukurasa wa 51 katika suala hilo hilo (f) kunaelezwa huku mwaka uliopita lakini sasa tunaendelea mwaka ujao. Kifungu (f) inaeleza "Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya viungo kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi ikiwemo vanila, pilipili hoho, manjano, tangawizi na pilipili manga katika hekta (5) za mashamba ya mpira Unguja na Pemba". Yaani mazao haya yote yaliyoelezwa hapa yametajwa hekta tano katika mashamba ya mpira Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, bado tunafanya utani, bado hatujaazimia kuyaendeleza haya mazao kibiashara. Kwa mfano, hapa mimi nilitegemea kwamba kitabu kitaeleza kwa mwaka huu basi tutawashajihisha wakulima zile sehemu zote ambazo mazao haya yatalimwa. Hapa tungeelezwa kwamba pilipili hoho tanatarajia kuziendea Wilaya zote zilizobakia ili kushajihisha wakulima, lakini tunaelezwa kwamba hekta tano katika mashamba yale ambayo hapa hatujaeleza azma ya hili suala kuliendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hebu tubadilikeni ili kuona kwamba hii azma yetu nzuri tuwashajihishe, hapa tungelisema kwa mara hii tutapeleka mbegu za pilipili hoho zile sehemu zote za ulikulima wa maweni ili hili zao lilimwe tupate mavuno yaliyo mengi. Lakini hapa tunarudia tena kule kule mwakani sijui tutakuja kuambiwa hapa zimesafirishwa kilo ngapi. Basi Mhe. Waziri akipenda Mwenyezi Mungu tukiwa hai tutakuja kusikiliza je, mwakani umesafirisha kilo ngapi za vanila, kilo ngapi za pilipili hoho, tusitegemee kwamba tena baada ya 24.5 tuambiwe kwamba tumesafirisha kilo 50 hiyo bado itakuwa hatujafanya jambo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba maeneo ya kulima pilipili hoho tunayo mengi. Kwa mfano, katika jimbo langu mimi tuna Shehia ya Shamiani Muambe, tuna Shehia ya Muambe, tuna Shehia ya Jombwe, Shehia ya Kiwani Mtangani, Kisiwa Panza/Makoongwe, humo mote pilipili hoho inafanyika na inatendeka vizuri na wananchi wetu watapata mavuno mazuri na watapata kujiendeleza wakulima wetu, tuamkeni.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye uvuvi. Kitabu kimeeleza hapa kwamba wataendelezwa wavuvi vijana ili wavue katika Bahari Kuu na kuyafanyia utafiti zaidi yale maeneo yenye samaki wengi. Mimi hili naunga mkono kwa sababu tukitaka tusitake sisi nchi yetu ni visiwa, tumezunguukwa na bahari. Sisi nchi yetu hatustahiki kuagizishia peduu, mpaka leo hii hapa Zanzibar tuje kuletewa samaki kutoka sehemu nyengine na sisi tumezungukwa na bahari. Ni vyema wananchi wetu hususan vijana wakaendelezwa kwenye masuala ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano mimi ninayo shehia yangu moja Shehia ya Chole, vijana wote waliokuwepo kule kazi yao ni kuvua lakini mpaka hii leo bado wanavua ule ule uvuvi wa zamani, uvuvi wa mshipi samaki mmoja, ndoana moja samaki mmoja. Hii imepitwa na wakati, wale vijana ni vyema wakaendelezwa katika uvuvi huu. Tuna Shehia ya Shamiani iko hiki ni kisiwa kimezunguukwa na bahari, Kisiwapanza, Makoongwe. Huku kote kuna vijana ambao waendelezwe ili kuona kwamba sisi Zanzibar tunajitosheleza kwa samaki, tusiwe tena sisi tunaagizishia peduu. Hatustahiki hivyo, samaki wapo wengi mameli ya nje siku zote hapa

yanakuja yanatuibia samaki sisi tumelala. Nadhani Mhe. Waziri, wizara hii ipige hatua ili kuona kwamba na sisi tunajitosheleza kwa samaki hapa nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nimwambie Mhe. Waziri Wizara yako ndio inayoshughulika na mashamba ya eka, mashamba ya mikarafuu. Sisi kule Pemba kuna mashamba mengi ambao wengi waliyopewa mashamba haya wamefariki dunia kwa muda mkubwa, sasa haya mashamba wamekabidhiwa watu wanayaendeleza. Lakini kwa mfano kama mwaka huu kulitokea mtihani mkubwa, wale watu waliopewa mashamba kuyaendeleza na haya mashamba wamepewa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kama mnayo barua hapa ya mzee mmoja anaitwa Hamad Vuai Haji, huyu amepewa shamba hili tangu mwaka 1995 analiendeleza. Lakini unapofika wakati wa kwamba karafuu zimeshazaa lazima anaambiwa akodi tena atoe pesa taslimu hana, inabidi shamba lile akodishwe mtu mwengine. Kuna watu mashamba haya yamekodishwa mpaka hii leo wale wanaoshughulikia ile asilimia yao hawajapewa.

Mhe. Mwneyekiti, mimi pointi yangu iliyokuwepo hapa kwamba huyu mzee kaliomba shamba tangu mwaka 1996 mwaka huu wa 22. Nakuomba Mhe. Waziri haya mashamba hawa watu waliyoyaomba wafikiriwe ili iondokane hii kadhia wakati mashamba yanapozaa tena isiwe tena kwamba hawa wakodishwe hawa wasikodishwe, iondoke hii kadhia. Ufuatwe utaratibu watu wayaombe na wale wanaoomba wanaostahiki kupewa wapewe ili haya manung'uniko yaondoke, mara hii kuna manung'uniko makubwa watu wameyashughulikia mashamba, wameyachukua mashamba, wamepanda mikarafuu, siku ya siku anakodishwa mtu mwengine yeye hata ile asilimia yale iliyobakia hapewi. Hili sio jambo zuri hii nchi ni yetu sote na wananchi ni wetu kwa hivyo wanastahiki na wao wapewe haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naona nisiendelee sana kuchangia hayo tu yanatosha. Naomba tu wale wavuvi wetu wadogo wadogo na wakubwa waendelezwe ili kuona kwamba vijana wetu na wao wananufaika katika nchi yao. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo mimi naunga mkono hoja na naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mussa Foum Mussa kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) na mchangiaji wetu wa mwisho leo kama muda utaruhusu basi atakuwa Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana, lakini vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri sana. Pia nimpongeze Dkt. Makame Ali Ussi, Naibu Waziri wa wizara hii kwa kutujibu vizuri mambo ya kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 17 wa kitabu chetu hichi. Mimi nitakwenda sana kwenye vitabu leo sitaki kuchangia sera zaidi. Kitabu hichi kinasema: Utekelezaji wa shabaha na programu ndogo ya maendeleo ya umwangiliaji maji. Wameeleza mengi sana niwapongeze sana kwa hatua yao kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. Lakini nilikuwa nina matatizo na hii sera ya umwagiliaji maji. Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali

Mohamed Shein tangu alipokuwa akiingia madarakani anahubiri kilimo cha umwagiliaji maji (*rice irrigation)*, tangu alikuja kijana Rais Shein mpaka ameota ndevu zimekuwa nyeupe anasema *rice irrigation*. Jambo la kushangaza mpaka leo wizara kubwa hii haijafika popote. Sasa na leo wanatuletea kutuomba pesa hizi hizi za *irrigation*. Niseme sana sitakuwa au nitakuwa mgumu sana wa kupitisha fungu hili na Makatibu muandike hii nataka nizuie fungu la *rice irrigation* kwa sababu halina maana nimeliona.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais aliaminishwa akapewa mbegu ya nerika, akapewa trekta akapanda akenda akavuna, leo nataka niulize katika hawa Wawakilishi wenzangu wa shamba nani kapata nerika mpaka sasa hivi. Kikaja kilimo chengine cha kupiga goli la kisigino kinaitwa Shadidi nacho hatukukiona. Lakini tukaaminishwa tena Mhe. Hamad Rashid Mohamed akaja akasema sasa mtanunua mbegu hii itakuweko pale Maruhubi inauzwa, bado hatujaiona vile vile. Sasa sijui tuna tatizo gani au hatuna wataalamu, si kweli kama hatuna wataalamu wa kutosha. Tuna wataalamu wa kutosha Mhe. Mwenyekiti. Lakini ninasema nitakuwa mgunu sana kupitisha fungu hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 31 Programu ya Maendeleo ya Uvuvi. Niwapongeze sana kwa hatua yao kubwa ya kuweza kuwashajihisha wavuvi wakavua. Lakini bado hatujaitumia ipasavyo bahari yetu kama wanavyosema na kwenye kitabu hichi kasema jumla ya doria hizo kafanya ngapi, nina wasi wasi na takwimu zilizotajwa humu kuwa hizi ni takwimu za kupika, nataka kutoa mfano. Mheshimiwa ukienda kwenye soko letu la Darajani kuna mizani gani ambayo inapima takwimu za samaki wingi wake. Leo kuna diko gani hapa Zanzibar linapima na nina wasi wasi sana kuwa hizi ni takwimu za kupika sio sahihi kabisa, niwaambie tu wajitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, usimamizi wa hifadhi hizi za baharini ambao wanaitwa *Marine Conservation Area* bado hapa kwetu hatujautumia ipasavyo. Aidha, unakwenda kwa maslahi ya mtu mmoja au kikundi cha watu ndio kinakwenda katika maslahi haya. Niliwahi kutembelea Pangani Tanga nikakuta jinsi gani hifadhi hizi zilivyowasaidia wananchi kujenga skuli na maabara. Leo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aniambie ni kijiji gani wamefanya hivi, ni kijiji gani wamefanya hivi. Na kubwa tukitaka humu tutaambiwa huyu kasaidiwa tanga, huyu kasaidiwa foromali, huyu ngarawa yake imefanywa hivi, hatujaweza kuitumia ipasavyo. Katika *Conservation Area* kuna watalii wanalipa kodi na baada yake tuna-*create* migogoro ya mara kwa mara. Tunawaomba sana wenzetu mfumo huu uliokuwepo sio sahihi, waje hapa watuambie sasa tuna mfumo huu tunaendeleza ili tuone basi faida ya *Conservation Area* iko kwetu. Juzi juzi tumepitisha tu ya *CHABAMCA* na *TUBAMCA* nayo pia sijui kama itakuwa na faida kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kwenye Soko la Malindi. Tulikuwa tuna Soko la Malindi hapa kila mwaka nimeangalia vitabu vya tangu 2013/14, 2014/15, 2015/16 vya iliyokuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, bado inatwambia eneo lile lililotengwa miundo mbinu tayari imekamilika. Lakini lini itakamilika au *UNESCO* imezuia? Hebu tuambie Mhe. Waziri utakapokuja kitu gani na umetwambia miundo mbinu ile imekamilika tangu vitabu hivi vyote ambavyo ninavyo mbele yangu nimevitaja navisoma, tuweze kuona faida gani tumepata mpaka sasa hivi au tumefikia wapi hata soko lile au diko lile linajengwa kwa ukamilifu wake, linatutia simanzi sana.

Mhe. Mwenyekiti, twende kwenye ukurasa wa 33 kuundwa kwa Kampuni ya Uvuvi. Mimi niipongeze sana serikali kwa kazi kubwa ambayo imeona imefanywa na kuweza kuirudisha kampuni ya *ZAFICO*.

Moja, Mhe. Mkurugenzi aliyeteuliwa hapa tunamjua anavyofanya kazi zake vizuri sana. Lakini khofu yangu ilikuwa tusije tukarudi kwenye vibanda vile vya dagaa vya Jang'ombe na Mwembenjugu. Lakini kwa huyu aliyepewa nadhani nimeangalia malengo ambayo ameyazungumza hapa anavyoweza kuyatekeleza yanaweza kuwa malengo mazuri sana na shabaha kubwa. Mimi nimpongeze sana na nimwambie tu aendelee na hizi programu zake.

Moja, inasema kuanza kuratibu na ununuzi wa meli za uvuvi. Sasa mimi hili nilikuwa na shaka nalo sana na kampuni amezitaja hizi zote ambazo wabia wake. Nampongeza sana kwa sababu hatua zake nazijua. Lakini Mheshimiwa nikiangalia kitabu hichi cha 2015/16 kinasema katika hizo hizo kulikuwa na pesa zimetengwa bilioni mbili ambazo SMZ inatoa milioni mia mbili lakini washirika wa maendeleo wanatoa bilioni nane kununulia meli hizo.

Lakini Mheshimiwa kuna kitabu chengine cha wizara hiyo hiyo iliyokuwa Mifugo na Uvuvi 2013/14 anasema tena pesa ambazo zilizotengwa za washirika wa maendeleo ni dola milioni 22,323,529. Lakini kwa upande wa serikali ikatenga milioni 300 za kununulia hizo hizo meli ambazo zitawafaidisha vijana 60 kwenda kuvua bahari kuu.

Lakini bado na kitabu chengine ambacho cha Wizara iliyokuwa ya Mifugo na Uvuvi 2014/15 tena. Anasema pesa zilizotengwa ndio zile zile milioni 22,323,529. Lakini hapa pesa zimepunguzwa za Kitanzania zimekuwa milioni moja. Lakini pesa hizi katika miaka yote hazijajitokeza kwenye vitabu vyovyote. Nataka tukuulize Mheshimiwa pesa hizi na dhamira yake je, zilitiwa kule kwenye kampuni ya *ZAFICO* au pesa hizi zimeingia na watu wasiojulikana? Tunataka tujue tu kitu kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niendelee tena kidogo sana kwenye Bahari Kuu. Niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya bahari kuu kwanza kwa kulinda bahari yetu na kuona basi sehemu kubwa ya bahari yetu imetulia na iko salama.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema tu kitu kidogo sana hapa tumeambiwa tumeona mapato yameshuka. Tukiangalia kwenye kitabu hichi cha fungu L01 ukurasa wa 23 mapato yameshuka kutoka mwaka 2017/2018, mapato yalikuwa shilingi 4,930,197,000/-, lakini mwaka huu ambao 2018/2019 imepangwa itakuwa ni shilingi 12,500,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, pesa zimeshuka sana hatujui, lakini sasa ije inambie ni sera gani zilizobadilisha kwa sababu tu hapa asilimia 30 inakwenda Bara asilimia 20 inakuja kwetu Zanzibar na asilimia 50 ni pesa za uendeshaji *(operation cost)* ya mamlaka yenyewe zinaingia pesa gani au baada ya kubadilisha sera hizi zimekuwa hivi.

Lakini hapa panasemekana kuna meli iko Mtwara sasa, na Mtwara pale tunaishikilia meli ile lakini sasa kila siku inatula kwa kulinda bidhaa ile ya mle tunawasha jenerata sisi ambao ndio ambao tunalipa *fuel* ile iliyokuwemo mle. Tunaomba sana Mhe. Waziri hili uje utwambie na

hapa nitakuwa mgumu kidogo nataka nizuie mshahara Mhe. Waziri, nataka kusema natoa nia na nataka nizuie shilingi yangu ili tusiende mbele hapa lazima niulize pesa hizi za walipa kodi zinatumiwa kwa jambo gani.

Mhe. Mwenyekiti, naingia sasa kwenye kitabu kikubwa moja kwa moja …
Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa una dakika tatu kama sikosei.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Ndogo sana kwangu nitajitahidi tu. Nakwenda kwenye viashiria na kama nyengine nitamuandikia kwa maandishi, lakini naomba nasema wazi kuwa nitazuia shilingi yote kwa pamoja *(in general).*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye fungu la LO1 (4) kuna kiashiria cha idadi ya mabwana na mabibi shamba. Mwaka 2017/2018 wamekuwepo na 179 lakini 2018/2019 imekuwa wametenga kuwa na mabibi shamba na mabwana shamba 329, lakini *target* ya mwaka unaokuja vile vile na *target* ya mwaka 2021 vile vile. Sasa tukasema hawaajiriwi, hawapungui huku kwengine, nataka niombe ufanunuzi wa kutosha ili niende nao sambamba.

Lakini jengine ni tani za mbolea zilizosambazwa kitakwimu kwa wakulima, 2017/2018 tulisambaza tani 700, lakini 2018/2019 tani 600 na *target* za miaka yote mitatu ya mbele mpaka 2021 ni 600. Je, wakulima hawaongezeki au haitumiwi ipasavyo mbolea ile nataka kujua.

Lakini kuna kiashiria cha idadi ya hekta za mpunga. Mheshimiwa nakwenda tena idadi ya matrekta yaliyotengenezwa mwaka 2017/2018 yametengenezwa matrekta 23, mwaka 2018/2019 matrekta 30 lakini na *target* za mbele za miaka mwili yote matrekta 30. Nataka kupata ufafanuzi tu kwa haraka najua nitakukwaza siwezi kumaliza vitu vyote kwa pamoja, lakini nataka kujua tu idadi ya hekta zilizopandwa mikoko.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kiashiria chengine cha LO1 (06) hapa wanasema 2017/2018 hekta 40 lakini *target* ya mwaka unaokuja ni 15, 15. Nataka kujua tu zinapungua vipi hatupangi tena au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda tena kwenye kitabu kikubwa naona nitachukua muda wako mwingi simalizi lakini hii naomba tu kuja kupata ufafanuzi wa vifungu naomba nivitaje vifungu tu. Kifungu cha PL, fungu LO1, ukurasa wa 28, kifungu cha PL0101, kifungu kidogo cha L01010101 kuweka miundo mbinu ya umwagiliaji maji ningeomba kupata ufafanuzi, na kifungu kidogo cha HL01010103, matengenezo ya visima vya pampu ningetaka kupata ufafanuzi. Lakini vile vile na kifungu SL010103 maendeleo ya huduma ya kilimo ni kutoa ushauri wa kitaalamu. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi. Lakini kifungu cha mwisho kabisa ni cha fungu la HL01010502 nilikuwa nataka nipate ufafanuzi na haya mengine naomba nipeleke kwa maandishi uniridhie Mhe. Mwenyekiti. Nakushukuru sana na siungi mkono hoja hata moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mohamed Said Mohamed, sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata nafasi hii na mimi ya kuchangia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu dakika zangu ni kidogo itabidi niende moja kwa moja kwanza kumpongeza Mhe. Waziri, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi moja kwa moja niende kwenye suala la Programu ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara kwa kumalizia uwekaji wa umeme pamoja na miundo mbinu katika bonde la Kirundunda eneo la Bumbwisudi. Eneo hilo kwa muda mrefu wananchi walikuwa wana tatizo la kuwekewa miundo mbinu lakini sasa hivi tayari miundo mbinu hiyo imekamilika kwa hivyo niipongeze sana wizara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo pia niendelee kuipongeza wizara pamoja na *TASAF* kwa kusimamia bonde la Kizimbani ya popo kuweza kuanzisha miundo mbinu ya umwagiliaji, lakini pia kupatiwa pampu ya umwagiliaji. Niwaombe tu wizara waendelee kusimamia ili na bonde hilo liweze kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili la umwagiliaji maji bado kuna changamoto, changamoto iliopo sasa hivi zaidi ni ya miundo mbinu. Kaka yangu Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kasema kuna fedha nyingi ambazo ziliwekwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, lakini bado miundo mbinu ni tatizo katika maeneo ya umwagiliaji maji. Kwa sababu miundo mbinu wanatengeneza ya udongo na sasa hivi imepitwa na wakati, maji unaweza kufungua eneo la kwenda kwa mda wa dakika kumi yakenda masaa mawili yanavuja njiani hayafiki kule ambapo yanakusudiwa. Kwa hivyo, niombe sana wizara kwa kupitia hizo fedha ambazo wanazo watengeneze miundo mbinu ya matofali ili maji yaweze kuwafikia kwa haraka wakulima. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika ukulima huu sasa hivi kumekuwa na changamoto kubwa ya maradhi ya mpunga. Nimuombe tu Mhe. Waziri pamoja na wataalamu wake wawe wanafanya ziara mara kwa mara kwenye mabonde haya, unaweza ukenda leo mpunga ukaukuta uko katika hali ya kawaida kesho ukenda mpunga wote umeshabadilika. Kwa kweli wakulima wanakuwa wameshapoteza nguvu nyingi lakini unakuwa wakati mwengine unashindwa kupata ushauri wa kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo linajitokeza kama changamoto kwenye visima vile vya umwagiliaji maji kwa sasa walinzi anakuwa mtu mmoja tu kwenye kisima kimoja, mlinzi yule ni binaadamu anaweza akaumwa akapata tatizo la aina yoyote, kwa hivyo akikosa kwenda kwenye kisima kile watu wanaiba vifaa, na ushahidi upo na kuna baadhi ya visima tayari wameshaiba vitu mbali mbali. Niiombe wizara katika ajira wanazotoa basi waajiri na walinzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo kuna ubovu wa ofisi zile ambazo wenyewe wataalamu wakitoka mjini au maeneo mbali mbali wanakwenda huko, majengo yale yote ni mabovu hayaridhishi hata Mhe. Waziri na wenzake wakifanya ziara hawana pahala hata kupata kile kitabu cha wageni cha kuweka saini. Kwa hivyo, niombe katika fedha hizi angalau wakakarabati japo mabanda mawili matatu waweze kupata.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ni upatikanaji wa mbolea wenzangu wamezungumza na kamati imesema, sasa hivi hata hiyo mbolea ukiipata ina bei tofauti, kuna baadhi ya wakulima wanauziwa bei shilingi 11,000/-, kuna baadhi ya wakulima wanauziwa bei shilingi 26,000/-. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie hizi bei kwa nini zikawa tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo jengine ambalo liko katika bonde la Bumbwisudi pampu nambari 14, bonde hilo tayari wananchi walikwishapata kazi ya kuwekea miundo mbinu na tulikuwa tunamwagilia lakini kwa bahati nzuri au bahati mbaya wenzetu wa Shirika la Umeme walikwenda kuweka laini mwituni. Kwa hivyo, watu wameiba vifaa na *transformer* ile imechukuliwa na watu wa Shirika la Umeme, kisima kile nacho watu wa umwagiliaji wamekuja kuitoa pampu hatima yake limebakia gofu. Wananchi wamepoteza nguvu nyingi na mpaka sasa hakuna matumaini.

Mhe. Waziri aliyepita alituahidi kama umeme huu utarejeshwa na wananchi watapata kulima tena umwagiliaji, lakini mpaka leo kitu hicho hakijafanyika. Nikuombe Mhe. Waziri naamini wewe ni mchapakazi, kazi hiyo unaweza ukaisimamia na umeme huo ukarejeshwa na wananchi wakapata kulima kilimo hicho cha umwagiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Programu ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mkurugenzi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika eneo hilo, lakini pia niwapongeze na walimu wa chuo hicho nao pia kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini niwaombe tu hawa wanafunzi wanapokuwepo pale chuoni lazima wapate maeneo ya kwenda kujifunza. Zamani ulikuwa ukikaa kwenye bonde la mpunga unawakuta walimu na wanafunzi wa Chuo cha Kizimbani wanakuja kwenye maeneo kuja kujifundisha kulima mpunga kwa sababu wanafundishwa darasani lakini hawaendi kule *field* kujionea wenyewe. Kwa hivyo, niombe Mhe. Mkurugenzi ananisikia na walimu wananisikia ule utaratibu waurejeshe wa kuja na wanafunzi ili kujifunza, isiwe mtu anafundishwa kulima muhogo lakini akenda kupata kishina cha muhogo badala ya macho kuelekeza juu anaelekeza chini. Kwa hivyo niombe waende kwenye *field*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nimpongeze Mhe. Rais kwa ununuzi wa haya matrekta 20, lakini pia matrekta 10 ambayo umepata na yale matrekta ambayo yameshakarabatiwa na sasa yanafanya kazi. Niipongeze serikali kwa kuwafidia wakulima bei, bei ya hekta moja ilikuwa iwe juu lakini kwa bahati nzuri tunalimiwa kwa shilingi 26,000/-, niipongeze serikali kwa kubeba hiyo gharama. Lakini niseme tu kwamba wajitahidi wakulima walimiwe mapema, ukilimiwa mapema unapata mafanikio mazuri, ukichelewa kulimiwa mafanikio yake yanakuwa mabaya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka jana Mwenyezi Mungu alijaalia tulipata mafanikio makubwa ya mavuno, lakini kwa mwaka huu hali mpaka sasa hivi inaonekana ni nzuri. Lakini bado niendelee kusisitiza maradhi yametukabili ya mpunga, kwa hivyo wizara kwa kupitia wataalamu wake wajitahidi kutembelea kwenye mabonde ya mpunga. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nizungumzie suala zima la madereva wa hayo matrekta, kweli matrekta yamepatikana lakini madereva ni kidogo, haidhuru katika taarifa yao wamesema wako madereva sasa hivi wanapata mafunzo. Lakini kwa mwaka jana uliopita dereva wanaanza

kazi saa sita za mchana kama alipangiwa siku moja alime hekta 20 analima hekta 10 na kesho anakuja tena saa sita za mchana. Hiyo inasababishwa na wao wenyewe wizara kwa sababu dereva anafanya kazi mchana kutwa lakini hawamlipi *overtime*. Kwa hivyo, niombe madereva hawa ambao wanafanya kazi za kilimo toka asubuhi mpaka jioni ile haki yao ya msingi ya kupatiwa *overtime* wao wanapewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye Programu ya Maendeleo, Rasilimali, Misitu na Mali Zisizorejesheka. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mkurugenzi kwa kazi nzuri ambayo wanafanya kwa sababu sasa hivi hata dereva kama anapakia mbao za wizi akizipeleka mjini khofu yake kubwa ni Mkurugenzi. Niseme tu kuwa askari wa misitu wanafanya kazi nzuri, lakini wakati mwengine inawezekana kwa utaalamu waliokwishakuwa nao hao ambao wenye misumeno ya moto, wanafanya kazi saa kumi na moja za alfajiri ikifika saa moja wameshamaliza kazi zao. Kwa hivyo, niwaombe tu Mkurugenzi yeye na timu yake wafanye kazi nzuri kwa sababu sasa hivi hali sio nzuri, miti inakwatwa tena miti ambayo ina matunda.

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi walipokuwa wanafanya kazi ya kudhibiti mchanga ilikuwa askari wanafanya kazi nzuri, lakini sasa hivi minazi inamalizika, ukenda kwenye maduka ambayo wanauza mbao za minazi zipo zinaonekana. Kwa hivyo, wakati ushahidi upo mtu akamatwe ili kunusuru hii minazi ambayo karibu itamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nizungumzie suala zima la eneo ambalo limeanzishwa kwa ajili ya utalii *Zanzibar City Park* liliopo Dole eneo la Dunduke. Eneo hili limezungukwa na vijiji vingi karibu shehia nane na vijiji hivi vina wakulima, wakulima hawa mle mna kimapunju wanaharibu mazao yao. Wenzetu wamezungumziwa kuwa huko wanalipwa fidia, mimi katika vikao vyangu ambavyo tunatembelea kwenye jimbo wakulima nao wanalalamika kuwa mazao yao yanaharibiwa lakini hawapati fidia kwenye eneo hili. Niombe sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie na wale wananchi ambao wanaharibiwa mazao yao kwenye maeneo hayo watapata fidia gani katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Nizungumzie suala zima la mifugo. Nimpongeze Mkurugenzi anayeshughulikia suala zima la mifugo, lakini nimuombe tu wananchi wangu wa Shehia ya Dole tayari wana mabanda wameshajenga wameyatengeneza vizuri wametoa gharama kubwa na wao bado hawajapata ng'ombe wa kuweka bandani. Eneo moja tayari limeshafanikiwa lakini eneo moja bado hawajafanikiwa kupata hao ng'ombe. Kwa hivyo, niwaombe tu wakati wowote wanapopata nafasi ya kuwapata hao ng'ombe na wao waweze kupatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niseme na mimi naipongeza Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kazi zake nzuri wanazozifanya, lakini pia niunge mkono hoja yao kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Masoud Abrahman Masoud kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha kikao nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji karibu 12 na tukizingatia kesho ni siku ya Ijumaa na sifikirii kama wachangiaji wote hawa wanaweza wakapata muda huo wa kutosha wa kuchangia. Kwa hivyo, nilitaka nitoe indhari kwa wale ambao hawajachangia na wameleta orodha yao, basi pia wajiandae kwa kuchangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote mliochangia na wale waliokuwa bado hawajapata nafasi ya kuchangia, lakini niwashukuru kwa utulivu wenu na niipongeze wizara na watendaji wake wote pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wa hotuba zao. Sasa naomba niakhirishe kikao hichi mpaka kesho tarehe 01/06/2018 saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

(*Saa 8:54 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 01/06/2018 saa 3:00 asubuhi)*